**6 NOVEMBA, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 6 Novemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa 17, Kikao cha Saba.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulize swali lake.

Na. 107

**Meneja Rasilimaliwatu wa Kiwanda cha Dangote**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Meneja Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Simenti cha Dangote Mtwara ni raia wa Nigeria wakati sheria inamtaka awe Mtanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko yanayotolewa na Mheshimiwa Mbunge yalishafika katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na kufanyiwa kazi. Kwa kuzingatia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni, Sura ya 436 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 10 ya Mwaka 2022, Ofisi ilifanya Ukaguzi Maalum katika Kiwanda hicho tarehe 23 na 24, Septemba, 2024, ili kujiridhisha na ukweli wa malalamiko haya ya utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa ujumla na Serikali imethibitisha malalamiko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali, tutaendelea kushughulikia suala hili na pindi litakapokamilika, hatua stahiki zitachukuliwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, suala hili ni la muda mrefu, zaidi ya miaka mitatu sasa hivi huyu *HR* bado yuko hapa ambaye ni mgeni. Swali la kwanza; ni kigugumizi gani ambacho Serikali inakipata inashindwa kumwondoa huyu mtu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; naomba Mheshimiwa Waziri tufuatane twende kwenye Kiwanda cha Dangote akaone uhalisia wa jambo hili ambalo tunalizungumza. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Seleman Mtenga. Kwanza, ninakiri na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Mtenga, jambo hili amelifuatilia sana na kwa kweli

kulikuwa kuna uvunjifu wa sheria ambayo tulibaini hizi sheria zinazohusiana na masuala ya kazi na staha. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Mbunge ajue siyo kwamba tuna kigugumizi kilichosababisha kuchelewa kidogo ni kwa sababu pia kulibainika kuwepo kwa tuhuma za uvunjaji wa Sheria ya Mwenendo ya Makosa ya Jinai, Sura ya 16, ambayo Sheria hii ya Kanuni za Adhabu inaeleza makosa ya jinai ambayo yalitendeka na tayari Polisi wanaendelea kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mamlaka ya uhamiaji *(immigration)*, pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaendelea kuyashughulikia kwa sababu tuliona tukichukua hatua haraka maana yake kuna makosa mengine kama ni ya jinai aliyatenda, maana yake sheria itakuwa haijatenda haki hasa kwa wale waliokuwa wametendewa. Kwa hiyo, tuliona kwamba ni vizuri tuhakikishe mashauri yote na tuhuma zote zinafanyiwa kazi na kisha kuchukua hatua pale ambapo tutakuta kuna changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kwenda Mtwara, tuko tayari Mheshimiwa tutafanya kazi hiyo ili kuhakikisha kwamba Watanzania na Wanamtwara wote wanapata manufaa kwenye uwekezaji ambao unawekwa hapa nchini.  Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 108

**Kuweka Mazingira Wezeshi kwa Wataalam Wabobezi Nchini**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO K.n.y. MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mazingira gani ya kuwavutia wataalam wabobezi kutoka nje na wangapi ni Watanzania na wangapi wanafanya kazi nje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa ajira za raia wa kigeni zinaratibu ipasavyo, Serikali ilitunga Sheria ya kuratibu ajira za wageni Na.1 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016. Sheria hii imeainisha vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa katika kutoa vibali vya kazi ikiwemo sifa za kielimu, ujuzi na uzoefu wa kazi. Aidha, Sheria hii imetambua Daraja D la Kibali cha Kazi kuwa Daraja la Wataalam wageni ambao ujuzi wao ni adimu katika soko la ajira la ndani ya nchi. Wataalam hawa wanahusu kada ya afya kwa ujumla wake, Walimu na Wahadhiri wanaofundisha masomo ya Hisabati na Sayansi, wataalam wa mafuta na gesi na watafiti wa kisayansi. Daraja hili limepewa nafuu ya ada ya maombi ya kibali cha kazi tofauti na daraja linalohusu wataalam wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia Sheria tajwa, Wataalam Wabobezi ambao hawajaainishwa kulingana na madaraja, wanapewa vibali vya kazi ikiwa watatambulishwa na mamlaka zinazohusika. Kwa mfano, wageni wanaotekeleza miradi ya Serikali ni lazima watambulishwe kwa Kamishna wa Kazi na mamlaka za Serikali zinazotekeleza mradi au kupitia usajili wa wageni hao katika bodi ya kitaalam, kama vile Wizara ya Elimu, Bodi ya Wahandisi na bodi nyinginezo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali inatumia njia gani ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanapata kazi nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha ajira zaidi zinapatikana ili kufikia zile ajira milioni nane ambazo zimeainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwamba Serikali inatumia njia gani kuweza kuhakikisha kwamba ajira za watanzania zinapatikana nje ya nchi. Moja ni kuingia makubaliano kati ya nchi na nchi *(bilateral agreements)*. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaingia makubaliano na nchi tatu sasa na tunaendelea, makusudio yetu ni kuhakikisha tunaingia kwenye makubaliano na nchi nane, zikiwemo Nchi za Umoja wa Nchi za Kiarabu ili kuweza kuhakikisha Watanzania wanafanya kazi huko na wameshakwenda kwa awamu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, tunatumia Balozi zetu. Mabalozi wana jukumu la kuhakikisha wanatafuta fursa za ajira kwa ajili ya Watanzania kwenye hayo maeneo na pale zinapotangazwa Watanzania wenye sifa kupitia Balozi na Wizara ya Mambo ya Nje tumekuwa tukiwasiliana na Wizara ya Kazi ili kuweza kuhakikisha fursa hizo zinapatikana. Hatua ya tatu ni umoja wa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi wakiwemo kwa umoja ambao ni maarufu *Diaspora*. Nayo imekuwa ni sehemu ya kuweza kutusaidia kuweza kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni juhudi binafsi za Watanzania wenyewe kulingana na visomo, sifa na vigezo kama ni wanamichezo, lakini pia kama wana vipawa au vipaji mbalimbali wamekuwa wakipata ajira nje ya nchi; na

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni Taasisi za Elimu, Wizara na Vyuo Vikuu imekuwa katika masuala ya kufanya tafiti, Watanzania wamekuwa wakipata nafasi kwenda nje ya nchi kwenda kufanya kazi hizo ikiwemo na masuala mengine ya michezo na wadau wa maendeleo kwa mfano chini ya *United Nations*, zile *agency* zake Watanzania wamekuwa wakipata kazi

na mojawapo tunaishukuru zipo kazi za kugombea Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ni moja ya kielelezo cha Watanzania ambao wanaendelea kupata fursa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na jitihada za Serikali katika kuhakikisha tunafikia azma ya kufikia ajira milioni nane. Lengo la Serikali na *target* yetu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maagizo mahususi ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya utekelezaji wa maagizo hayo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wa Nchi, tumeweka mpango wa kuhakikisha kwamba kila mwaka tunapata ajira milioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano 2024 kwa mwaka huu tu kuanzia mwezi Januari mpaka mwezi Julai kwa *administrative data* tulizonazo, tayari tumepata ajira za Watanzania 607,475 pia tunaendelea kufanya utafiti kupitia *National Bureau of Statistics* kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na *World Bank*, tutafanya *Integrated labour Force Surv*ey ili kuweza kupata takwimu halisi za ajira ambazo zinahitaji takwimu pamoja na *employment earning survey* ambayo tutaifanya kwa pamoja katika mwaka huu wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, nimekuona.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameyatoa, lakini kuna changamoto, tunajua kwamba vijana na watanzania wengi hawana ajira, lakini wana sifa nyingi ya kuweza kufanya kazi labda nje ya nchi. Tunaona nchi mbalimbali zimekuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba wanaangalia zile fursa zilizopo nje ya nchi na kuzitangaza na kutafuta watu ambao ni *competent* wa kuweza kufanya kazi hizo. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaziangalia hizo fursa na kuwatangazia na kuwatafuta Watanzania wenye sifa hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kama nilivyoeleza nikiwa najibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa aliyemaliza kuuliza swali lake, Mheshimiwa Esther Malleko, ni kwamba mkakati wa Serikali upo katika pande zote. Tunaingia makubaliano ya kimataifa katika fursa za ajira kulingana na kazi za kibobezi na utaalam ambazo zinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknoloja ya Habari, vivyo hivyo tayari tumeshaanza kuweka mpango maalum kwa kupitia Kitengo cha Ajira, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (*TaESA*), tunatafuta ajira ambazo zinatangazwa kimtandao na tunatafuta Watanzania ambao tunao kwenye kanzidata kupitia Kitengo cha Ajira cha Ofisi ya Waziri Mkuu, kuwapa nafasi ya kuweza kuomba nafasi hizo na kusaidiwa kuanzia mafunzo ili kuhakikisha kwamba wanapata zile ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo Mheshimiwa Tendega hata katika upande wa ajira ambazo ni za kitaalam na ubobevu, nchi nyingi zimeonesha utayari wa kufanya kazi na Tanzania na tunapokwenda kwenye vikao mbalimbali vikiwemo vya *AU*, *SADC*, Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza sana ule mchangamano na Mawaziri wakati wote akiwemo Waziri wangu wa Nchi, Mheshimiwa Ridhiwani, amekuwa ni sehemu yake ya kwenda kwenye vikao vile ili kuweza kutafuta fursa mbalimbali ambazo zipo huko na Mabalozi wameendelea kutupa *feedback*. Kwa hiyo, tupo kwenye hatua nzuri kwa kweli na tunatambua, tunataka kama Taifa kupata fedha za *remittance* zitakazoongeza nguvu kwenye bajeti. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amour.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali langu moja dogo ambalo linahusiana na masuala ya uwakala wa ajira hasa kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa nini *TaESA* ndiyo wakala pekee kisheria kwa upande wa Tanzania Bara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umemwelewa? Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kumwelewa lakini sitaki kumwekea maneno labda pengine alifafanue ili niweze kulijibu vizuri zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amour fafanua ili Mheshimiwa Waziri aweze kuelewa swali.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Wakala wa Ajira kwa upande wa Tanzania Bara, kisheria tuna wakala mmoja tu ambaye ni *TaESA,* wale wote waliobaki maana yake ukitazama wao wanapata nafasi za ajira kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria maana yake nafasi zote lazima zipitie *TaESA*. Sasa kwa nini kuna utaratibu wa aina hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni swali zuri ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza. Ukweli ni kwamba tuna Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na tuna sheria ambazo zinahusiana na Utumishi wa Umma, lakini katika maana ya Wakala wa Ajira, tuna *TaESA* kama anayesimamia masuala ya ajira kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana ya masuala ya ajira kwa mujibu wa sheria tulizonazo kwa sasa, tunaye Kamishna wa Kazi ambaye ndiye msimamizi na mratibu wa kuhakikisha kwamba mikataba ya kimataifa ambayo tumeingia kama Taifa kwa maana ya kupitia *ILO (International Labour Organisation)*, lakini pia makubaliano ya kikanda na *domestic* ambayo tumekubaliana kwa pamoja na sheria zetu za ndani lazima zisimamiwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TaESA* siyo wakala pekee yake, wapo pia mawakala wengine wa ajira ambao wanasajiliwa kupitia Ofisi ya Kamishna wa Kazi ambao ni binafsi na wanafanya kazi hiyo hiyo sambamba na Serikali. Moja ya mawakala ambao wanafanya kazi vizuri ni pamoja na *Global Link*, ambao wanawatafutia Watanzania fursa za kwenda kusoma au kupata

ajira na taasisi nyingine na wakala nyingine. Watanzania wanaruhusiwa kwenda kusajili wakala wa utafutaji wa ajira au fursa kwa ajili ya Watanzania, kwa hiyo hilo ni suala la wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Kamishna wa Kazi pamoja na *TaESA* ni suala la kupata taarifa, kupata kanzidata ya wataalam tulionao ndani na nje ya nchi, lakini pia kuzijua *levels*, hali ya ajira ilivyo kama ni *employment*, *unemployment* ikoje ili tuweze kufanya mipango sahihi na madhubuti kuweza kuhakikisha kwamba watanzania wote wanapata fursa hizo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, aulize swali lake.

Na. 109

**Upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi Nchini**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza upungufu mkubwa wa walimu kwa shule za msingi nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiajiri walimu wa shule za msingi kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali iliajiri walimu 16,598 wa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 20 Julai, 2024, Serikali ilitangaza ajira za walimu 11,015 wakijumuisha walimu 3,370 wa shule za msingi ambapo mchakato wa ajira ukikamilika watapangiwa vituo vya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali katika Jimbo la Tabora Mjini lenye Kata 29 bado kuna upungufu wa walimu sana katika Kata hasa za nje kama Kabila, Tumbi, Itonjanda na nyingine ambazo ni Kata za nje. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; walimu wengi hawapendi kwenda vijijini na wamejazana mijini hasa kwenye shule za msingi. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba walimu wanakaa vijijini na wanaacha mchezo wa kukimbilia mjini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi kwenye Jimbo lake. Kuhusiana na swali lake la kwanza, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, kwamba tayari ajira 11,015 za walimu zimetangazwa na mwaka huu baada ya mchakato huu wa ajira basi wataweza kupangiwa vituo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge naye pia kwenye jimbo lake atapata walimu, wakiwemo walimu wa shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, naomba nimhakikishie, Serikali inatambua kwamba kuna changamoto hizi za walimu kupenda kukaa mijini. Ndiyo maana ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwaagiza wakurugenzi wote wahakikishe kwamba kwa kuzingatia bajeti wanafanya msawazo wa walimu ili kutengeneza uwiano ulio mzuri kwa kuondoa

maeneo ambayo yana walimu wengi zaidi halafu kupeleka maeneo ya vijijini ambayo hayana walimu. Kwa hiyo wakurugenzi wafanye kazi hiyo ya kufanya msawazo wa walimu hawa kwa kuzingatia bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inachukua hatua tofautitofauti ili kuhakikisha kwamba inaboresha mazingira ya kazi kwa ajili ya walimu. Serikali inajenga nyumba za walimu na inahakikisha kwamba huduma za msingi kama barabara na afya zinapatikana hadi vijijini ili kuhakikisha kwamba walimu wetu hawa wanaweza kupata mazingira mazuri ya kufanya kazi ili wasikimbilie mijini na kuacha kufanya kazi vijijini.

**MWENYEKITI:** Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa. Shule nyingi za msingi katika Jimbo la Moshi Vijijini zina upungufu mkubwa sana wa walimu na kuna baadhi ya shule zina walimu watatu. Je, Serikali ina mpango gani kutusaidia kupata walimu ili kuondoa kero hii?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwawakilisha wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la nyongeza, kwanza kabisa ninaomba nimhakikishie kwamba katika mwaka huu Serikali itapanga walimu. Tutapata walimu kwa sababu kuna ajira mpya ambazo zimetangazwa na Serikali. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika jimbo lake atapata mgao wa walimu wa shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza katika maelekezo niliyoyatoa awali, ambayo nimeyatoa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwamba wakurugenzi wote wafanye msawazo wa walimu ndani ya halmashauri zao kwa kuzingatia bajeti ili kutengeneza uwiano ulio mzuri ili maeneo ya vijijini yasikose walimu kwa sababu walimu wengi wanakimbilia mijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aziza nimekuona na Mheshimiwa Waitara utafuatia.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wako walimu wengi ambao wanajitolea na walimu hawa utakapofika wakati wa kutolewa ajira na wao wanaomba lakini hawapati ajira. Je, Serikali haioni ya kwamba wanawavunja moyo wale walimu wanaojitolea kwa sababu wanakosa ajira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumpoongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya, pia nimpongeze kwa swali lake ambalo ni la msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba hawa walimu na si tu walimu bali pia watumishi ambao wanajitolea, wanahitaji kutiwa moyo ili wasivunjike moyo kwa kujitolea halafu wakakosa ajira. Ndiyo maana Serikali ilitangaza kwamba inaandaa utaratibu mzuri wa kutazama wale watumishi na walimu ambao wanajitolea wazingatiwe zaidi na kupewa kipaumbele katika ajira. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kufanya hivyo na tayari inatengeneza mikakati ya kuzingatia wanaojitolea ili wapate kipaumbele katika ajira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hivi karibuni Serikali imetangaza ajira za walimu. Niliona watu kutoka Tarime wanaenda kufanya *interview* Mtwara kwa gharama kubwa. Wote waliokaa miaka mitano, miaka kumi waliitwa kwenye usaili. Ninataka nijue, unawezaje kuwahakikishia wale walimu ambao wamemaliza muda mrefu nyumbani kwao watapata ajira ukilinganisha na ambao juzi wametoka vyuo mbalimbali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, tayari Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa tangazo la ajira za kada mbalimbali ikiwemo walimu. Kwa hiyo, kwa muktadha wa swali la Mheshimiwa Mbunge Serikali itazingatia maoni hayo. Serikali inafanya utaratibu wake wa michakato hii ya ajira ili vijana wote waweze kupata ajira wakiwa wana vile vigezo ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kupata ajira hizi. Kwa hiyo, Serikali imepokea Mawazo ya Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala.

Na. 110

**Ujenzi wa Barabara za Kata ya Chamazi – Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini Barabara za Juhudi, Dumbalume, Kwayamba, Kwamnyani/Kwa Nyoka, Sekondari, Bakhresa/Kingugi na Kibudi/Moringe zitajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Serikali iliifanyia matengenezo Barabara ya Kibudi/Moringe yenye urefu wa kilomita 1.29 kwa gharama ya shillingi 324,722,862 kwa kujengwa kwa zege kilomita 0.5 na kuweka tabaka la changarawe kipande cha kilometa 0.3. Aidha, katika mwaka 2024/2025 kupitia fedha za 10% za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Serikali itafanya matengenezo katika Barabara za Juhudi kilomita 0.6 kwa shilingi milioni 92, ikiwemo kujengwa kwa zege urefu wa mita 200 na Barabara ya Bakhresa – Kingugi kilomita 0.8 kwa shilingi 63.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi wa *DMDP* awamu ya pili, Serikali inaendelea na usanifu wa Barabara ya Dumbalume ambayo imesajiliwa kwa jina la Zomboko – Kingugi yenye urefu wa kilomita 2.5 na itajengwa kwa kiwango cha lami katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Vilevile, Barabara za Kwayamba kilomita 0.7 na Kwamnyani/Kwanyoka kilomita 0.6, ziko kwenye mpango wa utekelezaji wa 70%, ambapo utekelezaji wake utafanyika wakati michakato yote ya utekelezaji wa 70% itakapokamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuzikarabati barabara za Kata ya Kiburugwa ambazo zimeathirika na mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Mzambarauni – Saku ulio chini ya Mradi wa *DMDP* utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa ya uwakilishi katika jimbo lake na kwa hakika mara nyingi amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa sana wa kuhakikisha kwenye jimbo lake Miradi ya Barabara hasa hizi za *TARURA* inaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake alilouliza kuhusiana na Kata hii ya Kiburugwa na hatua za dharura, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka katika mipango kurekebisha barabara hizi katika Kata ya Kiburugwa. Nimhakikishie kwamba barabara zake katika mwaka huu wa fedha 2024/2025; barabara ya *Corner Bar* – Kiburugwa – Magenge itajengwa kwa tabaka la lami, barabara yake ya Zomboko – Kigungu itajengwa kwa tabaka lami; Zahanati – Kingugi itajengwa kwa tabaka la zege, Kizuiani – Zahanati – Kiburugwa itajengwa kwa tabaka la zege na Mbagala – Viwandani zote hizi zitaweza kujengwa kwa kiwango cha zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Manganya ambalo limewekwa katika mipango ya muda mrefu, limejumuishwa katika miradi itakayotekelezwa kwenye Mradi wa *DMDP Two*. Nimhakikishie kwamba sasa hivi tumefikia katika mchakato wa manunuzi na punde mkandarasi atakapopatikana, basi daraja lake hili litaweza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika maswali yake yote haya mawili Serikali ipo katika michakato ya utekelezaji na wananchi wake wakae mkao wa kupokea kwa sababu fedha zipo na tayari mipango ipo, ni kukamilisha tu utaratibu kwa ajili ya utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei nilikuona, halafu Mheshimiwa Saashisha halafu tutaendelea.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Serikali inaweza ikawahakikishia wananchi wa Vunjo kwamba Barabara za Uchira – Kisomachi – Kolarie na Pofo – Mandaka – Kilema zitatengewa fedha ya kutosha kuzikamilisha

kwa kiwango cha lami kwa sababu ni ahadi za viongozi wa juu wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya katika jimbo lake. Kuhusiana na swali lake, ninaomba nimhakikishie kwamba ahadi za viongozi wakuu ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanyia kazi kwa upekee kabisa ujenzi wa barabara hii, na tutafanya ufuatiliaji mimi na yeye Mheshimiwa Mbunge tutakuwa tunawasiliana mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba barabara hii muhimu ambayo ameitaja ijengwe ili iwe ina hadhi nzuri na iweze kuwanufaisha wananchi wa jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kutujengea Barabara ya Kwa Sadala kwenda Longoi kupitia Mradi wa Wizara ya Kilimo kwa zile barabara ambazo zinaelekea kwenye masoko. Barabara hii inaelekea Soko la Kwa Sadala. Mwaka jana iliwekwa kwenye bajeti lakini haikufanyika na mwaka huu pia. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa na taa juu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi na hasa kwa sababu swali hili tayari ameshakuwa akiliulizia mara kwa mara na nilishawahi kumjibu hapo awali. Niendelee kusisitiza kwamba msimamo ni ule ule; Serikali inatafuta fedha na fedha zikipatikana itahakikisha

kwamba inakuja kujenga barabara hii ambayo ni muhimu sana kiuchumi katika jimbo lake na itaijenga barabara hii kwa tabaka la lami na kuweka taa juu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge akae mkao wa mapokeo kwa kuwa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii muhimu kwenye jimbo lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala nilikuona, atafuatia Mheshimiwa Bishop Gwajima.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri wamekuwa wakiendelea kutoa ahadi kwenye Barabara ya Chemba – Soya na wanatenga bajeti ambayo hata hivyo hawaileti. Je, ni lini Serikali watakwenda kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya kutoka Chemba mpaka Soya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi. Ninaomba kuendelea kumhakikishia kwamba Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara na hasa barabara zetu hizi za *TARURA*. Ndiyo maana utaona katika Serikali ya Awamu ya Sita, bajeti ya *TARURA* imeongezeka mara dufu kutoka shilingi bilioni 275 kwa mwaka mpaka sasa kila mwaka inatengwa shilingi bilioni 710.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa awamu imekuwa ikizifikia barabara mbalimbali nchi nzima. Dhamira ya Serikali ni kuja kuifikia hii barabara na kuijenga ili iwe ina hadhi nzuri na iweze kuwanufaisha wananchi kutoka katika eneo analoliwakilisha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo kazini na itakuja kufika katika barabara hii na kuijenga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Bishop Gwajima* nimekuona.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zinazounganisha shina kwa shina, kata kwa kata na mtaa kwa mtaa kwenye Jimbo la Kawe hazipitiki kabisa na ziko kwenye hali mbaya. Je, Serikali ina mpango gani wa ziada na dharura wa kuzi-*repair* barabara zile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, kwa kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba miundombinu bora ya barabara na hasa hizi za wilaya zinapatikana katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba, fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam zipo. Sote tunafahamu kwamba kuna Mradi wa *DMDP Two* ambao ni mradi wenye fedha nyingi sana ambazo tayari zimepatikana; zimetafutwa na Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zote zitakuja kufikiwa zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimahususi kabisa nitumie nafasi hii kuendelea kumkumbusha Mkurugenzi na Meneja wa *TARURA* wa wilaya na wa mkoa waweze kufanya usimamizi wa mitambo ambayo Mheshimiwa Mbunge wameinunua katika jimbo lao na kwenye halmashauri yao ili ziweze kwenda kufanya uchongaji wa barabara hizi za mitaa anazozingumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba Mkurugenzi, Meneja wa *TARURA* wa ngazi ya Mkoa na Wilaya wanafanya usimamizi mzuri wa kutumia mitambo hii ili ikatumike kuchonga barabara hizi za Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na Mheshimiwa Mulugo nimewaona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Mwaka 2015, Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kutujengea kilomita tano kwa kiwango cha lami pale Mji wa Usa *River*. Mwaka 2020 tena akaahidi kujenga Barabara ya King'ori kuanzia Malula Kibaoni hadi Ngarenanyuki. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa kwa sababu mara nyingi amekuwa akifanya ufuatiliaji wa barabara katika jimbo lake na barabara hizi za ngazi ya wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimhakikishie kwamba barabara zote hizi mbili alizozitaja ziko kwenye mpango. Serikali inatafuta fedha ili kuhakikisha kwamba inazifikia na inakuja kutekeleza ahadi na kuzijenga barabara hizi ili ziweze kuwanufaisha wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Nami niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara ya kutoka Chang'ombe – Totowe mpaka Magamba Jimbo la Songwe ni barabara inayosimamiwa na *TARURA*. Mwezi Septemba wakati mwenge umekuja waliweza kuzindua barabara hiyo, lakini mpaka sasa mvua za vuli zimeanza mkandarasi huyo amekimbia na sijajua kama alipewa *advance* na Serikali. Naomba Serikali itoe tamko juu ya barabara hiyo kwa sababu wananchi wanashindwa kupita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, naomba mimi na yeye tuzungumze baada ya kipindi hiki cha maswali ili tuweze kufanya ufuatiliaji kujua hatma ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba inafikia mtandao mpana zaidi wa barabara zetu hizi za *TARURA* kwa sababu barabara hizi za ngazi za wilaya ni barabara ambazo zina manufaa makubwa sana kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tutalifanyia kazi; mimi na yeye tutazungumza ili tuweze kupata muafaka wa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 111

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Pagwi – Kilindi**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Pagwi – Kilindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Pagwi, Halmashauri ya Kilindi umeanza kupitia nguvu za wananchi wa Kata ya Pagwi, ambapo ujenzi wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje umeanza na umefikia hatua ya kumwaga jamvi, ambapo wananchi wamechanga jumla ya shilingi milioni 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Pagwi. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Pagwi ni kubwa katika Wilaya, ina jumla ya vijiji zaidi ya saba. Hiyo shilingi milioni 22 aliyoitaja ni mjumuiko wa michango ya wananchi katika vijiji hivyo, kwa maana hali nim baya sana. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja ya kuharakisha kupeleka hiyo shilingi milioni 100 kwa sababu yale *material* yaliyopo pale yanaoza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; hali iliyopo kwenye Kata ya Pagwi ni sawasawa kabisa na hali iliyopo Masagalu. Tunaomba Kituo cha Afya Masagalu ambacho Serikali ilipeleka shilingi milioni 100 mwaka 2018 ipeleke tena shilingi milioni 100 ili kituo kile kiweze kufanya kazi na *investment* ambayo imeshafanywa na Serikali iweze kuleta tija kwa wananchi wa Kata ya Masagalu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza

kuwapongeza wananchi wa Kata ya Pagwi katika Jimbo hili la Kilindi kwa namna ambavyo wameonesha juhudi zao katika kuchangia nguvu zao kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Pagwi. Hiyo ndiyo ndiyo sera ya mpango wa maendeleo ya afya ya msingi; kuweka nguvu za wananchi na Serikali inachangia nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mwanaisha Ng'azi Ulenge, kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka fedha mapema iwezekanavyo; na nimhakikishie kuwa bajeti hii ya 2025/2026 ni *tentatively,* lakini tuna uwezo wa kutafuta fedha kupitia kwa wadau mbalimbali na kuona namna nzuri ya kwenda kukamilisha kituo hiki mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kituo cha afya cha kata hiyo ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ambacho kilipelekewa fedha shilingi milioni 100, mwaka 2018, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafuatilia tuone miundombinu inayopungua na fedha inayohitajika ili kwa haraka tuone kama tutapata fedha mapato ya ndani tupeleke tukamilishe. Kama itahitajika fedha kutoka Serikali Kuu tupeleke ili tukamilishe kituo hicho, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe nilikuona, atafuata Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tarehe 23 Julai, 2017 tulifanya mkutano kwenye Kata ya Nanganga tukiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na alitoa ahadi ya ujenzi wa kituo cha afya baada ya wananchi kuomba. Pia, tulifanya tena mkutano tarehe 20, Oktoba 2020 na Mheshimiwa Rais alifanya mkutano tarehe 18 Septemba, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Julai mwaka huu vilevile Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Ndugu Emmanuel Nchimbi, alifanya mkutano kwenye kata hiyo na kumkumbusha Mheshimiwa Mchengerwa kuhakikisha fedha hizo zinakwenda kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nanganga. Ninataka

kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni nini kinakwamisha utekelezaji wa ahadi za viongozi wakubwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nawakumbusha, jitahidini maswali kwa ufupi ili mpate wengi zaidi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kutumia nafasi hii kumthibitishia Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kwamba maelekezo ya viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa miradi hiyo. Tunatambua kwamba eneo hilo la Kata ya Nanganga limeahidiwa na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa na Katibu wa Chama pia. Ninaomba nimhakikishie kwamba tayari tumekwishaingiza kwenye mpango wa *World Bank* kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Nanganga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi atafuatia Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Martha Mariki ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kile Kituo cha Afya cha Bweri ni kituo ambacho hakina hadhi kabisa ya kuitwa kituo cha afya. Nimekiombea fedha kwa muda mrefu lakini kila leo imekuwa ni ahadi. Je, ni lini sasa kituo hicho kitapata fedha ili kiweze kuwa kama vituo vingine vya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Bweri kina miundombinu pungufu na ya zamani na kinahitaji kuongezewa

miundombinu ili kiweze kukidhi haja ya kutoa huduma bora za kituo cha afya. Ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge Manyinyi kwamba kama Wizara tulifanya taratibu za kuainisha vituo vya afya chakavu na vyenye upungufu wa miundombinu vyote. Tayari tunaendelea na ukarabati wa hospitali 61 za halmashauri na tunaelekea kuanza ukarabati na upanuzi wa vituo vya afya ambavyo vina upungufu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Kituo cha Afya cha Bweri kitapewa kipaumbele, kitapanuliwa ili kiweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Gitting ni kongwe na ya muda mrefu yenye wakazi wengi. Ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika kata hiyo ya Giting, Wilaya ya Hanang? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Asia Halamga kwamba tumeweka utaratibu wa kutambua kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Ninafahamu katika Jimbo la Hanang wameshawasilisha kata ya kimkakati ikiwa kipaumbele na ninafahamu kata hiyo ya Gitting pia ni kipaumbele cha kata zilizopo katika Jimbo la Hanang. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imepokea ombi hilo na itamwelekeza Mkurugenzi kuleta taarifa rasmi ili tuanze kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo cha afya katika kata hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Martha Mariki, Mheshimiwa Shamsia Mtanda atamalizia.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kata ya Ilangu ni kata ya kimkakati na tayari wananchi wameshaanza kujichangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Ilangu. Je, ni lini Serikali itawa-*support* wananchi hao kwa kuwatengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Ilangu, Wilayani Tanganyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Sita ni sikivu na inathamini na kuweka kipaumbele kikubwa sana kwenye Sekta ya Afya. Ndiyo maana, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari vituo vya afya zaidi ya 650 vimejengwa, vikiwemo vituo vya afya katika Jimbo na Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Martha Festo Mariki, kwamba Serikali imetambua juhudi za wananchi katika kata hiyo na ninamhakikishia kwamba tutatenga fedha kupitia mapato ya ndani na Serikali Kuu kwa ajili ya kuendelea kukamilisha kituo hicho kwa awamu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikutaja Mheshimiwa Shamsia Mtamba.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea fedha, shilingi milioni 600, kwa ajili ya umaliziaji wa Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya cha Mkunwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii kumhakikishia

Mheshimiwa Asia kwamba tunatambua tuna uhitaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Kata ya Mkunwa na tayari alishaleta hoja hiyo Serikalini mara kadhaa. Tayari tumeshaingiza kwenye mpango mkakati wa kutafuta fedha na kwenda kutekeleza ujenzi wa kituo hicho. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie yeye na wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwamba Serikali inalifanyia kazi na tutakwenda kukamilisha kituo kile cha afya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naweka marekebisho, huyo ni Mheshimiwa Shamsia siyo Mheshimiwa Asia. Mheshimiwa Dkt. Kyombo, nimekuona.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa vituo vya afya ndani ya Wilaya ya Missenyi. Hata hivyo, Kata ya Mtukula ambayo iko mpakani na Nchi ya Uganda na ambayo imekua kibiashara katika eneo hilo kwa kweli wananchi ni wengi na imekuwa katika hadhi ya kimji, lakini inahudumiwa na zahanati. Je, ni lini sasa Serikali itaona ni muda muafaka wa kutenga na kutupatia bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Mtukula? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba eneo la Mtukula ni eneo ambalo lina wananchi wengi. Tumewahi kufanya ziara na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo la Nkenge pale Missenyi - Mtukula, tuliona idadi kubwa ya wananchi na kwa kweli kuna uhitaji wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Missenyi kuainisha eneo lenye ukubwa usiopungua angalau ekari 15 na kuleta maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ili iingizwe kwenye mpango wa vituo vya afya vya kimkakati na tuweze kuona namna ambavyo tutaweza

kujenga kwa awamu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na pia kupata fedha kutoka Serikali Kuu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana. Ninawashukuru Naibu Mawaziri wote wawili kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, Mbunge wa Amani, aulize swali lake.

Na. 112

**Kuongeza Wigo wa Biashara ya Hewa Ukaa**

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wigo wa biashara ya hewa ukaa ili kupunguza uharibifu wa ukataji wa misitu nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni ili kuhamasisha uhifadhi wa mazingira na kupunguza uharibifu wa ukataji misitu nchini ambapo hadi sasa jumla ya miradi 63 ya biashara ya kaboni kupitia Sekta ya Kilimo, Nishati, Misitu, Mifugo na Usimamizi Wa Taka imesajiliwa. Kati ya miradi iliyosajiliwa kupitia Sekta ya Misitu, miradi minne inahusisha shughuli za upandaji miti, miradi 20 ni kwa ajili ya kupunguza uharibifu na upotevu wa misitu na miradi mitano ni kwa ajili ya kurejesha uoto wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) ambao unahamasisha matumizi ya nishati safi za kupikia ikiwemo gesi asilia, nishati jadidifu, mkaa mbadala na umeme

ambazo zinaweza kuchangia katika biashara ya kaboni na kupunguza matumizi ya kuni na ukataji wa misitu. Vilevile, Serikali imeandaa na inatekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu 2024 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu (2024 – 2034) ambapo imeweka mikakati ya kuhamasisha matumizi ya hatifungani za buluu na biashara ya kaboni katika shughuli za rasilimali za Uchumi wa Buluu. Lengo kuu ikiwa ni kuongeza wigo wa biashara ya kaboni nchini ili kuimarisha uhifadhi wa mazingira. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa miongoni mwa vyanzo vya upatikanaji wa hewa ya ukaa ni misitu asili. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kutunza misitu asili ili kuongeza pato la Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanza kunufaika vipi na biashara ya hewa ya ukaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdul, Mbunge na mtumishi wa wananchi wa Amani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua fursa hii kwa kumpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya akiwa jimboni. Iko mipango au mikakati madhubuti ambayo sisi kama Serikali tumeichukua kuhakikisha kwamba tunatunza na kuhifadhi misitu hii kama sehemu ya mapato ama vyanzo vya uchumi. Kwanza, kupitia mpango wetu shirikishi Serikali Kuu tumekuwa tunawashirikisha Serikali za Vijiji, halmashauri, Serikali za Wilaya, shehia na ngazi nyingine kwa lengo na madhumuni ya kuwashirikisha wananchi katika suala zima la uhifadhi na utunzaji wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumekuwa tunatoa elimu mara kwa mara kuelimisha wananchi namna bora ya kutunza misitu. Vilevile, tumekuwa tukisimamia sheria; ipo sheria ya misitu kwa upande wa Zanzibar na sheria inayosimamia misitu kwa upande wa Tanzania Bara. Kikubwa zaidi tumekuwa tunachukua hatua mbalimbali zikiwemo za kutoza faini na hata kutaifisha ikiwa tunakuta mkaa, kuni au vitu vingine. Kwa hiyo, ninamwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua hizo zipo, tumezichukua na tunaendelea kuzichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kweli Zanzibar tumeanza kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wanaifahamu na wanaielewa na kuanza kupata fursa zitokanazo na biashara hii ya kaboni. Kwanza, tumeanza kutoa elimu, tumekutana na Wakuu wa Mikoa, tumewapa elimu Mawaziri na Waheshimiwa Wawakilishi. Pia, tuna mpango wa kufika mpaka kwenye shehia, masheha na Wakuu wa Wilaya kuwaeleza fursa na maana ya hii biashara ya hewa ukaa ama kaboni ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pia fursa ya kuwaeleza kaboni hii kwa sababu kuna *green carbon*, *blue* na *organic carbon* na *carbon* nyingine zote tumewaeleza. Tunaamini kwa taaluma tuliyoitoa kwa upande wa Zanzibar inakwenda kunufaisha kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa tumeshaanza kuwasaidia na wameshafika hatua kubwa kutengeneza kanuni na miongozo itakayokwenda kusimamia biashara hii. Kwa hiyo, wanakwenda kunufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na biashara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa vile biashara hii ya hewa ukaa inatekelezwa chini ya Ofisi yako ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; je, biashara hii kwa upande wa Zanzibar imeanza kutekelezwa kwenye maeneo gani au wilaya na mkoa gani, maana tukiangalia sasa hivi biashara hii ni takriban miaka minne au mitano imeshaanza kuingia nchini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Usonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba biashara hii kwa upande wa Zanzibar ilichelewa kidogo. Huku tulishaanza na ndiyo maana tukasema kwa sababu biashara hii inafanywa kwenye misitu mikubwa ya asili ya vijiji na misitu kama vile ya Ngezi na Jozani, tukasema kwanza twende tukawafundishe kwa sababu ilifika wakati tukaona kuna watu hata hiyo hewa ukaa au biashara ya kaboni hawajui maana yake ni nini. Kwa hiyo, tukasema kwanza twende tukawape taaluma kwa sababu tuliona yapo maeneo ambayo wanaweza wakavuna kwa sababu misitu mikubwa inayovunwa tunayo Zanzibar ama ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, biashara hii pia inavunwa kupitia mazingira ya bahari; hiyo tunasema inaitwa *blue carbon* maana kule kuna zile *seagrass*, *seaweeds*, matumbawe na ufukwe mzuri na mikoko iliyopo karibu na bahari inaweza kuzalisha. Kwa hiyo, nawaambia tu kwamba tunaenda kuanza kulifanya hili jambo la uzalishaji na faida kubwa itapatikana kwa upande wa Zanzibar. Tuwe na subira lakini tumeshaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini aulize swali lake.

Na. 113

**Mradi wa Umeme wa *REA* kwenye Mitaa ya Wilaya ya Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Mradi wa Umeme wa *REA* kwenye Mitaa ya Tampori, Kwamtwara, Chemichemi, Chandimo, Dumi, Hachwi na Guruma – Kondoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea na kazi ya utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme katika maeneo ya vijijini na vitongojini ambapo vijiji vyote vya Jimbo la Kondoa Mjini vimeshafikishiwa umeme. Aidha, Mitaa ya Tampori na Chemichemi itapatiwa umeme kupitia mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 kwa kila Jimbo. Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* inaendelea kuratibu kazi za kusambaza umeme katika mitaa ya Kwamtwara, Chandimo, Dumi, Hachwi na Guruma kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa, vijiji vyote tayari vimeshapata umeme na vikaacha nyuma mitaa ambayo imetajwa hapo na Mheshimiwa Waziri; Mongoroma, Chandimo, Dumi, Hachwi na Kwamtwara. Sasa je, Mheshimiwa Naibu waziri atakuwa tayari akishamaliza kujibu swali aende pale kwa bosi, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambaye ndiye Waziri wa Nishati kwenda kuongea naye kuhusu namna ya haraka ya kusaidia hii mitaa na yenyewe ikawekewa umeme kwa haraka ili tuondoke kwenye mitaa na vijiji twende kwenye vitongoji kama wenzetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; yale maeneo yote yaliyofikishiwa umeme wa *REA*, mkandarasi anapoondoka anaacha *TANESCO* anaendelea kutoa huduma kwa kuwaunganishia wananchi. Sasa, kwa kuwa *TANESCO* akienda anaunganisha kwa bei ya shilingi 300,000; je, Serikali inaonaje kuiwezesha *TANESCO* na yenyewe wakati wa ujazilizi wakaendelea kutumia bei ile ile ya shilingi 27,000 ili kuweka usawa kwa wananchi wote wa mtaa au kijiji husika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Kuhusu swali lake la kwanza, mara zote Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, amewaelekeza *TANESCO* kuhakikisha wanakuwa na miradi thabiti ili wananchi waendelee kuunganishiwa umeme kwa wakati. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Nishati ambayo tunasimamiwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, tumejidhatiti kuhakikisha maeneo hayo yanapata miradi hii kwa mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge maeneo haya yatapata miradi. Tumeanza na ile mitaa miwili na ile mitaa mingine itaendelea kupata miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la ujazilizi; miradi ya ujazilizi ambayo inafanywa na Wakala wa Nishati Vijijini gharama yake ya uunganishaji ni shilingi 27,000 hata katika maeneo ya mitaa. Rai yetu ni kuendelea kuwasisitiza wananchi waunganishe umeme wakati miradi inaendelea kwa sababu gharama yake inakuwa kidogo, kwa shilingi 27,000, kuliko kusubiri miradi ikiisha na miradi ile kuhamia *TANESCO*. Kwa hiyo, kwa sababu katika maeneo haya miradi ya ujazilizi gharama yake ya kuunganisha wakati miradi inaendelea ni shilingi 27,000; Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana kuhamasisha wananchi waunganishe maeneo yao wakati miradi inaendelea kuliko kusubiri wakati miradi imeisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 114

**Serikali Kupunguza Kodi kwenye Magari yenye Mfumo wa Nishati ya Gesi**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza baadhi ya kodi ili Watanzania wengi waweze kuingiza magari yenye mfumo wa nishati ya gesi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia bajeti yake kuu ya mwaka 2023/2024 ilitoa msamaha wa kodi ya ushuru wa forodha *(customs duty)* 25% kwa injini za magari yanayotumia gesi asilia yanapoingizwa nchini. Aidha, Serikali bado inaendelea kuangalia namna ya kupunguza au kuondoa kodi nyingine za uagizaji wa magari hayo ili kuhamasisha zaidi matumizi ya gesi asilia. Vilevile, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali za kuhamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye viwanda vinavyo tengeneza vipuri vinavyotumika katika kufunga mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari na mitambo hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaonyesha kwamba hakuna hata kiwanda kimoja ambacho kinatengeneza vipuri vya kutoa mfumo wa mafuta kwenda katika mfumo wa gesi hapa nchini. Pia, ameeleza kwamba wanashirikisha sekta binafsi ili iweze kuwekeza katika vipuri hivyo. Je, mpaka sasa hivi wameshawashirikisha na wamepata wawekezaji wangapi ambao wanakwenda kutengeneza vipuri hivi hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa, hatuna kiwanda cha kutengeneza vipuri; je, Serikali haioni haja ya kupunguza ama kuondoa kabisa kodi katika vipuri vinavyoingizwa hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesimama, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imechukua hatua hiyo ambayo ameisema katika Bunge letu la Mwaka wa Fedha huu 2024/2025 tunaoendelea nao. Tulitoa hizo *incentives* kwa magari pamoja na vipuri vinavyotumia gesi, kwa sasa tunavyoendelea, kuna baadhi ya maeneo ambayo hatua nyingine zinaendelea zikiwepo hizo za kuhusisha Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi hata katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025 ambao tumeshaanza maandalizi ya kuandaa hatua za kikodi mpya. Jambo hili ni jambo ambalo lina msukumo wa Serikali ukizingatia Mheshimiwa Rais ni *champion* wa kidunia wa hii *transition* ya masuala haya ya kwenda kwenye mabadiliko ya nishati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari na kwa kuzingatia kwamba uchumi upo kwenye magari makubwa ambayo ni ya usafirishaji kwa maana ya malori na mabasi. Kwa Tanzania sasa hivi tuna vituo 14 tu ambavyo vinabadili magari ya *petrol* na kuweka mfumo wa gesi, kwa magari ya *diesel* mpaka sasa hivi hata kituo kimoja hakuna ukiacha cha Dangote ambacho ametengenezea magari yake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inapunguza gharama za usafirishaji na usafiri kwa Watanzania kwa kuweka kituo cha kubadili magari ya *diesel*? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa ni kweli anavyosema, vituo vingi ni vya kubadilisha mifumo

kwa magari ya petroli, lakini tunaendelea kuwekeza kwenye vituo zaidi ili kuhakikisha pia na magari ya *diesel* na yenyewe yanaweza kubadilishwa kwa mfumo wake. Ni kwamba tu kwa namna mifumo hii ilivyo, inatofautiana kwa kiasi kikubwa ndiyo maana ilikuwa ni rahisi zaidi kuanza na magari ya petroli kuliko yanayotumia *diesel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kadri tunavyoendelea na kwa uwekezaji ambao tunashirikiana na Sekta Binafsi, tunahakikisha tunaweka vituo pia vya kubadilisha magari ya *diesel* ili kuendelea kuunga mkono azma ya Mheshimiwa Rais ya matumizi ya nishati safi kwenye kupikia pomoja na matumizi mengine ya kiuchumi na kijamii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kutoka Wizara ya Nishati.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, swali la Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa na Mheshimiwa Ghati Chomete.

Na. 115

**Waathirika wa Matendo ya Unyanyasaji wa Kijinsia**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza:-

Je, Serikali inawasaidiaje waathirika wa matendo ya unyanyasaji wa kijinsia baada ya hatua za kisheria kuchukuliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia wataalam mbalimbali wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii wanatoa huduma

jumuishi kwa waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia. Aidha, huduma zinazotolewa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii ili kuwarejesha katika afya njema ya akili na kujengewa ustahimilivu ili waweze kuendelea na maisha ya kila siku; huduma ya makazi ya muda katika Nyumba Salama na Makao ya Watoto na kuunganishwa na huduma ya matibabu; na msaada wa kisheria na huduma za uwezeshaji kiuchumi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghati Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa wahanga hawa wa matendo ya ukatili wa kijinsia huwa na makazi ya muda, je, Serikali haioni sasa ni muda wa kuwapa makazi ya kudumu ili kutonyanyasika pindi wanaporudi katika familia zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni haja sasa ya kutenga fungu ili kuwawezesha wahanga hawa pale wanapokuwa wakisoma au wakijiendesha kiuchumi katika familia zao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Ghati kwa kuendeleza waathirika wa ukatili na kuona kwamba wanapata manusura. Swali lake la kwanza, Serikali inasimamia na huduma za utoaji makazi ya kudumu kwa wale waathirika wa ukatili, lakini hapo hapo inaendelea kuwapatia makazi ya kudumu kwa wale ambao hawana makazi na wanawekwa katika nyumba zetu salama, katika taasisi zetu za makazi ya wazee au na kwa wale watoto ambao ni wadogo wanawekwa katika makao ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali inaendelea na kujumuisha waathirika wa ukatili kwa wale waliokuwa wamekatishwa masomo. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia

Suluhu Hassan ameelekeza kwamba, wale wote ambao wamepata changamoto ya ukatili na wakakatisha masomo yao, basi wapelekwe ili waendelee kupata elimu kwa kujiendeleza. Wale waliopitwa na wakati wa masomo ya kimsingi, basi wanapewa mafunzo ya ujasiriamali ili wajiwezeshe kiuchumi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, nimekuona.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwabaini wale wahanga wa ukatili ambao walipoteza viungo vyao ikiwemo macho, masikio, mikono, miguu na kadhalika ili kuweza kuwapatia mikopo na fursa mbalimbali waweze kujikwamua kiuchumi na kuendelea na maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa elimu kupitia Maafisa wetu wa Ustawi wa Jamii. Kwa wale wahanga wote ambao wamepata changamoto ya kuondokewa na viungo katika miili yao, Serikali inachukua juhudi ya kuwapatia viungo hivyo lakini pia kuwapatia mikopo ambayo itaweza kuwasaidia katika maisha yao ili waweze kujiendeleza kiuchumi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nyumba Salama ziko chache sana zilizojengwa na Serikali, lakini watu binafsi ndiyo wamejenga Nyumba Salama. Je, Waziri haoni huu ni wakati sasa wa Serikali kujenga Nyumba Salama kwa ajili ya kuwahifadhi watu hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika Serikali tuna Nyumba Salama kidogo na inaendelea kufanya jitihada kadri itakavyopata fedha, itaongeza nyumba hizi ili kuhakikisha wale wote wanaoathirika na vitendo vya ukatili, basi wanapata mahali salama na kupata huduma ambazo zinastahiki katika maisha yao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, aulize swali lake.

Na. 116

**Ujenzi wa Barabara ya Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, lini Ujenzi wa Barabara ya lami kutoka Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Puge – Ziba – Choma yenye urefu wa kilometa 109 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa kilometa 11 kwa sehemu ya Puge – Ndala yenye urefu wa kilometa tano, Ziba – Choma kilometa mbili na Ziba – Nkinga, kilometa nne. Serikali

inategemea kutangaza zabuni ya kumpata Mkandarasi wa kuanza ujenzi wa sehemu hiyo Novemba, 2024. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itawashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika utiaji saini wa mkataba huo mwezi huu Novemba kama walivyoahidi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwezi Novemba ni mwezi wa kutangaza zabuni, kwa hiyo, tuna hakika haitakuwa rahisi kusaini mkataba mwezi huu wa Novemba, 2024. Baada ya kumpata Mkandarasi, wakati wa utiaji saini, tutahakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaohusika na hayo majimbo wanakuwepo kushuhudia utiaji saini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, nimekuona.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ujenzi wa Barabara ya Masasi – Nachingwea umeshindikana na Daraja la Mto Lukuledi lilisababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya Mkoa wa Mtwara na Lindi. Je, ni lini Daraja la Mto Lukuledi litajengwa kwa hatua za dharura? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, si kwamba huu umeshindikana, uko utaratibu mwingine ambao unaandaliwa ili kuijenga hii Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Daraja la Mto Lukuledi, binafsi nimepita baada ya Bunge lililopita na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kati ya daraja ambalo liliathirika sana kipindi cha mafuriko na limeingizwa kwenye utaratibu wa

kujengwa katika hizi fedha ambazo tunategemea wenzetu wa *World Bank* na tayari taratibu zinaendelea za kuanza kulijenga hilo daraja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza, nimekuona na Mheshimiwa Kawawa ajiandae. Tuendelee.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Songwe wanataka kujua ni lini ujenzi wa Barabara kutoka Mbalizi – Mkwajuni utaanza? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kibali kilishatolewa na makabrasha ya zabuni yanaandaliwa kwa ajili ya kuitangaza hiyo barabara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawawa, nimekuona Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali iko katika maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026. Je, Wizara ya Ujenzi inaweza kuweka katika Mpango wa Bajeti wa mwaka huo 2025/2026 ujenzi wa Barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi ambayo inapita katika Kata za Nkongo, Nakawale, Ligela, Lusewa, Magazini mpaka Tunduru inaweza kuwekwa katika Mpango wa Bajeti wa mwaka 2025/2026 ili iweze kujengwa kwa lami kwa sababu iko katika Ilani ya 2025? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni kitu ambacho ndiyo tuko tunafanyia maandalizi. Ninamuahidi tu, sisi kama Wizara na Serikali tunatamani barabara zote zijengwe kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tutakachofanya kwa kipande hiki cha kilometa ziko 300. Tukubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama wizara, tutaweka kwenye mipango ili tuweze kuingiza kwenye ujenzi kwa mwaka huo wa fedha unaokuja 2025/2026. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnzava, atafuatia Mheshimiwa Hasunga, maswali kwa ufupi tafadhali.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi nyingi na kutenga fedha kwenye bajeti tunayoitekeleza sasa, bado Serikali haijaanza hatua yoyote ya mchakato wa ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka Korogwe – Bumbuli – Soni. Ninataka kujua, ni lini mchakato huu utaanza na mkataba kusainiwa ili tuweze kupata mkandarasi wa kujenga hiyo barabara? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli watu hawajaenda mawandani, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunavyoongea sasa hivi, hiyo barabara imeshapata kibali na tuko tunafanya maandalizi ili barabara hiyo iweze kutangazwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Deo Sanga nimekuona.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kilometa 20 za Barabara ya kutoka Njiapanda ya Iyula – Idiwili – Nyimbili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara za mfano ambazo tunategemea zijengwe na makandarasi wanawake. Tayari tuko tunafanya maandalizi ili waanze kwenda. Tulishatangaza, lakini kwa sababu ya *bidding* yao ilikuwa iko juu, tuko tunafanya nao majadiliano kwenda kwenye bei zinazotakiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Kibena – Lupembe – Madeke kuunganisha Taveta

Morogoro, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu iko kwenye Ilani? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli iko kwenye Ilani, lakini pia wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyotembelea Mkoa wa Njombe, alitoa maelekezo Wizara tujenge kwa kuanzia kilometa 40. Kwa hiyo, tuko kwenye mchakato na alishatoa kibali hiyo barabara ianze kujengwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua lini Serikali mtaanza ujenzi Barabara ya Mloka – Msamba kupitia Chitete ili wananchi waweze kunufaika na barabara hiyo? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zote za zabuni zimeshakamilika kwa ajili ya kuitangaza na namhakikishia tunaanza kilometa 10 upande wa Momba na upande wa Mbozi kilometa tano tano. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Abeid Ighondo, niliwaona.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali tayari imetuambia inafanya tathmini ya kipande cha Barabara ya kutoka Idete – Itonya – Muhanga inayokwenda kuunganisha Mngeta Morogoro. Je, ni lini sasa kazi hiyo itafanyika ili Mkoa wa Morogoro na Iringa iweze kuungana? Ili wafanyabiashara wa mbao waweze kufanya biashara zao vizuri? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayosema ni ambayo kimsingi kwa sasa ni barabara inayopita kwenye treni kubwa na wapo wataalam ambao wanaipitia upya ili kuona namna ya kuisanifu ili iweze sasa kuunganisha Mkoa wa Iringa kupitia Kilolo kwenda Mlimba. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abeid Ighondo na Mheshimiwa Iddi, nimewaona.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba kujua ni lini sasa Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini ujenzi wa Barabara ya kutoka Igauri – Ilongero kilometa 111/2 utaanza? Majibu sahihi yasiyo…

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tayari imeshapata Mkandarasi na tunachosubiri ni kufanya *signing* ili Mkandarasi aanze kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi nilikuona.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda sasa toka mwaka 2023 imetengwa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwenye Barabara inayotoka Busisi – Nyang'hwale – Chela – Busangi – Kahama. Swali sasa, ni lini upembuzi yakinifu huo utaanza? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, barabara inaunganisha Mkoa wa Mwanza, Geita na Shinyanga na swali hili Mheshimiwa Mbunge liliulizwa na Mheshimiwa Nassor, Mbunge wa Nyang'hwale. Tunavyoongea sasa hivi, tumepata Mkandarasi nadhani muda wowote ataingia uwandani. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi nimekuona na nyuma yake pale.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kwa kuwa Mkandarasi wa Barabara ya Kisolya – Lugezi amesimama, kazi haiendelei na kuna sintofahamu. Je, Serikali inaweza kutoa kauli kwa wananchi wa Ukerewe kuhusu hatma ya barabara hii ya Lugezi – Kisolya? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kumekuwa na kusuasua kwa huyu Mkandarasi na sisi kama wizara tumeshapokea hati ya malipo, tumeiwasilisha kwa wenzetu Wizara ya Fedha, ili kulipwa kuendelea na hiyo kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amewahi kutembelea kwenye eneo la Daraja la Mto Kilambo kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mtwara na Mozambique. Anawaeleza nini Watanzania wa Mtwara kwamba ujenzi utaanza lini wa barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimetembelea eneo la daraja ambalo linategemewa kujengwa la Kilambo. Daraja hili bado halijasanifiwa na nimewahi kujibu hapa, ni daraja ambalo kimsingi linahusisha nchi mbili ya Mozambique na Tanzania. Kwa kweli ni daraja ambalo litakapojengwa litakuwa na tija sana kwa upande wetu Tanzania na upande wa wenzetu wa Mozambique.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mtwara kwamba, kulijenga hili daraja kwa kweli kunahitaji siyo sekta tu ya ujenzi, ziko Wizara mbalimbali ambazo zinahusika, ikiwa ni pamoja na wenzetu wa upande wa Msumbiji, tutakapokamilisha makubaliano ndiyo tutalianza. Sisi kama Serikali tumeshatenga fedha kiasi cha kuanzia kama tutakuwa tayari basi hiyo kazi itaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, tutamalizia na wewe.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza tu; je, ni lini upembuzi yakinifu utakamilika kwenye Barabara ya kutoka Newala - Kitangali - Mtamba kilometa 74? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni ngumu kusema ni lini kwa sababu inategemea na kitu ambacho wanapofanya usanifu wanakikuta. Inawezekana tulitegemea wapate kwa siku 10, lakini kuna maeneo wanaweza wakachukua muda tu. Cha msingi tu labda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa wapo wanaendelea, baada ya hapa tunaweza tukakutana ili tuweze kujua lini hasa huyu msanifu wa ndani ambaye yupo atakamilisha usanifu huo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo.

Na. 117

**Kuweka Matuta na Vivuko Barabara ya Lupaso hadi Tukuyu**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini matuta na vivuko kwa waenda kwa miguu vitawekwa katika Barabara ya Lupaso - Lwangwa - Mbambo hadi Tukuyu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kuweka alama za barabarani kwa ajili ya waenda kwa miguu kuvuka barabara ambapo itawekwa michoro ya *zebra crossing* na vibao vya

alama za kuonesha watu kuvuka barabara. Maeneo yatakayowekwa alama hizo ni Mbambo, Buikuba, Malema, Kitusyo, Kasyeto, Mabonde na Bulyaga. Kazi ya kuweka alama hizo inatarajiwa kuanza ifikapo mwisho wa mwezi huu wa Novemba 2024. Aidha, tathmini ya kina itafanyika ili kubaini maeneo yote ambayo kuna ajali nyingi ili matuta ya kupunguza mwendo yaweze kujengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atupele Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana Mheshimiwa Naibu ametembelea barabara hii umejionea pamoja na Waziri mwenyewe, hata Waziri wa Fedha amepita kwenye barabara hii na mliona namna ambavyo kuna miteremko mikali sana katika ile barabara. Eneo la Lwangwa Mjini kuna shule mbili: Shule ya Msingi Lwangwa na Shule ya Msingi Muungano, ambapo watoto wanavuka barabara hii. Je, ni lini hasa Serikali itachukua hatua za dharura ili kuokoa maisha ya watoto hawa kwa kujenga matuta ili kuzuia ajali ambazo hadi sasa zimetokea ajali zaidi ya sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pole kwa watoto ambao wamekuwa wanapata adha hii kwa sababu ya ujenzi wa hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba natoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Mbeya aweze kufika haya maeneo ya shule mbili ambapo kuna watoto wanavuka hii barabara ili aweze kufanya tathmini ili aweze kupata kibali cha kujenga matuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitumie nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba kumekuwa na changamoto kubwa sana ya baadhi ya maeneo kuondoa alama za usalama barabarani. Hili kwa kweli iko mikoa

ambayo imekithiri na ni hatari sana kwa watumiaji wa barabara. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane ili kulinda watumiaji wa barabara, vyombo vinavyopita kwenye barabara na sisi wenyewe, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi kwa majibu hayo mengi sana ambayo umeyatoa kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, aulize swali lake.

Na. 118

**Uzalishaji wa Bidhaa zenye Viwango Hafifu Nchini**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu uzalishaji wa bidhaa zenye viwango hafifu na ukubwa tofauti zikiwa na bei sawa sokoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* Wakala wa Vipimo *(WMA)* na Tume ya Ushindani *(FCC),* inatekeleza jukumu la kudhibiti ubora (viwango), usalama, vipimo sahihi na kukuza ushindani wa kibiashara kwa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Sura ya 130, Sheria ya Vipimo Sura ya 340 na Sheria ya Ushindani Sura ya 285. Kwa kufanya hivyo, Serikali inahakikisha kuwa bidhaa zinazoingia sokoni zinakidhi matakwa ya sheria zilizowekwa na kukuza ushindani wa haki katika sekta ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe rai kwa wazalishaji wote nchini kuzalisha na kuuza bidhaa kwa kuzingatia sheria zilizopo nchini. Aidha, Serikali kupitia *TBS, WMA* na *FCC* itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha bidhaa zote

zinazalishwa kwa viwango, zinafungashwa kwa vipimo sahihi na kunakuwa na ushindani wa haki. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na uwepo wa taasisi hizi zote, *TBS, WMA* na *FCC* ni ukweli usiopingika kwamba, bidhaa hizi ambazo zimekosa ubora zimetapakaa kwenye mitaa yetu na masoko. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kukabiliana na changamoto hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa uwepo wa bidhaa hizi zisizo na viwango (ubora) ni wazi na inadhihirisha wazi kwamba, taasisi yetu ya *FCC* imezidiwa na majukumu yake mawili ambayo moja ni kulinda ushindani na la pili ni kulinda maslahi ya watumiaji. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuunda wakala moja tu ambao itasimamia maslahi ya watumiaji? Ninakushukuru, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, Mbunge wangu wa Kibamba kwa ufatiliaji kuhusiana na sekta ya biashara kwa sababu jimbo lake lina wafanyabiashara zaidi pia kwa kazi kubwa anazofanya kuwakilisha wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kuhusiana na bidhaa ambazo hazina ubora pia, ambazo hazikidhi matakwa na sheria. Tumeendelea kufanya marekebisho lakini zaidi kutoa elimu kwa wadau wote. Moja, taasisi hizi ambazo nimezitaja kwa kushirikiana na taasisi nyingine tunatoa elimu kwa waagizaji wa bidhaa kutoka nje, wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa hizo. Pia, hata wauzaji wa kawaida na sisi wenyewe walaji kwa ujumla wetu ili tuweze kutambua bidhaa ambazo zinakuwa hazina ubora, ambazo zina madhara au hazikidhi viwango ambazo ziko sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalifanya na kuwaomba Watanzania kila tunaponunua bidhaa tuombe risiti na hasa risiti ya *EFD* ambazo unapotaka kulalamika kwa maana ya bidhaa haina ubora au ina shida, utumie hiyo risiti kusema nimechukua kwenye duka fulani na sisi tunafanya ufuatiliaji. Zaidi, taasisi hizi huwa zinafanya ukaguzi kwenye viwanda, kwa wazalishaji pia hata mitaani ili kubaini pale kunapotokea na changamoto ya bidhaa ambazo hazikidhi viwango au hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuendelee kushirikiana sisi kama Wabunge kutoa elimu, pia na Watanzania wote kuhakikisha tunafuata taratibu ambazo zitatusaidia kubaini bidhaa zinazoingizwa au zinazozalishwa katika viwango duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nimhakikishie kwamba, *FCC* haijazidiwa, lakini kama ambavyo siku zote changamoto hizi unapotatua moja inaibuka nyingine. Nichukue ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuone namna gani Serikali inaweza kufanyia kazi na baadaye tuone kama tunaweza kuwa na sheria mahususi ya kumlinda mlaji kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Mahawanga na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo nimewaona.

Mheshimiwa Esther.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ninataka kufahamu, je, uwazi wa bei na ubora wa bidhaa unaimarishwa vipi sokoni ili kuwalinda wateja na walaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna wakati tunakuwa na bidhaa ambazo hazina ubora, lakini zinaingizwa sokoni na kuuzwa bei sawa na zile bidhaa ambazo zina ubora au ni sahihi na hii inatokana na

bidhaa nyingine kuwa bandia. Sasa, sheria yetu kupitia *FCC* kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunakagua ili kuona: moja, bidhaa inayouzwa ni ile ambayo hakika tunaijua na kwa maana ya ubora ule. Pili, bei zinaenda sawasawa na zile ambazo tumeziweka. Ndiyo maana tunaendelea kufanya utaratibu wa kuhakikisha katika maduka yote, katika maeneo yote ya kuuza bidhaa, bidhaa zote zibandikwe bei ili mteja anapoingia aone bei ya bidhaa na anakuwa anajua na bei hiyo maeneo mengine, ili kuhakikisha huu mkanganyiko wa bei za bidhaa zinazofanana na nyingine ambazo siyo sahihi ambazo hazina ubora tunapunguza au tunatatua kabisa changamoto hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar nilikutaja.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kwa kuwa hili jambo la bidhaa zenye ubora hafifu ni janga la Kitaifa. Serikali haioni ni muda wa kuharakisha Sheria ya Kuwalinda Watumiaji ili kuokoa fedha ya Watanzania ambapo mara nyingi ni *FCC* imekuwa ikiteketeza bidhaa bandia na hafifu badala ya kuizuia isiingie kwenye nchi yetu ili kuokoa fedha za Watanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo kwa kuwa mfuatiliaji na amekuwa kinara kuhakikisha tunakuja na hii Sheria ya Kuwalinda Walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukitoa elimu na bado ninaendelea kusema kwa sababu nia ya Serikali siyo kuharibu au kuwaumiza wafanyabiashara kwa sababu ni hasara kubwa. Kwa mfano, wengi wanaoagiza bidhaa hizi kutoka nje wanakuwa wametumia fedha za kigeni ambazo Serikali au nchi tumezitafuta kwa ajili ya kuingiza bidhaa ambazo nadhani ni muhimu. Sasa inapokuja kutokea na kuharibu haina tija kwa uchumi wetu. Sasa, tumeendelea kutoa elimu kwamba, wafuate sheria ya kuingiza bidhaa zenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta hata leo hii, sasa hivi kuna bidhaa ambazo zinakamatwa huko mipakani kupitia taasisi zetu pia na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ili kuzuia uingizaji wa bidhaa ambazo hazina ubora, lakini kufuata sheria na tunahamasisha wapitie kwenye taratibu za kuingiza bidhaa badala ya kuingia kwa magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunalichukua wazo hili la kuona ni namna gani tutafanya mchakato wa haraka wa kuanzisha Sheria ya Kuwalinda Walaji ili kupunguza adha na athari ambazo, *either* zinaambatana na madhara kwa walaji pia kuathiri uchumi wa nchi yetu. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 119

**Mradi wa Maji Kijiji cha Mang'ola Juu – Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji uliokwama kwa muda mrefu katika Kijiji cha Mang'ola Juu Wilayani Karatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Kijiji cha Mang'ola Juu Wilayani Karatu. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 270,000, ulazaji wa mtandao mabomba umbali wa kilometa 30, ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji, ujenzi wa Ofisi ya *CBWSO*, ujenzi wa nyumba ya

kuendeshea mitambo *(pump house)* na ujenzi wa Mbauti tatu za kunyweshea mifugo *(cattle trough)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 30% ambapo umeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya maeneo kupitia vituo saba vilivyokamilika wakati utekelezaji ukiendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025 na kunufaisha wananchi 5,616 waishio kwenye Kijiji cha Mang'ola Juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kazi ambazo zimeelezwa kutekelezwa na Serikali baadhi yake bado hazijafanyika. Kwa mfano, ujenzi wa matanki kazi haijaanza, ulazaji wa mabomba kazi haijaanza, lakini mnatuahidi mpaka mwezi Machi, kwamba kazi hii itakamilika, lakini uhalisia kule uwandani hakuna kazi inayoendelea. Nini kauli ya Serikali kwa wananchi hawa kuhusu uhakika wa kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kulikuwa kuna ahadi ya Serikali kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Karatu. Kwa hiyo, kulikuwa kuna andiko la shilingi milioni 864 kwa ajili ya kuhakikisha wananchi katika Mji Mdogo wa Karatu wanapata maji. Kama haitoshi wakati wanaunganisha zile mamlaka mbili za maji, Serikali iliahidi kutuletea bilioni nne kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wa Mji Mdogo wa Karatu wanapata maji lakini mpaka tunavyoongea leo hakuna hata senti tano iliyoenda. Je, nini kauli ya Serikali hasa tukizingatia kuna hali ngumu sana ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa

kazi nzuri anayoifanya na kwa kweli tumeendelea kushirikiana naye na nilifanya ziara katika Mji wa Karatu na haya yote ambayo ameongea kweli mimi nayafahamu. Pia, mradi huu ambao kama tunavyosema umefikia 30%, maana yake ni kwamba kuna kazi ambazo zimefanyika kwa kiwango cha *progress* kufikia *status* ya 30% maana yake ni kwamba kuna maeneo mengine ikiwepo pamoja na matanki yatakuwa bado hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wetu wameenda mbele zaidi, wameenda na kujiridhisha kwamba, mkandarasi aliyekuwa amepewa kazi hii uwezo wake kiufundi na uwezo wake kifedha anaonekana kusuasua. Serikali tayari tumeshampiga *liquidated damage* kulingana na kuchelewesha kazi na tayari mwanasheria wetu wa *AUWASA* tumeshamwelekeza aendelee kufanya mchakato wa kusitisha mara moja mkataba na mkandarasi wa aina hiyo. Tutaendelea kuchukua hatua kwa wakandarasi wote nchi nzima ambao wanaonekana kusuasua katika utekelezaji wa miradi yetu, kwa sababu sisi kazi yetu ni kusimamia utekelezaji na miradi iishe kwa wakati na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, ni kweli kabisa Serikali tuliahidi na niwahakikishie kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Sauluhu Hassan tutahakikisha hiyo ahadi ambayo tumeitoa katika Mji wa Karatu, tunaitekeleza pale ambapo pesa itakapopatikana. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi tafadhali. Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester na Mheshimiwa Esther.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, Mradi wa Maji Mogitu - Gehandu umechukua muda mrefu lini utakamilika ili wananchi wa Milongori, Gidabwanja, Marega na Mwanina wapate maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa Hanang ni mradi ambao una gharama ya bilioni 1.67 ambao una vituo takribani 40 na tufahamu kabisa kwamba, kuna kutandaza boma umbali wa kilometa 83. Mradi huu unatarajia kuisha tarehe 15 Machi, 2025. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Mkandarasi *JAMTA Construction Investment* ambaye anatekeleza Mradi wa Msangano - Chitete ameamua kutelekeza mradi huu pamoja na kuitwa Ofisi kwa *RAS* Mkoa wa Songwe. Licha ya kulipwa *advance payment* milioni 820 kati ya milioni 920, bado ameendelea kutelekeza mradi huu. Je, Wizara ya Maji wamekusudia kuchukua hatua gani kwa mkandarasi huyu gaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Condester. Hizi ndizo taarifa ambazo tunafurahi kuzipata kutoka kwa wawakilishi wa wananchi na sisi kama Serikali tutaenda kufuatilia kwa kina na kujiridhisha na changamoto hii na Serikali tutachukua hatua. Hatutakuwa na uvumilivu wa aina yoyote ile kwa mkandarasi yeyote yule ambaye atataka kutukwamisha kutekeleza miradi ya Serikali ambayo wananchi wanatarajia ikamilike kwa haraka na kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema uungwana ni vitendo. Niishukuru Wizara ya Maji kwa Mradi wa Manyamanyama Naibu Waziri alienda kuzindua mwenyewe. Nishukuru kwa Mradi wa Kisangwa milioni 400, nishukuru kwa Mradi wa Wariku bilioni 1.6 na nishukuru kwa Mradi wa Bunda Vijijini Nyamswa wa bilioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kumuuliza swali la nyongeza. Bunda ni miongoni mwa halmashauri ambazo

zinaongoza kwa upotevu wa maji, mia tatu na sisi hatuhitaji hiyo, tunataka tunufaike na Mradi wa Nyabehu. Tunatumia 45% tu ya maji, maji mengi yanapotea. Sasa kuna mradi umeanza wa shilingi 1.7 *billion* kutoka Bugutu – *Bunda Store* kwenda Mlima Kisakwa, ili kuweka bomba kubwa na kuzuia upotevu wa maji. Ni lini Serikali watatupatia hiyo pesa tuweze kumaliza, ili tuepukane na tatizo la maji, tutumie walau 60%, wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wapate maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kazi nzuri na kwa ushauri. Swali lake lina ushauri ndani yake na kweli kabisa, kama Serikali tumekuwa tukifuatilia sehemu ambayo tumekuwa na changamoto na kwa upande wa upotevu wa maji ni tatizo ambalo Serikali tumeanza kulichukulia hatua kali kwa sababu, lina tusababishia hasara kubwa. Badala ya maji kuwafikia watumiaji, mengi tunayapoteza wakati yametumia gharama kubwa katika kuzalisha. Kwa hiyo, tumeshaelekeza mamlaka mbalimbali nchini kote kuhakikisha kwamba wanaendelea kuboresha miundombinu yao ili kuzuia upotevu wa maji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** … ili yaweze kuwafikia wananchi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili maji yaweze kuwafikia walengwa kwa kadri ambayo yatakuwa yamezalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha ambazo ameomba Mheshimiwa Mbunge; ninaomba nilipokee tukalichakate kama Wizara. Baada ya hapo tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge kwa hatua ambazo tutakuwa tumezichukua, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimemwona Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi unaounganisha vijiji 37 wa kutoka Kata ya Kisorya hadi Kibara umekamilika. Je, ujenzi wa mradi huu utaanza lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu ukishakamilika Serikali inatafuta fedha, kwa ajili ya kuweka katika mpango wa bajeti unaokuja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi kwa kadiri ambavyo anatamani, wananchi wake wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka nilimtaja, Mheshimiwa Genzabuke, Mheshimiwa Festo, halafu tutaendelea na upande huu.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Mkoa wa Lindi na Wilaya zake zote kuna shida sana ya maji na hii inasababishwa na kutokuwa na chanzo kikubwa cha maji kwenye Mkoa huu. Je, Serikali haioni umefika wakati sasa kuja na mpango wa kutuletea maji ya Mto Rufiji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali hili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mkoa wa Lindi umekuwa na changamoto hiyo, lakini pia, tunafanya *study* ya kujiridhisha aina ya vyanzo ambavyo tunaenda kuvitumia, iwapo vitakuwa vinatuletea matokeo yenye gharama nafuu, basi

tutatumia Mto Rufiji, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri, lakini kama itakuwa vinginevyo basi tutatumia maji kutoka vyanzo vingine. Lengo ni kwamba, wananchi wapate maji safi na salama, lakini yenye gharama nafuu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke, Mheshimiwa Festo, halafu Mheshimiwa Minza ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Halmashauri ya Kasulu, Kata ya Rusesa, ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa ili wananchi waweze kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze dada yangu kwa kazi nzuri ya kuwasemea Wanakigoma kwa ujumla wake, hususan Kasulu. Kwa Kasulu tuna mradi wetu wa Miji 28 ambao unaendelea na mradi ule tunaamini kwamba, unaenda kuhudumia zaidi ya vijiji 11 utakapokamilika kwa sababu, una-*cut across* kwenye Kata nyingi. Baada ya hapo tutafanya *study* ya kuona ni sehemu gani ina upungufu na kama bado kuna changamoto tutachukua hatua stahiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niipongeze Wizara ya Maji kwa kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya maji. Kwa sisi Jimbo la Makete tunafanya vizuri kwa zaidi ya 95%, lakini tuna changamoto ya Mradi wa Ipelele, Mradi wa Kitulo na Mradi wa Mfumbi; wamewapatia fedha wakandarasi wamejenga *intake,* wamechimba mitaro, changamoto iliyopo ni kwenye mabomba wakisema wanafanya manunuzi ya *bulk system.* Je, ipi kauli ya Serikali ya kuachana na ununuzi wa mabomba kwa mkupuo mkoa mzima tukaanza kusubiria ununuzi wa mabomba kutoka eneo moja, badala ya kutumia ule mfumo wa nyuma ambao

ulikuwa unasaidia kupatikana mabomba kwa wakati na miradi inakamilika kwa wakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kulileta hili jambo. Tumeshalipokea kutoka kwa Wabunge wengi na kwa ruhusa yako naomba kidogo nitoe ufafanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tuliipata ni kwamba, mabomba yana-*exemption*. Haya mabomba yanapokuwa na *exemption* kila mkandarasi akisema kwamba, apeleke *exemption* peke yake ule utaratibu wa kuhudumiwa kwa haraka unakuwa na changamoto yake. Sasa, kama Serikali, tukaona kwamba, *bulk procurement* itaturahisishia zaidi kwenda ku-*submit,* kwa ajili ya *exemption* ili mabomba yaweze kupatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho lazima tuambizane ukweli ni kwamba, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna alivyotoa fedha nyingi kwenye Sekta ya Maji ndiyo maana tumetekeleza miradi mingi, *demand* imekuwa kubwa kuliko *supply,* maana yake ni wazalishaji wamekuwa ni wachache kulingana na *quality* ambayo tunaihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta kwamba, mabomba yanachelewa kwa sababu, miradi mingi bado iko kwenye *que* inasubiri mabomba yazalishwe, ili tuweze kuyafikisha kwa watumiaji. Kwa hiyo, tunaelewa kwamba, changamoto hii imekuwa ikitokea, lakini tunaendelea kuifanyia kazi kuhakikisha uzalishaji unaendana na kasi ya mahitaji ya sisi, Wizara na Sekta ya maji, tunavyohitaji. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kushirikiana, kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza na tutamalizia na Mheshimiwa Chege.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Meatu ni miongoni mwa Wilaya ambazo ni kame sana katika Mkoa wa Simiyu, haina maji, kwa kweli, maji ni tatizo kubwa. Je, ni lini sasa Mradi Mkubwa wa Ziwa Victoria utakamilika katika Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Minza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Minza ameweka kipaumbele katika ufuatiliaji wake, na hasa katika Wilaya ya Meatu, amekuwa akiwasemea sana akinamama. Nampongeza sana mama yangu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Wanameatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Dkt. Samia Suluhu Hassan amewapatia Wanasimiyu shilingi bilioni 440, kwa ajili ya Mradi Mkubwa wa Kimkakati wa Kutoka Ziwa Victoria ukianzia Nyashimo, kuja Bariadi, kwenda Itilima kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili itakuja kutoka Maswa kwenda Meatu kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba, itakapofika mwakani mradi huu utakamilika na wananchi watapata huduma ya maji safi na salama katika Wilaya ya Meatu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kazi kubwa, nzuri, inayofanywa na Wizara ya maji, lakini Mradi wa Maji wa Miji 28, Rorya Tarime, umesimama zaidi ya miezi minane, Mheshimiwa Waziri. Nataka nipate kauli ya Serikali, nini tatizo, hasa ukizingatia mradi huu ndiyo ulikuwa suluhisho la changamoto ya maji katika Wilaya ya Rorya na Wilaya ya Tarime?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia mradi

huu na kuendelea kuwasemea wananchi wa Rorya. Nimhakikishie kwamba, miradi yote ya miji 28 Serikali imeweka jicho lake na tunafuatilia kwa ukaribu sana. Miradi hii ilikuwa ni *design* and *build* kwa hiyo, kuna kipindi ambacho kulikuwa na taratibu fulani za uchoraji wa michoro ambazo ndiyo zilichelewesha, hatua inayofuatia ni ujenzi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba, kuanzia sasa wakandarasi watakimbia na wataweza kuutekeleza mradi huo. Mkandarasi wetu anayetekeleza mradi huu ni *CCC,* Kampuni kutoka China, ambapo Mkandarasi Mshauri ni *WAPCOS* kutoka India; wako vizuri na wanafanya kazi nzuri sana. Tunaamini kwamba, tutakapokuwa tume-*clear* baadhi ya vitu ambavyo ni vya kiufundi, mradi utaenda kasi sana na utakamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Majibu mengi kabisa kutoka Wizara ya Maji.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, aulize swali lake.

Na.120

**Hitaji la Minara ya Simu Eneo la Nyamohonda na Itiryo, Tarime Vijijini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka minara ya simu eneo la Nyamohonda na Itiryo, Tarime Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* inatekeleza na kukamilisha ujenzi wa minara 7 ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata sita zilizopo Tarime Vijijini za Gorong'a, Muriba, Nyamwaga, Kiore, Nyansincha na Nyanungu. Kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa minara mitatu kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(DTP)* katika Kata tatu za Nyarokoba, Kibasuka na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi inayoendelea katika Jimbo la Tarime Vijijini kutaboresha huduma za mawasiliano, hivyo endapo changamoto za mawasiliano zitaendelea kuwepo *UCSAF* itafanya tathimini katika Kijiji cha Nyamohonda kilichopo Kata ya Mwema na Kata ya Itiryo yenye Vijiji vya Itiryo, Nyankoni na Kangarioni, ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano ya simu na kuviweka vijiji hivyo katika mpango wa miradi inayofuata ya huduma za mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; hilo eneo la Nyamohonda ni Kata ya Mwema, ni mpakani kati ya Tanzania na Kenya. Sasa hayo maelezo kwamba, ikiwa kama kuna shida kule hakuna mawasiliano, wananchi wa kule wanapata taarifa kutoka Kenya na Kenya mnajua kinachoendelea kule. Kwa hiyo, tunaomba eneo hilo lifanyiwe kazi, utafiti ufanyike na huduma ya mawasiliano iwekwe katika eneo la Nyamohonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; hiyo siyo Itinyo inaitwa Itiryo, Kijiji cha Kangarioni, ndiyo Kata yangu mimi ninapotoka hapo. Eneo hilo pia, ni mpakani kule juu karibu na Masai Mara na kwenyewe pia, hakuna mawasiliano. Sasa ningependa nijue kauli ya Serikali kwamba, ni lini maeneo hayo yatapelekewa minara mahususi ili wananchi wetu wapate taarifa ya Tanzania na siyo taarifa ya Kenya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza, kaka yangu, Mheshimiwa Waitara kwa namna ambavyo ameendelea kufuatilia; naomba nimtoe hofu Mbunge kwamba, maeneo yote ya mipakani tumeweka mpango madhubuti kuhakikisha mawasiliano yanaweza kupatikana kutokana na minara yetu. Katika eneo hili naomba nimhakikishie Mbunge tutakwenda kulifanyia kazi, kama unavyoshauri, lakini kwa ufasaha kabisa kuhakikisha wananchi wa Tanzania wananufaika na kazi njema ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Benaya Kapinga nimewaona.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika maeneo ya Mkoa wa Simiyu ambayo haina minara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze, dada yangu, Mheshimiwa Esther Midimu kwa kufuatilia maeneo haya ya Mkoa wa Simiyu kupata minara. Jana Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote wameweza kugawa vitabu kuonesha utekelezaji wa Miradi ya Minara 758 kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali. Naomba Waheshimiwa Wabunge tukipitie kitabu hicho, kila mtu kwenye eneo lake, ili pale ambapo eneo unalolihitaji wewe mradi ujengwe na kwenye kitabu haionekani uweze kuwasiliana na namba za simu za watendaji wetu ambazo zimewekwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha vilevile maeneo yote ya Mkoa wa Simiyu yanapata usikivu wa uhakika. Naomba pia niseme, kupitia kitabu tulichokigawa humu ndani kwa Wabunge wote, tuna mradi mwingine wa *Rural Connectivity, Phase One* Minara 636 pia, ipo kwenye mchakato wa kazi kuendelea na hii itaendelea kusogea maeneo yote ambayo haikupata minara 758.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii minara 636 nayo inakwenda kujengwa, vilevile naomba kama itafaa tuone kwamba, mawasiliano yanafanyika kupitia namba zilizoandikwa humo. Tayari mimi binafsi nimeshaanza kupokea maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali humu ndani na pia, naendelea kupokea. Kama kuna lolote tafadhali nikirudi pale kwenye kiti karibu, ili tuweze kuona tunaweza kuyaweka haya mambo vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Khalifa, maswali kwa ufupi.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Halmashauri ya Mbinga tulipata minara mitano kupitia huu Mradi wa Minara 758 na miongoni mwa kata hizo ni Kata ya Amani, Makolo. Kwenye hiki kitabu nimesoma, wanasema mradi umekamilika, lakini kumbe mradi huu haujajengwa Amani Makolo, umejengwa Kata ya Liganga, Kijiji cha Mbomogo, Bombambili, lakini tunashukuru sana kwa sababu, pamoja na kuwa umejengwa huko Peramiho unatoa mawasiliano kidogo hapa Kiwombi. Sasa je, lini mradi huu wa Kiwombi utajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naye nimpongeze kwa kazi nzuri unayoifanya katika Jimbo lako kaka yangu, lakini kiutaalam wakati fulani tunalazimika kujenga mnara kwenye pointi ambayo inaweza ikahudumia eneo zaidi ya lile ambalo umeliombea. Kwa hiyo, ule mradi wa Amani, Makolo, kama unavyosema, umejengwa pale Liganga lengo ni kuona kwamba, wa upande wa huku waweze kupata *signals* na upande wa huku wapate *signals.* Kwa hiyo, kama bado kuna eneo la kule upande wa Amani, Makolo, unakosa mawasiliano. Nimhakikishie tunakuja kuona kwamba, kwenye mnara uliopo karibu zaidi tuongezee

nguvu, ili eneo lote sasa liweze kupata mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa, halafu tutamalizia huku Mheshimiwa *Engineer* Stella, pamoja na Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Maeneo makubwa mengi ya Pemba kunakosekana mawasiliano ya simu ikiwemo Kijiji changu cha Kidundo katika Jimbo la Mtambwe na kuona ni kuamini. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atakuja Pemba tumtembeze katika maeneo ambayo mawasiliano ni magumu katika Kisiwa cha Pemba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali ni la kwanza, la pili ni ombi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa kuendelea kufuatilia mawasiliano ya uhakika kwa wananchi na ndiyo dhima ya Wizara yetu ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ikimpendeza Mwenyezi Mungu, tarehe 20 tutakuwa pamoja Pemba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer,* nilimtaja Stella Manyanya na tutamalizia na Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi karibu shule zote za msingi na sekondari pamoja na vituo vya afya na zahanati vinatumia mifumo ya TEHAMA katika mawasiliano muhimu. Sasa katika Kata ya Linga, Kijiji cha Lukale, Ndingama na Litumba, Kohamba, vyote havina mawasiliano ya kueleweka yaani mpaka uvizie ni lini kata hiyo itasaidiwa iweze kupata mawasiliano ya uhakika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupongeze sana Mheshimiwa Stella Manyanya kwa ufuatiliaji mzuri sana wa uhakika wa masuala ya TEHAMA. Sisi kama Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tunahakikisha maeneo haya ya huduma za kijamii yanafikiwa na mawasiliano ya *internet* na Mkongo wa Taifa kule Nyasa umeshafika. Naomba niwasiliane na meneja husika na maeneo ya Vijiji vya Lukale, Ndingama na Kijiji hiki cha tatu, vyote nikuhakikishie tutafikisha Mkongo wa Taifa ili mawasiliano ya TEHAMA shuleni yaweze kupatikana na pia, vituo vya afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kutupa miradi miwili kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote katika Kata ya Kitanda, lakini pia, Kata ya Mpepai, Kijiji cha Ruvuma Chini. Mradi wa Kata ya Kitanda umejengwa, lakini tunasubiri ujenzi wa Kata ya Ruvuma Chini. Sasa nataka nijue, katika Kata za Kikolo na Kagugu kuna changamoto kubwa ya mawasiliano, je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha, kwa ajili ya kujenga minara ya simu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunda amekuwa na mawasiliano ya karibu na Wizara yetu na mimi binafsi na wewe tunaongea sana. Nimwombe, kadri ambavyo tunaendelea kutekeleza hii minara 758 na 636 tutahakikisha kadri tunavyoendelea kupata fedha hizi, Kata alizozitaja nazo lazima tuzifikie na tayari nilifika Mkoa wa Ruvuma; niliacha maagizo, maeneo haya ya Mbinga yapo kidogo mpakani na yenyewe pia, tunayaangalia kwa jicho la karibu sana. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na haya maeneo aliyoyatamka tutakuja kuyafikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza la mwisho.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Nimesoma Kitabu cha Tanzania ya Kidijitali, sasa Kata ya Geterer sehemu ya Changanyikeni haina mnara, Yaeda Ampa pia hakuna mnara, Endamilay sehemu ya Masqaroda hakuna mnara, Mewadan sehemu ya Haydarer hakuna mnara, Endoji, Erboshan hamna mnara, kunakoitwa Qamtananat Beju hakuna mnara. Mheshimiwa Waziri unanisaidiaje maeneo haya ili Tanzania ikaunganishwe kwa mawasiliano ya minara kule kwetu Mbulu Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninaomba nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Flatei Massay, ni jana tu ameweza kufika pale kwenye kiti changu na tumeongea, nilimhakikishia maeneo haya yote aliyoyataja ni lazima tunayaweka kimkakati kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano ya uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, maswali mengi sana kutoka Wizara ya Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa aulize swali lake.

Na. 121

**Ununuzi wa Meli Kubwa ya Uvuvi Ziwa Nyasa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Meli moja ya Uvuvi Ziwa Nyasa ili samaki wakubwa wanaoishi kwenye kina kirefu wasiendelee kufa?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haijaweka mpango mahsusi ya ununuzi wa Meli ya Uvuvi katika Maziwa Makuu ikiwemo Ziwa Nyasa, lakini Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* inaendelea kutoa mikopo ya gharama nafuu ya boti za kisasa za uvuvi ambapo hutolewa kupitia vikundi vya wavuvi, vyama vya wavuvi, taasisi za sekta binafsi na wavuvi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, boti hizo zina urefu kuanzia mita tano hadi mita 14 kwa ajili ya kuvua samaki wanaopatikana katika maji marefu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu kutoka kwa Serikali. Pia, nishukuru kwa Mheshimiwa Rais kutoa milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Samaki pale Manda. Ninayo maswali mafupi madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; sasa tupo kwenye kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa, hii sehemu ya uchumi wa bluu ili uweze kutengeneza ajira na kuongeza pato. Je, Serikali haioni haja ya kuweka mpango wa kuwa na meli za uvuvi kwenye maziwa haya makuu, likiwemo Ziwa Nyasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Serikali imetoa fedha nyingi sana kujenga soko la samaki na ilikuwa na mpango wa kwenda kutafuta maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki Ziwa Nyasa. Je, ni lini Serikali itakwenda Wilayani Ludewa Ziwa Nyasa kuyaainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki ili tupate samaki wengi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, Serikali kwa sasa haina mpango huo wa kununua meli hiyo kwa ajili ya kumilikiwa na Serikali, lakini mpango tulionao kwa sasa ni kuwawezesha wavuvi wadogo na wakubwa ili wao wenyewe

ndiyo wachukue meli hizo waende kuvua kwenye maji marefu. Kwa hiyo, tumelichukua hilo la Mheshimiwa Kamonga tutaenda kulifanyia kazi. Kwa sasa ni kweli kwamba wavuvi wetu tunaendelea kuwakopesha boti za kisasa ambazo zitawasaidia kwenda kuvua samaki kwenye maji marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu maeneo ya ufugaji, ni kweli kwamba dunia sasa ipo kwenye ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba na tayari tumeshatuma wataalam wetu kwenda Ziwa Nyasa na maziwa mengine ambayo yanatuzunguka katika Taifa letu na wameshaanza kutoa taarifa juu ya wapi panapaswa kuwa na vizimba na wakishakamilisha taarifa yao basi tupo tayari kuleta vizimba katika Ziwa Nyasa ili wavuvi wa maeneo hayo waweze kunufaika na vizimba. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Thea Ntara nimekuona.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kuna tatizo kubwa sana kwa boti za kisasa kwenye uvuvi hasa *Lake Nyasa*. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Chuo cha Mbegani kule Bagamoyo ili waweze kutengeneza boti hizo za kisasa ziende kule Nyasa na maziwa mengine na vijana wapate uchumi katika mifuko yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutakwenda kuufanyia kazi. Kama kutakuwa na uwezekano huo, tupo tayari kushirikiana na Chuo cha Mbegani kutengeneza boti hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon nimekuona.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimuulize Mheshimiwa Waziri. Alikuja Kigoma yeye pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, walihamasisha wananchi kwa ajili ya kuchukua vizimba ili waweze kuondokana na ile adha ya kufungwa kwa ziwa halafu wanabaki

bila kupata vitoweo. Ni lini sasa vizimba vitakuja katika Mkoa wa Kigoma hasa kwenye Ziwa la Tanganyika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya vizimba ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais, tulishagawa vizimba na Kigoma tumeshapeleka vizimba kadhaa. Tayari tumeshaendelea kupokea maombi kutoka kwa wavuvi wa maeneo ya Kigoma na maeneo mengine ya Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika mchakato wa utengenezaji, kwa sasa vizimba vinatengenezwa, vikishakamilika basi tupo tayari kuvigawa kwa wananchi wa Kigoma, kwa bahati nzuri tayari orodha yao tunayo ambao wanahitaji na tunaendelea kuhamasisha wananchi wote wa maeneo ya Kigoma kuzunguka Ziwa Tanganyika ambao wana uhitaji kwa sababu kule Tanganyika tulishajua vizimba vinatakiwa kwenda wapi. Sasa, kwa sababu tumeshajua na maombi yanaendelea kupokelewa, tunaendelea kuhamasisha wavuvi wa maeneo hayo waendelee kuomba, ili vizimba vitakapoanza kutoka basi vitoke kwa wakati unaostahili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela.

Na. 122

**Kukopesha Vifaa vya Kukaushia Samaki na Dagaa**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kukopesha vifaa vya kukaushia samaki na dagaa pale ambapo mwananchi anahitaji kukopa?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na tathmini kwa lengo la kuona uwezekano wa kupanua wigo wa mikopo hiyo kwenye maeneo ya kati na juu ya mnyororo wa thamani, ikiwa ni pamoja na uchakataji wa samaki ikiwemo dagaa, ambapo, kwa sasa yanapotokea mahitaji ya mikopo inayohusu uchakataji ikiwemo ukaushaji wa samaki, Wizara kupitia dawati la sekta binafsi, inatekeleza jukumu hili kwa kuwaunganisha waombaji hao kwenye taasisi za kifedha zenye masharti rafiki na nafuu, ikiwa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* ili waweze kukopa vifaa kulingana na mahitaji yao vitakavyowawezesha kuendeleza shughuli zao za uzalishaji mali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali bado inaendelea na tathmini kuona namna ya kuweza kupanua wigo, kuweza kutoa vifaa vya kukaushia kwa wananchi hao. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kutumia miundombinu iliyoko katika vyuo vyetu vya *VETA* pamoja na vile Vyuo vya Uvuvi vya *FETA* ili wananchi hao waweze kuvitumia na baadaye waweze kuwatambua na kuwapatia vibali kwa ajili ya biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Serikali inatekeleza mradi wa *smart cities* na wameshatoa zaidi ya bilioni 33.5 katika Manispaa ya Ilemela kwenye Mwalo wa Igombe, Kayenze Ndogo pamoja na Kirumba. Je, haioni sasa ni vizuri kutumia fedha za ndani kuweza kuboresha maeneo yale ya kukaushia samaki, ili kuweka miundombinu hiyo wakati Serikali inajipanga na tathmini ya kuweza kupata hiyo? *(Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze na hili la kwanza la kutumia *VETA* zetu na vyuo vilivyopo katika maeneo hayo. Huu ni ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupokea tutakwenda kuufanyia kazi tuone namna ya kushirikiana na *VETA* kama tunaweza tukafikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, niiombe sana Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela kwa sababu kweli ni kwamba mazao haya ya samaki, dagaa, samaki na kadhalika hata Halmashauri wanapata kipato, kama kuna uwezekano wa kutengeneza maeneo ya kukaushia dagaa ili waweze kukusanya ushuru vizuri ni vizuri wakaliona hilo katika Kamati zao. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi ambayo ipo katika Halmashauri, anahudhuria vikao hivyo, wanaweza wakapanga bajeti kidogo kwa ajili ya kusaidia walau kwa kuanzia. Watakapoanza Wizara tutatuma wataalam wetu kuja kuona namna ambavyo Wizara ya Uvuvi inaweza ikasaidia kuyaandaa maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa nimekuona.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wananufaika na fursa ya mikopo ya vizimba na fursa zingine ambazo zinapatikana ndani ya Wizara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikopo hii ambayo inaendelea kugaiwa ya vizimba, boti na nyenzo zingine za uvuvi kwa kweli walemavu wanapewa kipaumbele. Tukikuta kuna mlemavu ambaye anahitaji huduma hii Wizara tunampa kipaumbele zaidi, kwa haraka zaidi na atapata mkopo huo kwa haraka zaidi. Kwa bahati nzuri tayari tumeshapokea maombi ya walemavu kadhaa na tayari tumeshayatoa kwa upande wa Mwanza na tunazidi kuhamasisha kwa maeneo mengine kama kuna wengine tuko tayari kushirikiana kwa hilo.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija siyo wakati wa taarifa. Sasa hivi ni wakati wa maswali.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** *No,* kuna jambo limetokea hapa sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Kama una swali la nyongeza ungesimama tu.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Hapana siyo swali. Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija, kaa basi baadaye.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makosa yamefanyika hapa ndiyo maana ninataka nisahihishe hapo, ombi langu ni hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija unaweza ukauliza kwa mpango mwingine kama ni swali la nyongeza, lakini siyo taarifa.

Tunaendelea nilimwona Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Kilwa ni Wilaya ya kimkakati ambayo inaongoza kwa uvuvi wa samaki katika Bahari ya Hindi. Je, ni lini Serikali italeta vifaa vya kukaushia samaki na dagaa katika Wilaya hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba wavuvi wa dagaa wana uhuru wa kuungana kwa pamoja na kwa sababu Serikali bado tunaendelea na mazungumzo na Benki yetu ya *TADB*, tuone namna ya kuwawezesha wavuvi hao ili waweze kupata vikaushia vya dagaa. Kwa kuanza niiombe Halmashauri ya Kilwa ione kwa umuhimu wake na kwa sababu wanapata mapato kupitia wavuvi hao, waone namna ya kuanza, walau kwa kutengeneza miundombinu hiyo ili na sisi Wizara tukija tuje tukamilishe kwa kuwapatia vifaa hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni kwa nini Serikali isiwe na programu maalum ya kuwakopesha

wavuvi wadogo zana za uvuvi ikiwemo nyavu ili waweze kuepukana na uvuvi haramu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tayari Serikali imeshaanza kukopesha wavuvi nyavu, boti na vifaa vingine kupitia mpango ambao Mheshimiwa Rais aliuzindua hivi karibuni. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge ana wavuvi ambao wanahitaji vifaa hivi Wizara ipo tayari kuendelea kukopesha na tunaendelea kuvitoa, hata mwezi ujao tutaendelea kuvitoa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. nikushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tunamalizia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 123

**Sheria na Uratibu Kupunguza Ajali Barabarani**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kuweka Sheria na Utaratibu mzuri wa kupunguza ajali za barabarani zitokanazo na uzembe wa Madereva?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kwa sasa linasimamia masuala ya usalama barabarani kwa kutumia Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Katika mkakati wa kuboresha sheria hii ili kupunguza ajali za barabarani Serikali imekusanya maoni kutoka kwa wadau na sasa inamalizia kuyafanyia kazi na baada ya hapo itawasilisha Muswada wa Sheria Bungeni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, ni hatua zipi zinachukuliwa na Serikali ili kuhakikisha zinawadhibiti madereva wazembe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuhakikisha sheria hii inakuja Bungeni ili kudhibiti ajali za barabarani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri hayo ndiyo maswali ya kibunge. Ahsante sana Mheshimiwa Amina kwa mfano.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kuhusu hatua kwa madereva wazembe. Kwanza ni kufutiwa leseni kwa dereva ambaye anaendesha gari kwa uzembe na kusababisha ajali. Hatua ya pili, ni kufikishwa mahakamani na ikithibitika pia ni kifungo jela na hatua ya tatu ni kulipa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, dhamira ya Serikali kweli ni kuhakikisha kwamba ajali za barabarani zinapungua ama zinakwisha kabisa, ndiyo maana tumekusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunarekebisha sheria hii ili kupunguza ajali hizi. Nikuhakikishie tupo hatua za mwisho kabisa tayari kwa kuleta Muswada wa Sheria hii Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, nimewaona.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi. Waziri anasema nini juu ya fujo ya matumizi ya barabara hasa kwa upande wa bodaboda ambapo watu wengi sana hupata ajali na juzi hapa Mbunge mwenzetu

alikuwa amepanda boda boda akagongwa na amepata ajali. Je, nini mtazamo wa Serikali kuhakikisha biashara hii inaendeshwa kwa utaratibu mzuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo la nyongeza hapo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Gulam Tarimba Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa watumiaji wa barabara wote, watembea kwa miguu pamoja na waendesha vyombo vya moto kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani ili kuepusha ajali ambazo siyo za lazima na matumizi bora ya barabara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwa kuwa bado kuna ajali nyingi kwa abiria zinazotokana na madereva wa bodaboda, ni lini Serikali itakuja na kipengele kwenye sheria cha kulazimisha uvaaji wa kofia ngumu kwa abiria pamoja na madereva wa bodaboda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha maarufu kama Bi. Mshua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sheria iliyopo sasa ina mapungufu, haimlazimishi hata abiria kuvaa kofia ngumu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika maboresho haya tunayofanya sasa ya hii Sheria ya Usalama Barabarani, jambo hilo tumelizingatia ili kuhakikisha kwamba itakuwa ni lazima sasa kuvaa kofia ngumu kwa ajili ya usalama wa dereva pamoja na abiria anayepanda bodaboda pamoja na dereva bodaboda. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija nitakupa, ngoja nimalize matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru wote kwa maswali mliyouliza na Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu, sasa ni wakati wa matangazo. Kuna tangazo la wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii, wapo waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi Mbunge, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni viongozi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria; Ndugu Franklin Rwezimula - Naibu Katibu Mkuu; *DCP*. Neema M. Mwanga - Mkurugenzi Idara ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi; Ndugu Mbaraka R. Stambuli ambaye ni Mkurugenzi Idara ya Sera na Mipango; Ndugu Nkansori M. Sarakikya - Mkurugenzi wa Haki za Binadamu; Ndugu Jane Lyimo - Mkurugenzi wa Katiba na Ufuatiliaji wa Haki; Ndugu Esther Msambazi - Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria; Ndugu Remida Lulambo - Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimaliwatu na Ndugu Felix Chakila - Mkurugenzi Msaidizi wa Usuluhishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni nane ambao ni Wabunge kutoka Bunge la Congo; Mheshimiwa John Banza Lunda, Kiongozi wa Msafara na Mwenyekiti wa Mtandao wa Maendeleo Endelevu *(SDG);* Mheshimiwa Bosco Pendani - Mbunge; Mheshimiwa Enock Nyamwisi - Mbunge; Mheshimiwa Tania Mokolo - Mbunge; Mheshimiwa Jethro Muyombi - Mbunge; Ndugu Richie Muhozi - Msaidizi wa Spika; Mheshimiwa Said Mshana - Balozi wa Tanzania nchini Congo na Wakili Joseph Laizer - Afisa Mwandamizi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Congo. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Bukombe, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi - Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni Wastaafu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti - Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Waheshimiwa Madiwani pamoja na Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya kutoka Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa - Naibu Waziri wa Madini ambaye ni mpiga kura wake kutoka Longindo, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Joseph George Kakunda ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Madiwani, Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la *Christian Embassy* kutoka Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambaye ni Padri kutoka Geita Mjini. Karibu. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki ambaye ni mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Juma Hadam Omar, familia yake kutoka Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ambao ni walimu sita na wanafunzi watatu wa *Feza Primary School* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 30 wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga ambao ni Wanachama wa Taasisi ya Fata VICOBA Endelevu, kutoka Jijini Da es Salaam. *(Makofi)*

Kuna wageni 45 wa Mheshimiwa Juliana Shonza ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kutoka Wilaya ya Songwe. *(Makofi)*

Tuna wageni 109 wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ambao ni wanafunzi 104 na walimu watano wa Shule ya *St. Anne Marie Academy*, kutoka Jijini Dar es Salaam. Katika hao kuna wanafunzi wa darasa la saba ambao wamehitimu na ambao wote wamepata ufaulu wa alama A kwa mwaka 2024. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki watoto wetu wa darasa la saba mliopata alama A na Mwenyezi Mungu azidi kumjalia Mheshimiwa Rweikiza. *(Makofi)*

Wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kuna wanafunzi 21 wa Asasi ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Kuna wanachama 32 kutoka Taasisi Isiyo ya Kiserikali, *Mutual Generation International* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 20 wanaosoma Shahada ya Kwanza ya Biblia na Theolojia katika Chuo cha Kanisa cha *Trinity College of Theology* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu kwa leo, ninampa ruhusa Mheshimiwa Khadija.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na pole sana kwa *interruption* ambayo imetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali la Mheshimiwa Stella Ikupa linajibiwa, Mheshimiwa Mnyeti ambaye ni Naibu Waziri alitamka maneno ambayo kwa sasa hatuyatumii. Maneno ambayo yametumika yalikuwa ni walemavu, walemavu, walemavu na neno sahihi ni watu wenye ulemavu. Unapokuwa unazungumzia watu au mtu maana yake ni lazima utangulize mtu mwenye ulemavu ama watu wenye ulemavu, lakini yeye alikuwa akizungumza walemavu, walemavu, walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni lazima utangulize utu, kwa hiyo, ninaomba mwongozo wako. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija, ninafikiri umeeleweka na Mheshimiwa Waziri pamoja na wengine wote wataendelea kujirekebisha. Ni watu wenye ulemavu au watu wanaoishi na ulemavu; ndilo neno sahihi. Kwa hiyo, huo ndio mwongozo wangu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

## Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae. Mheshimiwa Juma Hamad Omar.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya upendeleo. Kwangu mimi ninahesabu siku ya leo kwamba ni siku ya baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo au shukrani hizo, ninaomba nimshukuru sana Mtanzania wa kwanza, raia Mtanzania wa kwanza, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu. Kwa kweli, kama kuna mtu ameitendea mema Tanzania ni Rais wetu Mama Samia Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia *Economic Diplomacy*, basi Mama Samia kaupiga mwingi kuliko yeyote hapa. Kwa nini ninasema hivyo? Jambo la kwanza tumeona utitiri wa watalii wanaoitembelea Tanzania. Zamani Wakenya walikuwa wanatupita kwa fedha za kigeni, kwa maana ya utalii, sasa hivi tunawapita mara mbili mara tatu na wageni wengi sana wanakuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitazungumza tena baadaye, lakini ninataka kuchukua nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Fedha na pacha wake Waziri wa Mipango. Ama kwa kweli, kama kuna watu Mama Samia aliwaotea kuwachagua, hawa wawili wanastahili sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa Naibu Waziri wa Fedha, nimefanya kazi na Mawaziri wa Fedha wengi sana, lakini siku zote ninamwambia ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Kama kuna Waziri wa Fedha ameitendea haki nchi hii, mmoja ni wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Waziri wa Mipango kwa kweli anaitendea haki. Ninakukumbuka alivyokuja

ukai-*feed* Kamati ya Bajeti, kwa kweli tulitosheka. Ni Waziri wa mwanzo ambaye pamoja na mipango yake mizuri lakini anataka kutengeneza kitu kinaitwa dira ya mpango. Sasa, huko nyuma hakuna Dira ya Mpango, ni yeye wa kwanza wa kutengeneza dira ya mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi moja katika Afrika ambayo ni *top ten in economies.* unapozungumzia *top ten economies* za Afrika unaizungumzia Tanzania. Kwa nini tumefika hapo? Tumefika hapo kwa sababu ya Mama Samia. Yeye amezungumza na mataifa mengi ya nje, hasa mataifa yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tu alikuwa Urusi; hivi Juzi tu alikuwa China, amekuwa Marekani, amekuwa nchi duniani akiitangaza Tanzania kiuchumi. Ninadhani kwa kweli kama kuna nchi 10 za mwanzo, yeye ni nchi ya 10. Kama kuna nchi 10 za mwanzo katika uchumi wa Afrika, kwa maana ya zile *Big Economies;* mwanzo tunazungumzia *South Africa*, pili tunazungumzia Egypt *(Misri)*, ya tatu tunazungumzia Algeria, ya nne tunazungumzia *Nigeria*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nigeria* ni *big economies*; lakini tofauti ya *Nigeria* na Tanzania, ni *very interesting*, ninataka mnisikilize vizuri sana hapa. *Nominal GDP*, Pato la Taifa kinamba, siyo *really*, maana kuna kitu wataalam wanasema *nominal* na kuna kitu kinaitwa *really.* Hii ninazungumzia *nominal GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nominal GDP* ya *Nigeria* ni *199.7 billion dollars, while as that of Tanzania* ni *79.86 billion dollars*. Tunapitwa, sisi tuko wa 10; lakini tazama sasa, *the per capita Income* (wastani wa pato la mtu mmoja mmoja), *Nigeria* ni dola 877, lakini Tanzania pato la mtu mmoja ni dola 1,200. Tunategemea pengine ikifika mwaka 2030 pato hili litaongezeka hadi kufikia dola 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini imekuwa hivyo? Ni kwa sababu Tanzania ni tulivu; utawala ambao unaendeshwa ni utawala wa kisheria. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, tangu wakati wa Baba wa Taifa hakuna vita, hakuna mgogoro,

watu wanakwenda vizuri, watu wanaelewana. Tanzania ni tulivu na ndiyo maana tumefika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti wa *IMF* na *World Bank*, ifikapo mwaka 2035, nchi nyingi za Kiafrika zitakuwa zinafanana na za *Europe* na *USA*. Hilo ni jambo zuri; kwamba, *prediction* huko tunakokwenda ni kuzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumzie habari ya *SGR*, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia. Sasa, mimi ninaiangalia *SGR* kama ni ukombozi mkubwa, lakini *so far* tumeona kwamba *SGR* inasafirisha abiria, haisafirishi mizigo. Kwa kweli, ili reli ipate faida ni lazima i-*concentrate* zaidi na kusafirisha mizigo. Sasa, tumemamilza *lots* mbili hizi; kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Makutupora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, vipande hivi viwili, ninataka mnifahamu vizuri hapa; ninasema vipande hivi viwili ni asilimia tu tumekamilisha, asilimia 14.3 ya reli yote hiyo ambayo inatazamiwa kujengwa. Urefu wa reli ninafikiri kama sikosei ni kilometa 5,089, lakini vipande hivi viwili vimechukua *only* kilometa 722. Kilometa 300 kutoka Dar es Salaam – Morogoro, kilometa 422 kutoka Morogoro – Makutupora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa hesabu za kawaida, *simple arithmetic*, kama umemaliza 14.3% ya reli, umeshajenga iko tayari, utekelezaji ni 99%. Umetumia shilingi za Kitanzania trilioni 7.4, je, kumaliza yote? Unakuta utatumia shilingi trilioni 52.8. Shilingi trilioni 52.8, ni fedha nyingi sana. Kwa mfano, kama ingekuwa hii reli yetu inachukua watu tu, basi itachukua zaidi ya miaka 800 kulipa. Kwa hivyo, bado tunasema inafaa sana tuendelee kusafirisha mizigo kuliko watu. Tusafirisheje? Kuna mambo matatu hapa ninashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, hizi *corridors* tatu, kuna ile *Northern Corridor* ambayo inatoka Tanga – Musoma, inakwenda pale mizigo inachukuliwa inayokwenda *Uganda* na kadhalika. Kuna hii *Corridor* ya Katikati *(Central Corridor)* ambayo kama sikosei ina-*connect* Tabora – Isaka – Mwanza na pale Isaka patakuwa na Bandari kavu; ina-*connect* Uvinza – Malagarasi –

Msongati na ina-*connect* Kaliua – Mpanda – Kalema. Kuna hii *Southern Corridor* ambayo itakuwa inakwenda kutoka Mtwara – Mbamba Bay; lakini tusisahau kupitia kwa rafiki yangu yule Mbunge wa Ludewa, ili kubeba chuma cha Liganga na makaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hapa ninapendekeza mambo matatu. Kwanza, tu-*concentrate* kwenye kupeleka mizigo katika hivyo vipande ninavyosema; la pili, kuna kitu kinaitwa *open access*. Sisi watu tuliotembea Ulaya, unaweza ukakuta ile njia ya reli ni Serikali, lakini unakuta mabehewa kwa mfano ya Shabiby na Bakhresa. Kwa hivyo, unawapa nafasi *Private Sector* kushiriki katika reli. Bila shaka *Private Sector* hatobeba abiria, *interest* yake kubwa ni kubeba mzigo, kwa hivyo, inaipunguzia mzigo Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, vipande hivi vilivyobakia, Serikali isijibebeshe mzigo, kuna haja ya kwenda katika *PPP (Private-Public Partnership*. Ninadhani ushauri wa mambo hayo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ninataka nizungumzie habari ya nishati. Kwa kweli kama kuna sekta tumefanikiwa, *I recognize the presence of* Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pale. Kama kuna sekta tumefanikiwa katika Tanzania ni Sekta ya Nishati. Mradi wa Julius Nyerere ni ukombozi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *by the time*, sasa hivi tumeshamaliza vinu vitano kama sikosei bado vinu vinne; tumekwishasimika vinu vitano bado vinne. *By the time* tunamaliza *we will have 2,200 Megawatts* za Julius Nyerere. Kwa hivyo, itatosheleza hapa ndani, hivi sasa tunatosheka na huu umeme uliopo na tutauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa ninamtania rafiki yangu Waziri wa Kilimo nikamwambia, *there will be no sugarcane in future* na sasa hivi simtanii lakini ninamwambia ukweli Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwamba hakutakuwa na *energy gap; there will be no energy gap* na *excess* tutauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri pamoja na mapendekezo hayo bado kuna tatizo. Tatizo gani? Upotevu wa umeme sasa hivi ni kwa kiwango cha 14%, lakini *allowable loss in energy* ni kama asilimia nne. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba, huu mradi unaoendelea na unaendelea sana, katika Mkoa wa Dar es Salaam, wa gridi imara, uendelee kwa mikoa mingine; kwa maana ya kubadilisha miundombinu ya umeme ambayo ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, ninajua alikwishalifanyia kazi, ninalisema tu hapa, suala la *geothermal*, suala la *geothermal*; wanasema nguvu joto. Wenzetu Kenya wameshatumia *advantage* ya kuwa na *geothermal*; ninadhani kama sikosei, *is the only country in Africa* ambayo inatumia *geothermal energy* na kama sikosei inazalisha *megawatts* 891.8. Ninafikiri *more than* 90% ya mahitaji ya umeme Kenya wanaipata kwa *geothermal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninafikiri tunge-*concentrate* kwenye hili. Ninashukuru kwamba hivi karibuni alikuwa na kongamano ambalo liliwashirikisha watu wengi kwa ajili ya kuzungumzia *geothermal*. Ninasema hilo ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna sababu mbili za kwa nini tuwe na *geothermal*. Kwanza ile *Rift Valley* si kwamba iko Kenya tu, ime-*extend* mpaka Tanzania. Pili, ukienda kisayansi *geothermal* inatokana na *many rocks*. Majabali mengi haya yanatoa *geothermal*. Kwa sababu majabali mengi haya yanakuwa yana-*undergo radioactive decay*. Sijui tutasema nini, lakini inatoa mionzi hii mitatu ya *alpha, beta* na *gamma*. Inapotoa hiyo ina maana pia kuna uwezekano wa kuwa na *geothermal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, maeneo yale ya Singida na Manyoni kwenye *Rift Valley* kuna mawe mengi kama mnapeleleza. Kwa hivyo, ni njia ya pili ambayo inawezekana kupatikana kwa *geothermal* na inawezekana tukapata *more than 891,000 Megawatts* hata kuliko za Kenya. Ninadhani hilo ni jambo zuri na ninashukuru kwamba amekwishafanya kongamano la...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa kengele yako ilishapiga.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishia hapo lakini ninasema kwa asilimia mia moja ninau-*support* mpango na nina-*support* mwongozo wa mpango. Ninakushukuru sana na ninawatakia kila heri Mawaziri hawa wawili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hamad Omar. Nilimtaja Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla, kwa jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Serikali, hasa kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo inaendelea mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake kubwa ameendeleza miradi ambayo mtangulizi wake aliianzisha, kitu ambacho hakikuwa rahisi. Tumeshuhudia miradi mikubwa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, Reli ya *SGR* ambayo inaendelea mpaka sasa, Mradi mkubwa wa Kigongo – Busisi, yote hiyo imekuwa ikienda vizuri na upanuzi wa bandari kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujikita kwenye maeneo ya kiuchumi ambayo Serikali ni lazima tubadilike tuanze kuangalia vyanzo vipya vya mapato, ambavyo vitaisaidia Serikali kupata fedha na kujitegemea yenyewe bila utegemezi wa kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia Mpango wa Taifa kama ulivyo sasa na niliishauri Serikali kuhusu uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Misitu kwa ajili ya uvunaji wa *carbon credit*. Nchi yetu ina misitu mikubwa sana, tuna takribani misitu ya hekta milioni 48. Ni msitu mkubwa na asilimia kubwa ya nchi yetu

tumeimiliki hiyo misitu kupitia hifadhi za Taifa, misitu inayomilikiwa na Serikali kupitia *TFS* na misitu inayomilikiwa na Serikali za vijiji. Maeneo haya hatujayafanyia kazi vizuri. Nilikuwa ninaishauri Serikali tuwekeze miradi ya uvunaji wa hewa ukaa ambayo italeta fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule Wilaya ya Tanganyika toka tumeanza mradi huu tumepata takribani shilingi bilioni 22 ambazo zimeenda kwenye Serikali za vijiji. Sasa Serikali kama itawekeza tukaitumia misitu tuliyonayo ya Hifadhi ya Taifa, ya *TFS* tukaenda kwenye uvunaji; tani moja ni shilingi 168,000. Ukizidisha pekee kwenye eneo la misitu kwa nchi nzima tunaweza tukapata karibu shilingi trilioni 19 mpaka 20 ambazo zinaweza zikachangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya kayafanyieni kazi. Tena utafiti tulioufanya ni kwa ile bei ambayo ni ya dhuluma, lakini Serikali kama itakita na ikawekeza na ikafanya utafiti wa kina tukapata wawekezaji wa kutoka kwenye *source* halisi, tunaweza tukapata mapato makubwa sana. Kwenye eneo hili naomba Serikali mlifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kutengeneza uchumi wa nchi baada ya uwekezaji mkubwa tuliyowekeza kujenga reli ya *SGR* ambayo imetoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na inaenda mpaka Kigoma, inaenda hadi Mwanza na inaenda mpaka maeneo ya Karema. Ili tuwe na uchumi imara ni lazima tuwe na mikakati ambayo itajenga msingi wa kuhodhi uchumi wa Congo *(DRC)* kupitia nchini kwetu. Ninawapongeza Mawaziri wote kwa mpango mliouleta, lakini nikupongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwenye kipindi kilichopita, Kamati yangu ya Miundombinu ilileta mapendekezo kwa ajili ya kuachia *wharfage* kwa ajili ya bandari. Mmefanya hivyo tunawapongeza sana pamoja na Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine tulishauri waache kwenye eneo la viwanja vya ndege, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na tunawaomba mwakani wajitahidi wawaachie *passenger service charge* ili hizi taasisi ziweze kujiendesha zenyewe. Kwenye maeneo haya tunahitaji sasa waelekeze

nguvu tuimarishe reli ya *TAZARA* ili iweze kuunganisha na Nchi ya Zambia. Tuunganishe mipango ya kukamilisha reli kwa ajili ya kuchukua uchumi wa Congo upitie kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Tanga inaweza ikafanya kazi kubwa na tukapata fedha nyingi ambazo zitapitia kwenye nchi yetu kwa uwekezaji mkubwa uliopo. Si mbaya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pale ambapo watakuwa na mahusiano mazuri wakaweka mikakati waende wakajenge upande wa pili wa Nchi ya Congo *(DRC)* Mji wa Kalemie wawekeze bandari ambayo itaunganisha kati ya Nchi yetu na ya Congo *(DRC)*. Wakiweka mazingira ambayo wataweka mikataba inayolinda pande zote mbili, nchi yetu ndio mnufaikaji mkubwa kuliko wale ambao tutakwenda kuwekeza uwekezaji huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lifanyieni kazi kwa sababu uchumi lazima uende ukawekeze sehemu nyingine ili uvute upitie kwako. Sambamba na hilo upande wa Nchi ya Uganda wahakikishe wanaunganisha treni itakayokuwa inatoka Dar es Salaam mpaka Mwanza kuwe na mikakati ambayo tunapeleka mzigo mkubwa sana kupitia Nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda tunapeleka mzigo mdogo sana ni kama asilimia tano, wakati tunajenga hii miundombinu ambayo inahitaji sasa kuwa na uwekezaji mkubwa kwenye maeneo yale ambayo tutachukua walau nusu ya mzigo upitie kwetu na bahati nzuri Nchi ya Uganda ipo tayari kupitisha mizigo yake kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Kwenye maeneo haya kupitia uchumi wa usafirishaji ambako tumepitisha fedha nyingi na zimetumika tunaweza tukawa na *return* kubwa ambayo inaweza ikasaidia ukuaji wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni suala la uwekezaji kwenye maeneo ya nishati. Nchi yetu ina gesi, nchi yetu ina makaa ya mawe, nchi yetu ina chuma. Eneo hili toka mimi nasoma shule, Liganga na Mchuchuma tumeisoma kwenye vitabu. Ninaamini hata wale wengine ambao mpo humu mmesoma sana juu ya mradi wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huku tuwekeze, tuweke fedha kama tulivyoweka kujenga bwawa la Mwalimu Nyerere. Eneo hili litaweza kuzalisha fedha ambazo sisi tutakuwa na uwezo wa kujitegemea. Tunaishauri Serikali, wakati fulani wenzetu wazungu wanaweka mikakati ya kutudhoofisha sisi wenyewe. Sisi tunachimba makaa ya mawe, Watanzania hawautumii, lakini leo hii Kenya wanatumia makaa ya mawe, Uganda wanatumia makaa ya mawe, sisi wenyewe hatuwezi kutumia kwa sababu ya masharti. Naomba na eneo hili, ili tuweze kulinda misitu, makaa ya mawe tuyatumie yatatusaidia sana kukuza uchumi wetu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la kilimo. Watanzania walio wengi wanategemea shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi. Kwenye maeneo haya pamoja mmebainisha kwenye Kitabu cha Mpango lakini dhamira ya dhati haijawekwa ipasavyo, tunaomba wawawezeshe. Kilimo kinahitaji uwekezaji mkubwa, lakini kinahitaji suala zima la uwekezaji kwenye miradi ya umwagiliaji na kubwa zaidi ni kuweka mpango mkakati wa masoko. Maeneo haya hayajafanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye mazao ambayo yanazalishwa hapa nchini, nchi yetu itakuwa na uwezo wa kuzalisha na kupeleka nje ya nchi, tunaweza tukapata fedha za kigeni za kutosha. Maeneo haya ni vyema Serikali wakayatumia, wakawekeza ili kuwasaidia Watanzania ambao kimsingi wana nia njema na maendeleo tunayaona kwa sababu watu wanafanya kazi, tunakwamishwa na vikwazo ambavyo bado vipo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kilimo cha umwagiliaji bado hakijafanyika. Asilimia kubwa wakulima wengi wanalima kwa kilimo cha mkono ambacho hakiwafikishi mbali. Hata hicho hicho kilimo cha mkono ambacho kikiandaliwa kuna tatizo kubwa kwenye masoko. Mazao mengi yanakosa masoko yenye uhakika. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha tunaweka mipango mkakati ambayo itawasaidia Watanzania kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Nilimtaja Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Bahati Ndingo wajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kulihutubia Taifa kutoka Bungeni. Awali ya yote nipende kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili ambao wametuletea mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na vilevile mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza nikasema kwamba haya mambo mawili ambayo yameletwa mbele yetu yanalenga kuwatafutia Watanzania maisha bora kwa Watanzania wote. Kadhalika inaweka misingi inayohusu utawala bora katika Taifa letu na vilevile utawala wa sheria na tatu mipango hii yote inalenga kujenga uchumi imara kwa watu wetu, lakini vilevile kwa Taifa na kutuwezesha kuhimili mashindano ya kiuchumi ambayo yanatokea duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inakuwa kwa haraka sana katika masuala mazima ya kiuchumi. Tunaambiwa kwamba uchumi wa nchi yetu unafikia asilimia 5.8 ukuaji wake na hata *World Bank* wanaangalia uwezekano vilevile tunaweza tukafikia asilimia sita. Hii ni mipango mizuri ambayo inatokana na Mheshimiwa Rais na lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutuwekea mifumo ambayo inahakikisha Tanzania inaendelea kutajwa na kutajika. Sasa hivi tunasikia Tanzania ni moja kati ya nchi 10 barani Afrika inayofanya vizuri katika uchumi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashawishika kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kufanya vizuri zaidi ya hivi ambavyo tunavyofanya hivi sasa. Kauli yangu hii ninaiangalia ninapofanya mlinganisho wa uwiano wa kodi na fedha zile ambazo tunazoziita za uchumi *(GDP)*. Tanzania sasa hivi tumepiga hatua kwenye makusanyo yetu au uwiano kutoka 11.8% mwaka 2022/2023 na kufikia 12.5%. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu,

hongera sana kwa Serikali na ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia mpango wa uchumi wa miaka mitano ambao unakwenda kutamatika mwakani, tulikuwa tumeazimia tufikie uwiano wa 14% na sasa tupo 12.5%. Sasa sijui Serikali itakuja na mpango gani thabiti ambao utatuhakikishia kwamba yale malengo tuliyoyaweka ya kufikia 14% tunayafikia. Ni ndoto yangu kuiomba Serikali ije na mipango ambayo itatupeleka hadi 15%, kwa sababu kwa mujibu wa Benki ya Dunia uwiano wa 15% ile *ratio* ya *tax to GDP* ya 15% itatuondolea umaskini katika nchi hii na itaukuza uchumi wetu na hiyo inawezekana. Nasema hivi nataka niguse jambo moja dogo sana, lakini ni kubwa unapoliangalia katika masuala mazima ya kukuza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ufanyaji wa biashara, wafanyabiashara wanapolipa kodi ni kawaida wanatakiwa wafanyiwe kitu kinachoitwa *tax audit*. Maana yake ni kuleta uhakika kwamba *TRA* inapitia kodi zote zilizolipwa na mfanyabiashara yule na hatimaye kuweza kuangalia maeneo ambayo pengine kodi haikulipwa kiukamilifu. Naomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, anisikilize vizuri; tafadhali sana haya mazungumzo anisikilize vizuri. Sasa hivi utaratibu wa *TRA* ukishafanya biashara na ukimpelekea hesabu zako za mwaka zilizokaguliwa yeye atakaa akusubiri mwaka wa pili haji, mwaka watatu haji, anakuja ukishakamilisha hesabu za miaka mitatu. Binadamu siku zote huwa anafanya makosa, mengine ya makusudi na mengine ya kupitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakikufanyia *tax audit* ya miaka mitatu unaweza ukajikuta umefanya makosa mengi ambayo yana-*attract*, yanaleta adhabu, yanaleta na *interest* ndani yake kiasi kwamba deni ambalo ulikuwa ukidaiwa linakuwa kubwa na huwezi ukalihimili kama mfanyabiashara. Kuna mambo mawili yatatokea; namba moja, unamlazimisha mfanyabiashara ambaye anataka na yeye kuishi azungumze na watu wa *TRA*. Tumeyaona, wengi sisi ni wafanyabiashara humu ndani, unapelekwa kwenye kona lazima uzungumze na ninaposema

kuzungumza nafikiri mnanielewa na ili uishi lazima uzungumze na ukizungumza angalau unapata unafuu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninachojaribu kusema hapa ni nini? Kama tunahitaji kodi za Serikali na fedha za Serikali ziingie Serikalini kwa wakati, kuna ugumu gani kufanya *tax audit* ya kila mwaka? Jibu wengine wanaweza wakakwambia wafanyakazi hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana vipi leo tukawa na Afisa Maendeleo kila kata, tunao watu hao. Tuna Afisa Ugani, tuna Afisa gani, lakini waelewe kitu kikubwa ni mkusanyaji wa kodi za Serikali kwa usahihi na kwa wakati. Sasa watu hawa sisi hatuna wa kutosha ni afadhali tukajihakikishia tutafute watu wa kutosha kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanakuwa *assessed* kila mwaka na kodi zao zinalipwa kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? Kwa sababu zile ni fedha za Serikali unaziweka, ukimbambikizia mtu kodi na hakuridhika ndio sababu wanakwenda kwenye Mahakama. Hela za Serikali zinaendelea kukaa kule na ubaya zaidi wanaolipa vizuri ndiyo wanaokamuliwa sana. Sasa ushauri wangu, Serikali ijikite kwenda kuangalia mambo mawili; *number one*, kuja na mipango ambayo kweli itakwenda kutupandishia uwezo mzuri wa kukusanya fedha za Serikali kwa maana ya kodi, lakini la pili, walete mfumo wa kuwa na *tax audit* ya kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VAT* tuliizungumza sana katika mjengo huu, katika Bunge hili, utaratibu wa kudai na kutoa risiti. *EFD* mashine zile za kutoa risiti zilianzishwa tangu mwaka 2010, miaka mingi sana iliyopita. Kauli ni kwamba tutoe elimu na elimu inatolewa. Sasa hii kama ingekuwa ni elimu hata ya *PhD* saa hizi mtu angeshamaliza hata *PhD* sijui ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si rahisi mtu kulipa kodi anavyopenda kwa sababu unachukua hela yake hivyo kungekuwa na mifumo ya kidijiti. Tujifunze waliofanya vizuri katika *VAT* kuwa na mifumo mizuri ya kidijiti inayomlazimisha mtu kutoa risiti, tuondokane na suala mpaka uombe. Kuna utaratibu upo

*stock management* waende wakajifunze katika nchi ambazo zinafanya vizuri katika vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la pili na hapa nataka tujikumbushe muasisi wa Taifa letu Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere aliwahi kuyasema maneno haya miaka takribani 50 iliyopita. Alikuwa anasema, ili tupate maendeleo akaweka vitu vinne na kila mtu anajua humu ndani, naomba niviseme; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Katika kipindi tulichonacho sasa hivi, najua watu wapo, ardhi ipo vitu viwili tu vya kujiuliza; je, tunayo siasa safi? Tuna uongozi bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, Taifa la Tanzania linapita katika kipindi kizuri sana ambapo vitu vyote vinne vipo: watu tupo, ardhi ipo, siasa safi aah! Hiyo tena huwezi kuuliza, ndani ya Chama Cha Mapinduzi tuna siasa safi, lakini ukiangalia uongozi bora, tuna uongozi bora sana katika kipindi hiki cha Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let's take advantage*, tuchukue muda huu kuimarisha zaidi uchumi wetu. Katika *point* hii naomba nizungumzie jambo langu kule la jimboni ambalo linaweza likatumika Tanzania. Kinondoni ni eneo ambalo linakua haraka sana kimaendeleo. Kinondoni hatuna ardhi sasa hivi hata ya kujenga hatuna, ni nyumba ya zamani ujenge mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa shughuli za Kinondoni ni biashara sana. Watu wakinunua nyumba kuzigeuza; na ninaomba mchukue mfano wa eneo kama la Kijitonyama, limekuwa ni kama mkoa. Kiuchumi ni eneo kubwa sana, ni kata tu lakini ukinunua nyumba pale lazima kuna ule utaratibu uende manispaa uombe *change of land use* ambayo na yenyewe ni balaa kubwa sana; inakuchukua muda, inachukua fedha, uzungumze, ufanye vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mawaziri na Serikali mliopo hapa tengenezeni utaratibu katika mipango ya maendeleo, angalieni miji inayokua kwa haraka *declare;* itangazeni miji ile kwamba ni miji, maeneo yake ya makazi iwe pamoja na biashara

ili kuondoa kikwazo cha kuomba idhini ya kubadilisha matumizi ya biashara (*change of the land use)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba Serikali anzeni na Kinondoni limeiva! Tena siyo Kinondoni kama Wilaya, Jimbo la Kinondoni limeiva kuanza kuli-*declare* kutangaza eneo lile kama ni eneo la makazi na biashara na viwanda. Ili mtu akinunua nyumba moja kwa moja anachohitaji ni kwenda kupata *building permit* avuke ule utaratibu wa kwenda kuomba *change of land use*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukifanya hivyo maana yake tutasaidia watu, tutasaidia uchumi, tutaongeza kodi na Serikali yetu itafaidi maendeleo kwa haraka zaidi kwa watu wake, na itatimiza lile lengo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaangalia muda, tayari! Bado sana.

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize na eneo la tatu kuhusu Barabara. Barabara ni mali ya Serikali, barabara moja kipande cha kilomita moja kinafika shilingi bilioni 1.2, ni gharama kubwa sana. Kama ni nyumba, ni nyumba ya maana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga Barabara, lakini kuna kitu kimoja *very important,* ukarabati wa barabara katika barabara zetu ni *very poor,* ni mbaya mno. Miaka ya nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa *PWD (Public Works Department)* kazi yao asubuhi wakiamka wanatembea kwenye barabara wakikumbana na shimo wanalitengeneza pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii barabara za Tanzania zinaharibika, zinakaa miaka miwili, mitatu, minne shimo linakuwa halafu baadaye wakandarasi wale wa kujitegemea wanakuja wanatengeneza, baada ya mwezi, inaharibika tena hali hiyo siyo

nzuri kwa uchumi wa nchi. Tunatumia fedha, lakini hatukarabati barabara zetu. Hiyo ni *TRM,* zamani kulikuwa na *Trunk Road Maintenance* halafu kulikuwa na *RRM (Rural Roads Maintenance)* zote hizi hazipo, waliopo sasa hivi ni ukandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ibadilishe ifanye utafiti iangalie ni kwa jinsi gani itakwenda kuboresha barabara zetu ili maendeleo ya Taifa letu yaweze kutimia vizuri sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nakushukuru sana kwa muda huu. Naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Nimemwita Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mheshimiwa Janejelly na Mheshimiwa Daimu Mpakate, ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuungana na wenzangu kuchangia. Kwanza, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri pamoja na Watendaji wao wanaoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Mpango uliopita, ni Mpango ambao utekelezwa kwa miradi mikubwa mingi ikiwepo ya *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Madaraja makubwa likiwepo la Busisi, Miradi mingi ya *REA* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mikubwa ni lazima nimpongeze sana Jemedari wetu Mheshimiwa Rais, wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na wasaidizi wake wanaomshauri vizuri akiwepo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, kwa namna ambavyo wanamshauri vizuri ili kukamilisha miradi hii ambayo wote humu ndani tutakuwa ni mashahidi, baadhi ya watu walikuwa wanasema miradi hii mikubwa haitaisha. Sasa miradi hii imetekelezwa kwa asilimia

kubwa, tunapongeza sana pamoja na Baraza la Mawaziri ambao wameshirikiana kufanya kazi hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo sasa niende kwenye sekta muhimu ambazo napenda nitoe ushauri. Kwa mfano, kwenye afya, mambo mengi makubwa yamefanyika sana. Naomba waweze kuboresha zaidi ili miradi mingi ya vituo vya afya, zahanati na hospitali ziweze kuwahudumia wananchi kama ambavyo Serikali imekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye elimu kazi kubwa kwenye elimu imefanyika sana. Ombi langu ni kwamba sasa Serikali katika mpango huu tuangalie namna ya kujenga nyumba za walimu ili kuwawezesha kukaa baadhi ya maeneo ambako wanakuwa wamepangiwa. Utakuta kwa mfano, walimu wengi wakipangwa kule vijijini, hawapendi kwenda kufanya kazi huko kwa sababu hakuna nyumba. Kwa hiyo, naomba katika mpango huu Serikali ijikite kutengeneza nyumba za walimu katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuna maboma ambayo yalianzishwa na wananchi na Waheshimiwa Madiwani na Wabunge wenyewe ninyi mliopo humu ndani. Maboma hayo ni mengi kila jimbo. Ombi langu katika mpango huu muone namna ya kuunga mkono jitihada za wananchi katika maboma haya ambayo yamejengwa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu hapa juu ya madeni ya wakandarasi. Zipo shughuli mbalimbali zimesimama kwa sababu ya madeni. Sijajua tatizo ni nini Wakandarasi hawajalipwa? Ombi langu katika mpango huu tuone namna ya kuwalipa wakandarasi hawa ili waweze kuendeleza miradi ambayo inakusudiwa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo muhimu ambalo na wenzangu kadhaa wamelizungumza hapa, jambo hilo ni la siku nyingi lakini tunaishukuru sana Serikali juu ya Liganga na Mchuchuma ambalo Serikali ya Awamu ya Sita imekwenda kulipa fidia zaidi ya shilingi bilioni 15.4. Wananchi wa Wilaya ya Ludewa

Mkoa wa Njombe na Watanzania kwa ujumla tunategemea sasa Serikali katika mpango huu, muone namna ya kutia msukumo nguvu ili kuhakikisha Liganga na Mchuchuma sasa inaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mwekezaji ambaye alikuja hivi karibuni, tumetia saini ya mkataba kule Njombe. Nampongeza sana pia Mkuu wetu wa Mkoa Mtaka ambaye ameweza kumsogeza na kumkaribisha mwekezaji huyu katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyozungumza tayari ameshaanza kujenga kiwanda kikubwa cha chuma pale Makambako lakini vilevile anajenga kiwanda kingine kule Ludewa katika eneo la Mndindi. Kwa hiyo, naomba Serikali ione namna ya kuwaleta wawekezaji wengine ili Liganga na Mchuchuma iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamelizungumza hapa juu ya Reli ya *TAZARA*. Reli hii nadhani ni vizuri Serikali ione namna ya kuimarisha ili iwe kiungo cha kusafirisha mizigo na mambo mengine kama ilivyokuwa zamani. Reli hii kwa ukanda ule ilikuwa inaweza kusaidia sana. Naomba Serikali mshirikiane, sijajua kwa sababu ni ya nchi mbili, muweze kuona mnaimarisha Reli ya *TAZARA* irudi kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, katika Mkoa wetu katika mpango huu Serikali ione namna ya kuimarisha kujenga kiwanja cha ndege katika Mkoa wetu wa Njombe kwa sababu sisi Njombe ndiyo tunaolima sana parachichi ambazo zinakwenda nchi mbalimbali. Katika Mkoa huu wa Njombe na Iringa ndiyo walimaji wakubwa wa parachichi katika ukanda huo. Kwa hiyo, naomba Serikali katika mpango huu tunaokwenda nao sasa, tuone namna ya kutujengea kiwanja cha ndege katika Mkoa wetu wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau jambo lingine ambalo na wenzangu wamelisema zao la misitu; Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa kwa ukanda wetu huu ndiyo unaoongoza kwa misitu mingi mikubwa ya Serikali, ya watu

binafsi. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kama ambavyo wenzangu wamelizungumzia, tuone namna ya kuhakikisha tunaimarisha, tunawekea mpango kwa hili ili kusudi Serikali iweze kupata mapato yake kupitia misitu iliyopo Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tukifanya hivyo, amezungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwamba tani moja inauzwa kiasi fulani. Nadhani tukiimarisha tunaweza tukapata fedha nyingi zaidi kupitia misitu iliyopo katika ukanda wetu huu wa Njombe na Iringa na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ninazungumzia kwa ujumla wake. Tunapozungumza Serikali hii ya Awamu ya Sita pamoja na wasaidizi wake hao niliowataja, mwenye macho haambiwi aone. Kazi iliyofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita haki ya Mungu haijapata kutokea. Huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana na ninaomba Mheshimiwa Rais wetu Mungu amjalie afya njema ili mwaka 2025 inakwenda yenyewe kwa sababu kazi alizofanya katika nchi hii za mabii na mabii (mabilioni na mabilioni); na matii (matrilioni) ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Deo Sanga. Nimemtaja Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mheshimiwa Janejelly na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa nianze kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kuwasilisha mapendekezo ya mpango na mapendekezo ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa maono yake ya kuanzisha Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. Pili, kwa

kuiwezesha Tume ya Mipango ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri maono ya Mheshimiwa Rais, hasa kwenye Dira ya Maendeleo ambayo tunaendelea kuitengeneza na baada ya ukamilishaji wa dira hii itakwenda kutungiwa sheria, haya ni mapinduzi makubwa sana kama Taifa kwenye suala zima la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naenda kushauri Serikali kwenye baadhi ya mambo nikianza na hali ya umasikini na maendeleo ya watu. Kwanza, kwa sasa taarifa niliyonayo ya hali ya umasikini wa watu, tunatumia taarifa ya mwaka 2017 na 2018. Sasa ni dhahiri kabisa kwamba taarifa hii imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kwamba kwa kuwa tunakwenda kwenye maandalizi ya Bajeti ya 2025/2026, naomba Serikali ione ipo haja ya kutenga fedha ili tuweze kwenda kufanya tafiti ya kuangalia hali ya mapato na matumizi ya kila kaya ili tuwe kwenye nafasi nzuri ya kuweza kujua hali halisi ya umasikini wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tukiangalia kwenye takwimu za Sensa tunaambiwa tupo takribani ya watu milioni 61.7 na natarajia kufika 2035 tutakuwa watu zaidi ya milioni 87.5. Sasa ongezeko hili linakadiriwa kwamba kila mwaka kuna ongezeko la asilimia tatu ya watu. Pia kwenye takwimu hizo tunaambiwa kila watu 100 watu 87 ni tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba ongezeko hili la watu haliakisi na ongezeko la uchumi tulionao. Sasa ni dhahiri kwamba wenzetu wa Tume ya Mipango chini ya Wizara ya Mipango waoneshe ni namna gani ongezeko hili la watu linaakisi uchumi wa Taifa letu. Hicho ni kitu muhimu sana kwa sababu hali iliyopo siyo nzuri kama kila watu 100 watu 87 ni tegemezi. Ni lazima Mpango uonyeshe njia ya kuona ni namna gani ongezeko letu kama Taifa la watu linaakisi ongezeko la uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana kwamba Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ilieleza kwamba ili umaskini wetu upungue, tunahitaji uchumi ukue asilimia nane mpaka 10, lakini tumeona katika hili, jitihada za Serikali kwanza kwa kuboresha sera mbalimbali na kuimarisha na utekelezaji pia wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la kilimo haikwepeki, tunaambiwa watu takribani milioni 28 wana-*deal* na kilimo. Watu milioni 28 ni sawa sawa na asilimia 45.9 wana-*deal* na kilimo kile cha kawaida. Kwa hiyo, hawa watu milioni 28 natarajia katika Mpango wa Serikali nione tija ya kumaliza miradi ya kilimo kwa wakati, nione tija ya kuhakikisha masuala ya kilimo, pembejeo za kilimo, ruzuku za mbolea na kila kitu zinatoka kwa wakati ili kuimarisha kundi kubwa hili la watu milioni 28 waweze kuimarika kiuchumi na tuweze kupunguza hali ya umaskini tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hali ya umaskini na maendeleo ya watu, naomba pia niishauri Serikali, tunatamani Mheshimiwa Waziri kwamba Tume ya Mipango iwe ni *coordinator* wa Wizara zote. Kwa mfano, huwa tunakaa tunauliza sana kwenye Kamati, tunaona Wizara ya Uvuvi wanachimba mabwawa ya ufugaji wa Samaki, na ni bajeti kubwa sana, Wizara ya Kilimo wanachimba mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji, na Wizara ya Maji wanachimba mabwawa kwa ajili ya maji. Hivi ni kweli hatuwezi kutumia bwawa moja likafanya shughuli zote tatu? Inawezekana. Naomba *coordination* ya Wizara hii iwe chachu ya ku-*coordinate* mambo yote ya Wizara mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, hata kwenye mawasilino ninashukuru Mungu sasa hivi mmeanza kwa sababu ilikuwa kila Taasisi kila Mnara wa Voda, wa Tigo kumbe inawezekana tukawa na mnara moja na wale wengine wakaweka pale minara yote na mitandao yote ikawa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, miradi yetu lazima Tume ya Mipango ituoneshe miradi hii tunayoenda kuitekeleza, Serikali inayo uwezo wa miradi ile; na itachukua muda gani yote? Dira ionyeshe Mipango ili tuweze kuepuka ongezeko la riba ambayo inaigharimu sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, hata wakandarasi wetu wengi wamefilisiwa na benki, lakini hata mzunguko wa fedha kwenye benki zetu unakuwa siyo nzuri kwa kutowalipa kwa wakati. Kwa hiyo, hayo ni mambo ya msingi ambayo nilitamani nami niichangie kwenye Serikali na hususani katika Mapendekezo ya Mpango na muone haja ya mambo haya yaingizwe kwenye mipango na bajeti ili kuweza kuimarisha hali za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kupata fursa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bahati Ndingo. Naendelea na Mheshimiwa Janejelly James, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Joseph Tadayo, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa wasaa huu. Niwapongeze sana Mawaziri wetu wawili Profesa na Daktari. Kwa hiyo, ukitafuta huo mchanganyiko lazima utaleta mambo mazuri. Nawapongeza Manaibu wetu Waziri na timu zenu za wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze Mheshimiwa Rais, kwa maono yake ya kimkakati, ya maendeleo na maono yake makubwa ameyaweka kwenye kilimo na ili kukuza uchumi wa Kitaifa ni lazima mwongeze mauzo ya nje ili kupata fedha za kigeni. Tunaongezaje? Eneo ambalo ni muhimu ni hapa kwenye kuzalisha mazao ya biashara, mbogamboga, maua na matunda pendwa kama parachichi. Tukijikita huko tutaweza kuwa na uchumi ulio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema uimarishaji kwenye huu uchumi wa kilimo, ni uzalishaji wa tija, yaani eneo dogo lakini lizalishe kwa zaidi; na ukiona maono ya Serikali, haya yanapatikana, kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka minne iliyopita bajeti ya Kilimo ilikuwa ni shilingi milioni 294; leo hii tunapojadili huu mpango bajeti yake ni shilingi trilioni 1.2. Kwa hiyo, kuna haja kuona kwamba kilimo ndiyo kinaweza kikainua uchumi wetu. Hata hivyo,

bajeti kubwa ya kilimo imeenda kwenye *BBT*. Naomba, kuna haja ya *BBT* sasa kuzalisha yale mazao ya kibiashara na chakula, hasa kilimo cha mpunga. Kwa Afrika chakula cha mchele kinapendwa sana. Sasa tukijikita kwenye kulima mpunga, tutaweza kuzalisha na kuuza nje ya nchi na kupata mazao na fedha za kutosha ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye rasilimali watu. Tanzania tumepata bahati ya kuwa mama wa Lugha ya Kiswahili, lakini hapa hatujaona kwamba tunaweza tukapatumia na kupata fedha za kigeni. Lugha ya Kiswahili inazungumzwa Afrika nzima na baadhi ya nchi nyingine duniani, ila kama sisi tutaitumia na hatujaweza kuitumia fursa hii, yawezekana bado hatujaiona kama ni fursa ya kutumia wataalamu wetu na walimu wetu wa Kiswahii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuitumie hii fursa ya kupeleka walimu wa Kiswahili nje ya nchi na wataalamu wa kutafsiri Kiswahili nje ya nchi. Faida itakayopatikana ni kupata fedha za kigeni lakini na kuondoa ombwe la kutokuwa na ajira ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye rasilimali hapo hapo, kumekuwa na ombwe la kutopanga, tunaelewa rasilimali watu ndiyo kitu muhimu na kikubwa katika ujenzi wa Taifa, lakini hata hivyo kuna mgawanyiko usio sahihi kwa watumishi wetu Tanzania. Ni kwa nini watumishi hawataki kukaa wilaya za pembezoni? Hawataki kukaa vijijini, wote wanapenda kuwa mjini. Hapa kuna kitu Serikali inatakiwa ikiangalie kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani watumishi ambao walikuwa vijijini na pembezoni kulikuwa na *incentives* za kuwafanya waweze kukaa huko kwa miaka mitatu hata mitano. Sasa kuna haja ya Serikali kurudisha *incentives* hizo za watu ambao wapo pembezoni, watu ambao wapo vijijini na wilaya ambazo zipo pembezoni ili wote wasikimbilie mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu ambapo, mtumishi huyu atakapokuwa kule ni lazima sheria iseme wazi ingawa ipo lakini hatuitekelezi. Ni lazima mtumishi akae kwenye

kituo cha kazi kwa miaka mitatu. Huo msawazo utakuja vizuri. Vilevile, tuna *Human Resource Assessment System,* hii itumike vizuri ili kuweka msawazo wa watumishi kulingana. Kuwe na ulinganifu kati ya mjini na vijijini ili haya maendeleo tunayoyataka, basi watumishi waweze kuyachangia kama rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naungana na Kamati ya Bajeti, huku imetuambia kwamba iundwe Kamati ya kuangalia matumizi ya Serikali ili yaweze kuwa sawa. Mheshimiwa Bahati wakati anachangia amesema hilo, kwamba kitu kimoja kinafanywa na Wizara zaidi ya tatu; na nilishawahi kuchangia kwenye Bunge hili kwamba, Wizara ya Kilimo wanachimba mabwawa ya umwagiliaji, yaleyale wanayoyachimba yanaweza yakatumika kuvuta maji, yakatumika kwa wananchi, yaleyale mifugo, yanaweza yakafugia samaki ndani ya mabwawa hayo. Kwa hiyo, bajeti itakuwa imetumika kidogo kuliko kila Wizara kuwa na bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini hivyo kwa sababu tuna Tume ya Mipango na ndiyo maana siendi kwenye maoteo ya bajeti ijayo. Najua hii bajeti na haya mapendekezo yameletwa kutokana na Mpango uliopangwa na Tume ya Mpango. Nawapongeza sana, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kurudisha hii Tume ya Mipango, nina imani mambo yataenda kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly James.

Tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Joseph Tadayo na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi mchana huu nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri ambazo zina malengo ya kuwasaidia wananchi wetu. Vilevile, nitakuwa mchoyo wa fadhila bila kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amewasaidia wakulima wetu wa korosho kupata pembejeo nyingi sana na kufanya uzalishaji wa korosho kubwa mwaka huu tofauti na tulivyotegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru sana Waziri Bashe kwa kazi kubwa aliyoifanya, kuhakikisha *TMX* inafanya kazi. Bei sasa zimekuwa nzuri ni zaidi ya elfu tatu na kitu wakulima wanapata. Hili jambo limetusaidia kwa asilimia kubwa kuleta imani kwa wananchi wetu, na kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, kuna changamoto ambazo nawaomba Mawaziri wote wawili, pamoja na mipango mizuri ya kutoa pembejeo bure, wageuzie zoezi hili kwenye changamoto ya maghala katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vyama vingi vya msingi vinapima korosho kupitia majumba ya kupanga ya watu binafsi. Maghala mazuri ya kuhifadhia mazao haya ni adimu, na sasa hivi mvua zinakaribia kuanza, korosho nyingi zipo nje ya maghala. Tunaomba, kwenye mpango huu wasisahau kuweka mpango wa kujenga maghala kwenye vijiji vyetu ili mazao ya wakulima hasa korosho, ufuta na mbaazi yaweze kupimiwa kwenye maghala ambayo yapo katika ubora uliokuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye suala hili la korosho, naomba mtusaidie hasa Waziri wa Fedha. Kuna changamoto imejitokeza maeneo mengi kuchelewa kwa malipo kutokana na Sheria ya Fedha ya Benki Kuu inayoitaka akaunti yoyote ile ya mkulima kama haijaweza kufanya kazi ya miamala ndani ya miezi sita akaunti inafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limefanya wakulima wengi kuhangaika, fedha zao hawapati kutokana na sheria hii ambayo inataka benki zote, akaunti yoyote ya mtu binafsi, au

kampuni kama haijafanya kazi ndani ya miezi sita inafungwa. Kwa hiyo, *transaction* yoyote ya fedha haiwezi kuingia mpaka mhusika aende tena benki ili aweze kufufua akaunti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasumbua sana wakulima wetu na linasababisha wakulima wengi kujaa kwenye benki zetu. Tunaomba sheria hii kwa wakulima tu, irekebishwe, watu wengine wa kawaida au wateja wengine, ibaki kama ilivyo ili tuweze kuwasaidia hao wakulima wa korosho ambao wanapata taabu na mapato yao yanategemea korosho mwaka kwa mwaka, kwa maana ya kwamba akiuza mwaka huu anaenda kuchukua hela yake yote. Baadaye anakaa mpaka mwakani atakapouza tena korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kwa kweli mtakuwa mmewasaidia wakulima kama mtatengeneza hii sheria kwa upekee kwa wakulima hawa ili watusaidie kupata malipo yao ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kutuwezesha Mtwara kupata Barabara ya kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay*. Sasa hivi kusini tunakwenda kwa lami kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* lakini bado lipo jambo la *Mtwara Corridor* kwa maana ya reli. Reli hii itatusaidia kuhakikisha kwamba mizigo mikubwa ile ya makaa ya mawe ambayo yanapatikana Ngaka, Wilaya ya Mbinga, Liganga na Mchuchuma, mradi ambao tunauzungumzia kila siku, reli hii itasaidia kupunguza mzigo mkubwa ambao unakwenda kwenye barabara zetu na zinakuwa mbovu mara kwa mara kutokana na mzigo mkubwa unaopita kwenye barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie sana kuhusiana na barabara ni barabara yetu ya kimkakati ambayo ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Barabara ya Mtwara - Pachani na Rasi mpaka Tunduru, barabara hii ni ya kilometa 300. Tunaomba kwenye Mpango huu, hii barabara iingizwe ili ijegwe kwa kiwango cha lami kwa sababu, zaidi ya vijiji 70 vya Wilaya ya Tunduru na Namtumbo wanatumia barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bora zaidi, kwenye barabara hii tunatarajia kuwa na mradi mkubwa wa uzalishaji wa *copper*, mradi ambao unajengwa pale Mbesa na una zaidi ya shilingi bilioni 40. Shilingi bilioni 40 wanaenda ku-*invest* kwenye Kijiji cha Mbesa kwa ajili ya kuchenjua *copper* ambayo itasaidia kuongeza uchumi wa Tunduru na wa Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, barabara hii inapita katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama barabara hii itakuwa kama ilivyo, huu mradi unaweza kuchelewa kwa sababu *copper* ni kati ya madini mazito ambayo yanatakiwa yabebwe kwenye malori makubwa ambayo yana zaidi ya tani 30. Kwa hiyo, naomba sana, kwenye mpango huu uonyeshe ni lini barabara hii ya Mtwara - Pachani na Rasi – Tunduru, itaanza kujengwa ili huu mradi unapoanza mwakani uwe umekuta barabara imeshakuwa tayari ambapo itaendelea kuleta uchumi mzuri kwenye barabara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye Mkoa wetu wa Ruvuma hatuna barabara inayounganishwa na ya Msumbiji kuanzia Tunduru – Namtumbo – Songea – Mbinga mpaka Nyasa. Hakuna barabara yoyote ya lami inayoishia kwenye mpaka huu wa Msumbiji, kitu ambacho kinasababisha tukose biashara na wenzetu wa Msumbiji tofauti na maeneo mengine. Ni mkoa pekee ambao hauunganishwi na barabara ya lami na majirani zetu wa Msumbiji. Tunaomba, tuna barabara ambayo tumezungumza mara nyingi ile ya Songea. Tunaomba ile fedha ipelekwe ili iweze kutengeneza barabara ile na tuone wenzetu wanatumia barabara ile kwa ajili ya kupeleka bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda nilizungumzie ni suala la ujenzi wa soko kwenye Wilaya yetu ya Tunduru. Tunashukuru na tunawashukuru sana Wa-Sri Lanka, wawekezaji wetu waliotujengea soko kwa *PPP* la madini ambalo ni la kisasa; na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja kulizindua. Kutokana na kuchangamka kwa Mji wa Tunduru, sasa hivi tunahitaji soko la mazao mchanganyiko (bidhaa mbalimbali). Hili litatusaidia kuleta hadhi kama ilivyokuwa

soko la madini ili kufanya mji ule uendelee kuchangamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimesema hakuna barabara nyingine yoyote ya lami inayounganisha Msumbiji kutoka Tanzania tunaomba Mpango ujao uonyeshe namna gani pale Lukumbule tunaweza tukaweka soko la kimataifa ambapo mara kadhaa wanunuzi kutoka Msumbiji wa bidhaa mbalimbali wamepitia ili kuhakikisha kwamba nao wanaweza kufaidika na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ningependa kuishauri Serikali katika mpango wa matumizi ya gesi kwa nchi nzima. Tuwe na mpango, *TPDC* wapewe nguvu ya kujenga vituo vya gesi kwa ajili ya kujaza kwenye magari. Hii itatusaidia kupunguza matumizi makubwa ya mafuta. Kama kila mkoa na kila miji mikubwa kungekuwa na vituo vya gesi kwa ajili ya magari yetu, uwekezaji kwenye magari ya gesi ungekuwa ni mkubwa sana na ungepunguza matumizi makubwa ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mpango huu ili uende vizuri tuhakikisheni tunaweka vituo vya kuuzia gesi kwa maana kupunguza matumizi ya mafuta lakini kuweza kupunguza matumizi ya fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Iddi Mpate. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti wa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea hoja hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri wetu hawa wabobezi kabisa ambazo kwa

maandishi yao wenyewe wamesema kwamba zimekusudia kujenga Taifa lenye mafanikio, haki na linalojitegemea *(A prosperous, justice and self-reliant nation)* kwa kutumia maneno yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii imekuwa ikionekana kila mwaka na siyo Tanzania tu, na kila nchi, lakini mara nyingine huwa inakuwa vigumu kuona ile *impact* yake yaani kuona kabisa yale manufaa yake kama ilivyo kwenye makaratasi. Lazima nikiri kwamba kwa mara ya kwanza katika nchi yetu tumeshuhudia matunda makubwa na kishindo kikubwa cha mpango ambao uliwekwa na Serikali yetu katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ni mashahidi tumeshuhudia miradi mikubwa na ya kihistoria kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR,* na miradi mikubwa ya maji. Asifiaye mvua imemnyeshea. Kwangu mimi kuna Mradi wa Same – Mwanga - Korogwe, miradi mikubwa ya umwagiliaji na miradi mikubwa ya barabara. Kwa hiyo, kwa kweli kwa hili tunapaswa sana kuipongeza Serikali chini ya kiongozi wetu mahiri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo inawezekana sisi wa ndani kama vile ambavyo mama anaweza asione kwamba mtoto wake anakua kwa kasi, lakini majirani wakaona, yawezekana kabisa sisi ndani tusione kwa haraka, lakini wenzetu wa nje wanaona na ndiyo maana mwaka 2022 ilitolewa tuzo ya pekee ya *Babacar Ndiaye Award* kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Wenzetu walitangulia kuona kwamba huko tunakoelekea tunakwenda kupata mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshuhudia ubunifu mkubwa ambao na matokeo yake tumeyaona kama suala zima *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa Rais aliifanya na matokeo yake tumeona jinsi ambavyo utalii umekuwa mkubwa katika nchi yetu na mapato yake yanavyoongezeka kuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sasa tunafanyaje ili kuyalinda mafanikio haya na kuyafanya yawe endelevu? Mimi nina mambo machache tu ambayo ningependa kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kumlinda mkulima mdogo, yaani kufanya jitihada za makusudi kumlinda mkulima mdogo. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu nilishangaa kuona kwamba inakuwaje sisi *inflation* yetu inakuwa nzuri kuliko baadhi ya nchi ambazo tukizitazama tunadhani kwamba labda zipo vizuri sana. Nilipouliza wataalamu waliobobea kiuchumi, wakasema kwamba sababu mojawapo ni kwamba angalau sisi tuna chakula *(food security)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, chakula chetu sisi hatulishwi na ma-*settler* wala na wakulima wakubwa sana, ni wakulima wadogo. Kwa hiyo, tunahitaji kuendeleza juhudi za kumlinda mkulima mdogo kuhakikisha anapata mbolea kwa wakati, anapata pembejeo, anapata mbegu bora, anapata huduma za ugani na soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendesha gari hapa kwenda Dar es Salaam njia nzima unaviona vyakula vimepagwa, lakini vyakula vile ni vya kuharibika *(perishable)*. Baada ya wiki moja sijui wale watu maskini wanavipeleka wapi? Kwa hiyo, tusipokuwa na namna ya kuhakikisha kwamba vile viazi visipouzika moja kwa moja kwetu sisi, vinaenda kwenye kiwanda, vinaongezwa thamani halafu vinauzwa, hawa wakulima wataendelea kuwa maskini; na wakiwa maskini tutaendelea kupata matatizo ya *inflation* yetu kuvurugika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kumlinda mkulima mdogo ni suala zima la kupima ardhi tuliyonayo. Ardhi ambayo haijapimwa thamani yake ni ndogo sana. Tunahitaji kupima ardhi tujue wapi kwa wakulima, wapi kwa wafugaji, wapi kwa wachimbaji wa madini kwa sababu hizi ardhi thamani zake ni tofauti, lakini tukiacha tu ni rasihi sana kutengeneza *slums*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nchi ambazo tunafahamu zina *slums* kubwa kwenye miji, tatizo lilikuwa ni hivi hivi kwamba ardhi ilikuwa inauzwa. Mkulima ana ardhi yake anaiuza kwa bei ambayo haimfanyi hata aweze kuendelea hata ajenge nyumba bora au anunue hata trekta, matokeo yake wanaenda kuishi kwenye maboksi, tunapata matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika kulinda mafanikio haya ni suala la mfumo wetu wa elimu. Tunahitaji kufanya jitihada za makusudi ili kuendelea kuwa na mfumo wa elimu ambao unafikika kwa watu wote. Yaani mfumo huu kila mtu aweze kuifikia elimu, lakini elimu ambayo inaendana na wakati, yenye gharama ambazo wananchi wote wanazimudu, lakini yenye kiwango cha juu *(an accessible, affordable, relevant and high-quality education system)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo, hata wawekezaji watalazimika kuleta wafanyakazi kutoka nje na sisi hatutaweza kulifikia soko la nje la ajira ambalo sasa lazima twende huko kwa sababu ajira imeshakuwa changamoto. Hapa hatuwezi ku-*absorb* watu wetu wote, lazima tuwajengee elimu ambayo itawafanya waweze kwenda nje kufanya kazi. Bila kulinda mafanikio haya, itakuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu kwenye kulinda mafanikio ni suala zima la utawala bora. Natambua sana juhudi za Serikali, uwekezaji mkubwa katika sekta ya utoaji haki na hata tume mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tume ya Haki Jinai ambayo Mheshimiwa Rais ameiunda, kwa kweli hizi ni jitihada kubwa sana. Tunatakiwa sasa tuzipokee, tutendee kazi na tutumie hii mifumo ambayo Serikali yetu inatutengenezea. Kwa suala hili kwa upande wa Tanzania mimi nasema siyo suala gumu sana kwa sababu tuna pa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote ambayo yanaweza yakasemwa, lakini nataka kusema Katiba yetu ni nzuri, na endapo tutaitumia vizuri, hakuna haki wala *failure* ambayo itatokea kwenye utawala bora. Katiba yetu inatutengenezea mihimili mitatu ambayo kwa mujibu wa Katiba yote ipo huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kizuri kama kuishi kwenye nchi au kufanya biashara mahali ambapo kuna Mahakama ambayo ipo huru, Mahakama ambayo imetengeneza falsafa yake, imetengeneza msimamo wake, yaani ina kitu ambacho tunasema, *a formidable jurisprudence*. Hali ambayo mtu akitenda jambo, mvurugane huko nje, lakini mkifika

Mahakamani ni *break*. Mnajua pale haki lazima itasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifika hapo hata imani kwa wawekezaji inakuwa kubwa kwa sababu, mtu anajua nikienda kuwekeza Tanzania, nikionewa au nikikutana na mhuni, basi iko Mahakama ambayo itanilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika Mhimili wetu wa Bunge tusimame kwenye nafasi yetu kutunga sheria ambazo tuna hakika kwamba zinaweza zikasukuma hii mipango ya maendeleo mbele na Serikali pia, kusimamia eneo lake. Mihimili hii mitatu ni lazima ikae kwenye mazingira ya kuogopana kidogo, kila mmoja ukisimama kwenye nafasi yake, isiwe ni urafiki wa kupitiliza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tufike mahali ambapo mwekezaji akitaka kuja kuwekeza Tanzania, hana haja ya kujiuliza anamfahamu nani? Anamfahamu Waziri au Mbunge gani? Au anamfahamu dalali gani? Aje kwa vile anafahamu mifumo yetu iko imara na ile mifumo iweze kumpa kile kitu ambacho anakitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesema, Katiba yetu ina uwezo wa kutupa hizo haki. Tunachokikosa ni nini? Kinachopungua ni Ukatiba *(Constitutionalism)*. Ule utashi wa watu kupenda kujifunza Katiba, kuitumia na kuikimbilia pale ambapo kunakuwa na tatizo na kuiheshimu. Nikisema kuitumia, nasema kuitumia kama mkuki, yaani kama unafanya jambo lako uende kwa mujibu wa Katiba, na kama kuna mtu anaingilia haki yako, uitumie Katiba kama ngao, *as a sword and as a shield*. Tukifika hapo, wala hakuna tatizo. Tunaweza tukawa na Katiba unayoiita wewe ni nzuri, lakini kama hakuna utashi wa kuitumia, basi itabaki hapo bila kutufaa kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ni kitu kizuri, lakini haiwezi kufanya kazi peke yake, lazima iwe ndani ya mfumo mzima ambao unafanya kazi. Ndiyo maana hata yale mawazo ambayo mara nyingi huwa yanasemwa kwamba tuwe na mpango wa muda mrefu, tuutungie sheria, kweli inapendeza kuusikia, lakini

nina mashaka na uwezekano wa hayo kwa sababu, mpango huu unakwenda kubadilika kwa nyakati zinavyobadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachotakiwa ni kuwa na mfumo mzima ambao unafanya kazi vizuri na siyo kutegemea kitu kimoja tu cha kusema kwamba, unamlazimisha mtu kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* kwa kweli, kwa mtu ambaye anatembeatembea humu nchini na nchi za nje, anaona kabisa kwamba hali yetu inatia moyo sana. Tumetekeleza miradi mikubwa, hali ya nchi ni nzuri na hata ukienda kwenye mitandao ya kijamii sasa hivi utaona kabisa jinsi ambavyo suala zima la ujenzi wa miundombinu Tanzania linasifiwa kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi kama wa *BRT,* kwa kweli una sura nzuri sana. Sasa suala ni kwamba, tutauendeshaje, ili tuweze kupata faida na uweze kuwa endelevu? Siyo mradi wa leo na kesho. Kwa hiyo, hayo ndiyo maeneo ambayo ni ya kutilia mkazo, lakini vinginevyo kwa kweli tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anaiendesha nchi hii vizuri pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta mbalimbali. Kwa kweli, kazi yao ni nzuri na ninaamini kabisa *future* yetu iko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Tadayo. Nilimtaja Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika hoja ambayo imewasilishwa na Serikali. Naamini na ninaendelea kuamini kwamba siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea ndiyo ambayo inaweza kuleta maendeleo makubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kazi tulizofanya katika miradi mikubwa ni kielelezo kwamba, Taifa letu lina uwezo wa kujitegemea na lina uwezo wa kufanya mambo makubwa. Hii inaonesha *prosperity* kubwa katika nchi yetu. Naipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa tuliyoifanya. Watu wengi wamesema na Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema habari ya miradi ya mabwawa, umeme na reli. Yote haya mengi tumeyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu leo nilitaka niishauri Serikali. Pamoja na kwamba tuna ulinzi wa kutosha kwenye mipaka yetu, tuna uwekezaji katika miundombinu mikubwa, lakini kama bado hatujaimarisha usalama ndani ya nchi, hatutaweza kupata wawekezaji ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu wa bajeti, nashauri fedha nyingi zipelekwe kwenye usalama wa ndani ya nchi yetu. Kwa maana ya kuboresha na kuleta mapinduzi makubwa katika Jeshi letu la Polisi. Nchi zilizoendelea siyo lazima Polisi aonekane mtaani, anatakiwa akae kwenye *control room* aangalie mtaa ule ni nini kinafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaweka *camera* kwenye mitaa yetu na kuna watu wanasema, siyo vizuri kugombana na watu kwa sababu ukitembea mtaani hakuna *camera* inayokumulika kwa hiyo, unaweza kufanyiwa jambo lolote. Naishauri Serikali, ili nchi yetu tuwe na usalama na uhakika, ni lazima tuwekeze katika kufunga *camera* katika mitaa yote na hili ni haki ya wananchi wetu na Taifa letu liwe salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha miundombinu mizuri ndani ya nchi yetu, vilevile tuboreshe na maisha ya askari wetu. Tuna Makao Makuu ya Polisi hapa, ukienda mita 200 wanakoishi Polisi, haiakisi maisha yale. Tunashindwaje kuwajengea Polisi wetu, *apartments* kama tulivyofanya katika vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa wanayoifanya na katika *welfare?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha wanayoishi Polisi wetu katika nyumba zile pale *quarters* hayaendani na kazi kubwa

wanayoifanya ya kutulinda sisi wananchi. Inawezekana kuna *stress* kubwa kwa Askari wetu kwa sababu hatujawekeza katika makazi yao. Naiomba sana Serikali iwekeze katika usalama wa ndani ili Taifa letu liwe na uhakika kwanza wa maisha yetu ya ndani. Kwa kufanya hivyo, tutaleta uwekezaji na tutafanya biashara hata usiku wa manane kwa sababu tuna usalama. Naomba jambo hilo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu utekelezaji wa miradi ya Serikali, hususan barabara. Tunapitisha bajeti mwezi wa Saba, tukishapitisha, mwezi wa Nane, wa Tisa, mfumo wa Serikali umefungwa. Mwezi wa 10 tunaanza *procurement,* inachukua miezi miwili. Mwezi wa 11 na 12 mvua zinaanza kunyesha, hatuwezi kufanya kazi. Tunaenda hivyo tena mwezi wa Nne tunaanza mchakato wa kuandaa bajeti, mwezi wa Saba tunarudia hivyo hivyo. Miradi yetu haitekelezeki kwa sababu, tulivyojiwekea namna ya kutekeleza bajeti zetu na msimu wa mvua, barabara zetu haziwezi kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kama tutaweza kuwa na nyakati *special* kwamba, bajeti za miradi yetu ya barabara ipitishwe mwezi wa Kwanza, ili mambo mengine yaje. Michakato ikifika mwezi wa Tano, tunaanza kazi za ujenzi, tunaenda mpaka mwezi wa 12, ambapo mvua zinapoanza, tayari tunakuwa tumeshajenga Barabara. Tukienda kwa namna hii, hatujengi barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, wakandarasi wetu hawalipwi. Hiyo ni *crisis* kubwa katika nchi yetu na tunawaumiza Watanzania wenzetu. Naiomba Serikali, hebu iangalie kwanza namna ya kulipa kabisa madeni ya wakandarasi wetu ili kwamba, tujenge *base* kubwa ya ndani katika kushughulikia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, China wana benki ya wakandarasi *(The Chinese Construction Bank)*. Tuige mfano ule kwa ajili ya kuwainua wakandarasi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, upo utaratibu ambao umeletwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

kwamba, baadhi ya halmashauri wanatakiwa wachange 40% za maendeleo na 20% ya maendeleo. Nataka niseme, kwangu katika Wilaya ya Bahi utaratibu wa 20% kwa 80%, sisi umetuathiri sana. Ina maana tukikusanya shilingi bilioni moja inatakiwa tupate shilingi milioni 200. Shilingi milioni 800 tunaenda kusaidia kuiendesha Serikali, naona hii siyo *fair*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukusanye shilingi bilioni mbili, shilingi milioni 400 ndiyo inaenda kwenye maendeleo. Hii yote tunaitunza Serikali kwa maana ya kuendesha halmashauri. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hii *formula* ya 20% kwa 80% kwetu Bahi inatuathiri. Tunakusanya fedha, lakini fedha nyingi tunatumia kuendesha Serikali. Naomba mliangalie jambo hili, walau hata tuje kwenye 40%, isiwe kazi yetu kuitunza Serikali. Kama nilivyosema, sisi tunakusanya fedha, lakini fedha nyingi tunaitunza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba mwaka huu katika Taifa letu tumezalisha chakula cha kutosha, lakini uzalishaji huu umefanyika katika mikoa mingine. Nimekuwa nasema siku zote, Serikali iangalie na ije na sera mahususi kwa maeneo kame, kama hapa Dodoma, uzalishaji wetu uko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ametoa fedha katika maeneo kwa shughuli ya umwagiliaji, lakini bado haitoshi. Serikali ije iangalie uzalishaji katika maeneo yetu ya Kanda ya Kati ambayo ni maeneo kame na watu wengi wanategemea kilimo. Kufanya hivyo, itapunguza umasikini kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaliwa kuwa ni lango katika nchi kama nane, kwa maana ya bidhaa zinazoingia kuzipeleka katika maeneo mengine. Hatujajiandaa, Tanzania inatakiwa kuwa *logistic hub* ya uhakika na hata uzalishaji wa bidhaa nyingine ambazo zinaagizwa kwa kiasi kikubwa, inatakiwa sisi hapa tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kuhusu Bandari ya Bagamoyo. Mradi ule ni muhimu sana ili tuongeze tija ya kuweza kupokea kwanza, bidhaa kupeleka katika nchi nyingine, na vilevile na tujenge hapa. Tuna *Economic Processing Zone* moja, ile ya kuzalisha nguo na kupeleka nje, nayo haikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali iwekeze katika *logistic hub*. Tujenge Bandari ya Bagamoyo, vilevile tujenge viwanda, kama ambavyo wenzetu wa Ethiopia wamefanya katika uzalishaji wa viatu na sisi tufanye hivyo. Suala hili litatusaidia, kwanza, kuweza kupata fedha na vilevile kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niseme ni tunafanya mambo mengi. Taifa letu limebarikiwa, kwanza tuna lugha moja ambayo wote tunaelewana, Kiswahili, lakini tulipofikia nchi yetu hatuna ubaguzi wa kikabila. Mtu yeyote katika nchi hii ana fursa bila kuangalia kabila analotoka, lakini bado hatujatengeneza mpango kama Taifa, kwamba, *focus* yetu sasa ni ipi na nchi yetu inaendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuwekeze katika *culture* ya Watanzania. *Culture* kubwa ya Watanzania ni katika kufanya kazi na *discipline*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wachina, *one billion people* wameweza kufanikiwa kwa kuwa na mwongozo na *culture,* hasa ya kufanya kazi. Nataka niliseme hili, yapo mambo mengi, sisi tumejiingiza kwenye kamali, *betting* na tumewekeza sana katika *shortcuts* za maisha, lakini tangu zamani tunasema kazi ni utu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iendelee kulisisitiza jambo hili. Kuangalia namna hasa ya kuwezesha vijana katika kujiajiri na vilevile Serikali iongeze mahitaji kuona ni kwa namna gani tatizo la vijana ambao walioko mtaani wataweza kuingizwa kwenye *workforce*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo. Kwa vile muda wetu bado wa mchangiaji mmoja, ninampa Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, kama utakuwa tayari. Karibu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi ya kuweza kuchangia Mwongozo wa Mpango wetu. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima sisi pamoja na ndugu zetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nachukua nafasi hii kuendelea kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya ya kutuongoza sisi Watanzania, pamoja na viongozi wengine wote wanaomsaidia akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimemruka Mheshimiwa Makamu wa Rais, lakini pia, hata Mheshimiwa Rais wetu wa kule Zanzibar; kwa upande wa Bunge, Mheshimiwa Spika pamoja na wote, Naibu na Wenyeviti mnaomsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitakuwa na ya tofauti sana, ni kuweka msisitizo na mkazo katika mambo ambayo naona ni muhimu sana. La kwanza ni mpango huu ufanye tafiti za kutosha kuona ni jinsi gani katika hii Dira ya Taifa inayokuja ya mwaka 2025 kwenda 50 kama itaishia hivyo, kuangalia suala la ardhi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi ni jambo ambalo sasa hivi linaanza kuwa ni tishio. Kutokuwa na mipango mizuri kunaanza kuwa ni tishio kwa Watanzania wenyewe. Nasema kwamba, ardhi itamilikiwa na Watanzania. Ardhi iko chini kwa Watanzania, lakini Mheshimiwa Rais ndiyo anakuwa kama msimamizi mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi sasa hivi ina watu wengi wanaokuja kutoka nje na kuchukua maeneo ya kutosha kwa kisingizio cha uwekezaji, lakini pengine hata siyo uwekezaji kiasi kwamba Watanzania wenyewe wanaiangalia tu hii ardhi kwa sababu walizoea kuishi kwenye koo zao na kuona hapo ndiyo

kwao. Matokeo yake utafika wakati Watanzania watakuwa hawana ardhi na huo ndiyo mtaji mkubwa katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanyike mpango wa kutosha, hili kundi la vijana wengi waliozaliwa na wengine wameshakuwa wakubwa sasa, waweze kusaidiwa namna ya kuweza kupata ardhi kwa utaratibu ambao ni wa kuwawezesha na siyo lazima kila mtu aitafute kwa pesa yake mwenyewe. Kwa sababu, hawa vijana wanamaliza shule au vyuo, lakini unakuta hawana hiyo mitaji ya kupata hata ardhi. Basi ufanyike utaratibu maalum utakaowawezesha hao kupata ardhi za kuendeleza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, sasa hivi idadi kubwa ya Watanzania ni vijana. Hawa vijana wa leo ndiyo tunaowatarajia wawe wazee wa miaka kadhaa mbele. Kwa hiyo, leo tunajivunia kwamba kila mtu anasema mimi kijana, unaona mimi kijana, anajifurahia bado kijana, lakini baada ya muda fulani atakuwa mzee. Kwa hiyo, lazima pia tuwe na mikakati ya kuona hao wazee huko mbele wanafanywa nini? Watatumika vipi? Kwa sababu watakuwa wazee wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia hao vijana pamoja na kujivunia kuwa ni vijana, pia, wanaogopa kuwa na watoto. Kwa hiyo, tutajikuta tumekuwa na Taifa la watu wazee kuliko vijana. Basi kwa misingi hiyo, Taifa letu lazima liangalie pia, tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona suala la miundombinu limepewa kipaumbele katika mpango huu, naungana nalo kabisa. Kwa hali ya kawaida, maeneo yote ambayo ulikuwa ukipita mwanzo labda yalikuwa hayana miundombinu ya barabara, ikija kujengwa miundombinu ya barabara, iwe ya lami au ya changarawe, unakuta hali ya ustawi wa wananchi inabadilika ghafla, yaani kunakuwa na mabadiliko makubwa sana ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu zote zilizojengwa miundombinu ya barabara au madaraja yakajengwa vizuri, wananchi wenyewe wanachukua hatua za kujenga uchumi wao,

siyo kusubiri tu labda kupewa kwenye bajeti. Kwa hiyo, tulifanya vizuri sana katika kuhakikisha kwamba, mikoa inaunganishwa kwa lami, tukaenda kwenye wilaya ziunganishwe kwa lami. Sasa hivi tulikuwa tunaanza kwenda hata katika maeneo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, pamoja na changamoto zinazoweza kujitokeza kwamba labda pesa haitoshi, tulijibana kwa ajili ya kufanya miradi ya kimkakati, lakini sasa tuone kwamba hii miradi inapokuwa haipati fedha za kutosha na makandarasi wanapokuwa hawalipwi, basi tunajirudisha tena nyuma kwenye kasi yetu tuliyokuwa tumejipangia. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ione umuhimu wa kuendeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa sababu, ilikuwa imeshawekwa katika mpango mkuu wa kichama, Ilani ya Uchaguzi, naomba ile miradi yote ambayo ilikuwa bado haijapata nafasi ya kutekelezwa kwa sababu mbalimbali, ikiwemo fedha, basi katika mpango unaokuja ihuishwe iweze kwenda mbele. Siyo tuanze na vitu vingine wakati wananchi walikuwa wameshapewa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kule kwangu Nyasa, kuna barabara kutoka pale Amani - Makolo kwenda mpaka Lituhi na sasa mpaka Ndumbi. Pia, kuna Lituhi – Ndumbi kwenda mpaka *Mbamba Bay* - Chiwindi na Nyoni kwenda mpaka Mitomoni. Hizo barabara zote ziendelee kuhuishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuona kwamba iko haja ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja yale niliyokuwa nayalalamikiwa ambayo yaliondolewa na maji wakati wa mafuriko. Sasa hivi Daraja la Mitomoni na la Mkili linaenda kujengwa na juzi mikataba imesainiwa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna suala la miradi ya maji. Maji ni uhai, lakini maji ni siasa kwa upande wa wanawake. Bila maji tunakuwa tumewatenga wanawake katika maendeleo. Naomba fedha za kutosha zipelekwe kwenye maji ili hawa wanawake waendelee kufurahia kauli mbiu ya mama,

Mheshimiwa Rais wetu, ya mkumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana safari hii mfuko wa maji uongezewe fedha za kutosha ili miradi ya maji iliyoanza, makandarasi walipwe. Pia kama ambavyo wenzangu wamezungumza, hawa makandarasi tunawaingiza kwenye mateso makubwa, mali zao zinawekwa mnada kwa sababu ya kushindwa kulipa madeni waliyochukua kwa ajili ya kujenga hii miradi. Kwa hiyo, naomba sana fedha hizo zipelekwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali yetu, tumejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, sasa umeme angalau umezidi kutoa hali nzuri. Kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo moja, Serikali iendelee kutoa ruzuku kwa Shirika letu la Umeme, *TANESCO*. Pamoja na kwamba, tunazungumza labda shilika hili lina madeni au pengine halizalishi faida, *TANESCO* wanazalisha faida ambayo ni *indirect*. Ni faida ambayo haipimiki kwa fedha moja kwa moja, lakini ni faida kubwa sana ya kuchochea maendeleo ya Watanzania katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukisema Shirika kama *TANESCO* halizalishi faida, siyo kweli. Mimi ninasema nini? Baada ya *TANESCO* kupata umeme wa kutosha kupitia vyanzo vingine, kama hiki ambacho kimejitokeza cha Bwawa la Mwalimu Nyerere, pamoja na vyanzo vingine ambavyo vinategemea kujengwa, Ruhuji na maeneo mengine, siyo lazima sana tupunguze bei ya umeme kwa Watanzania wote. Tuangalie maeneo ambayo tukipunguza hapo, tukaweka bei maalum ya umeme itasaidia kunufaisha watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo wanapata umeme kwa bei kubwa sana. Maeneo kama ya Mkoa wa Manyara, yanapata umeme kwa bei kubwa sana, kwa ajili ya miradi ya maji, kiasi kwamba gharama za uendeshaji au *bill* za maji zinakuwa ni ghali sana kwa sababu ya umeme. Kama ambavyo ipo kwenye umeme wote nchi nzima tunautumia kwa bei maalum, kwa nini na huko kusiwekwe ruzuku ambayo itasaidia kuweka bei ya umeme kwa upande wa mitambo ya maji, ikawa

ya nafuu halafu ikasaidia kutoa maji mengi kwa watu wote kwa bei inayokaribiana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, iko haja Wizara ya Maji pamoja na Ofisi yetu Wizara ya Mipango, kuliangalia jambo hili kwa kina. Haiwezekani mwingine anunue maji, *unit* kwa shilingi 5,000/= mwingine ananunua *unit* ya maji kwa shilingi 50/=, hapana. Kwa hiyo, naomba sana iangaliwe *tariff* maalum, kwa ajili ya kuzalisha maji ya kunywa ambayo kila mtu anayahitaji. Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba mikakati iliyopo ya kuhakikisha maji yanapatikana, inaendelea kwa kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kusema kwamba, pamoja na hayo yote niliyochangia, Mradi wa Barabara kutoka Songea…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka pale…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake umeisha, anamalizia sentensi ya mwisho.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Lukumbulu kwenda huko, naomba sana, barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wetu wa Tanzania kwa ujumla, basi iweze kupata fedha na ifanyiwe kazi mapema kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu na wote wanaomsaidia. Namshukuru sana Mheshimiwa Bashe, lile duka la mbolea pale Nyasa tayari limeshaanza. Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya. Huyu ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi hiki cha asubuhi.

Nitawataja ambao wataanza kuchangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujakamilisha shughuli zetu, tuna matangazo kidogo hapa. Tuna wageni ambao wameingia muda huu. Kuna wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge Wakatoliki. Wageni hao ni Askofu Msaidizi wa Chuo cha Kanisa, ameambatana na Flateri kutoka Jimbo Kuu la Dodoma; Askofu Wilbroad Kibozi, ambaye ni Askofu Msaidizi, Jimbo Kuu la Dodoma. Pia, tuna Flateri Suleimani Sango, karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu pia, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wageni 10 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, hao ni wapiga kura wake kutoka Halmashauri ya Mji wa Geita, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, ambao ni wapiga kura wake pia, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, ambao ni wamiliki na Wanafunzi wa *Day Care Centre* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 125 na walimu 10 wa Shule ya

Sekondari Ihumwa kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza shughuli zetu za asubuhi hii mpaka mchana huu. Nawatakia mchana mwema.

Nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tunaanza na Mheshimiwa Flatei Massay,

atafuatiw ana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, na Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu sana kwa kunijalia kusimama hapa mchana huu wa leo. Lengo langu kwa kweli ni kuchangia Mpango huu wa Bajeti wa mwaka 2025 kwenda 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo ameifanya kwenye maeneo yetu hasa katika mpango ule uliyopita. Nina maana gani kusema hivi? Mipango hata Mungu kwenye Biblia alianza kuipanga. Wakati Mungu anaunda dunia kwenye Biblia alisema, na tufanye dunia na pia akasema na tufanye mtu. Haya yote ilikuwa ni mipango ya Mungu. Leo sisi tumepata bahati ya kuingia ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kusaidia nchi hii kupanga mipango ya 2025 kwenda 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka niongee maeneo mawili makubwa. Eneo la kwanza ni kuisaidia Serikali kutafuta fedha ili mipango hii iweze kukamilika na Serikali ikapata fedha ya kupeka kwenye maendeleo ya mipango yenyewe. Nimesoma Mpango wenyewe wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Prof. Kitila, nawapongeza kwa kweli, wameuwasilisha vizuri sana, ukizingatia leo hii tunaingia mwaka huu wa 2024 kwenda 2025 tunayo maeneo ambayo ukiangalia bajeti yetu yote ya mwaka huu ambao tunaenda 2025 ni wazi kwamba kuna nakisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri ndugu zangu wapendwa, yapo maeneo ambapo Serikali tungeweza kupata fedha ya kufanya miradi, kwa mfano, sasa hivi kuna eneo la misitu yetu ambayo inawezekana kuweka mikataba ya kuvuna hewa ya ukaa maarufu kama *carbon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jafo alikuja Jimboni kwangu au Mkoani Manyara akatugawia shilingi bilioni nne ya hewa ya ukaa ya mwaka uliyopita. Hebu angalia kama sisi tunaweza kupewa shilingi bilioni nne katika mauzo haya

ya hewa ya ukaa, je, Serikali ina misitu kiasi gani ambayo ingeweza kuwekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ndugu zetu wanachohitaji ni kitu kimoja tu, kukubali misitu ihifadhiwe ili nao wapate ile *volume* ya hewa ya ukaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu angalieni, ongeeni wenyewe ndani kwa ndani Serikali muweze kuwasiliana ili muone. Tanzania tuna misitu mingi inakaa bure, kwa sisi kwa vijiji vyetu kule tumefanya hivyo, vijiji vinalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu ni Serikali waone namna hii, kwamba eneo hili limeshakaa bure kwa muda mwingi, iingie mikataba kwa sababu mikataba ile kwanza wao hawaji na kwa mujibu wa sheria na taratibu zao maana yake ni kwamba unapoingia ile mikataba unaitunza misitu yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *TANAPA, TFS* watoe tu misitu ambayo sawa inazalisha, tunapata asali, lakini ukiweka katika eneo hili tutapata fedha katika nakisi ya bajeti na hii itatusaidia sana kwenye Mpango ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema haya? Nasema hivi kwa sababu tunaona Mpango wa mwaka mmoja, Mpango wa mwaka uliopita ambao tunakwendanao, sasa hivi ukiangalia nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameonesha pia kuna utekelezaji wa Mpango huo wa mwaka huu unaoelekea, lakini ukiangalia mipango hii yenyewe hatujaikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu sasa akitaka kukamilisha naomba Mipango hii inapotekelezwa iangaliwe, pia eneo la kupatikana kwa fedha, tupange Mipango lakini tupange mipango pia inayotekelezeka kupata fedha. Kwa nini nasema hivi? Kwenye nchi yoyote inayoendelea, ukiangalia sekta ya miundombinu ni sekta ambayo inaisaidia mipango yote ya nchi ili nchi ikue kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mungu ametubariki tumeingia humu ndani. Nataka niwakumbushe tena ndugu zangu wawili hawa, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa

Waziri wa Fedha, hongera sana. Pia kamteua pia ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kuwa Waziri katika Wizara hii ya Mipango. Hawa wote wanatoka Singida, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida ni karibu karibu kabisa, ni jirani na Mbulu nao ni watani zangu. Wewe ni nani? Si unajifahamu mwenyewe, nikisema *ulaileani,* uongo! *Hamcha wanghu; Habari ya diu; umufangana;* tunaelewana lugha za nyumbani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba kuna barabara ya kimkakati ambapo Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu wa kwanza alikuja hapo, anaitwa Herman Elias, ukiangalia Taarifa za Bunge mwaka 1965, alisema kuhusu barabara ile, lakini haikujengwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile inatoka kule Usukamani na Mheshimiwa Nyongo Mungu amembariki amewekwa hapo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Mungu aendelee kumbariki kawachagua kawaona. Wewe unayeitwa Mheshimiwa Nyongo barabara inatoka inapita Jimboni kwako ndiyo inakuja kwangu, inapita kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu inakuja kwangu, barabara hii inaitwa Karatu – Mbulu - Haydom – *Sibiti River* – Lalago. Hii barabara inapita Majimbo tisa. Barabara hii ikiwekwa kiuchumi, itainua maeneo yale. Kwa hiyo, kwenye mpango huu unaoelekea iwekewe fedha ili ijengwe yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Rais ameiona imetengewa fedha. Sasa umeona imetengewa fedha lakini fedha yenyewe haipelekwi. Sasa ombi langu, ninyi mnaopanga mipango hii pangeni mipango kweli, lakini angalieni mahali pa kuweka fedha ili zikatumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia leo hii tuna madeni. Madeni haya ni hatari kwa nchi yetu, kwa sababu gani? Leo mmesaini mkandarasi wa Labai kwenda Haydom lakini mmesaini pia mkandarasi pia wa Masqaroda au Garbabi kwenda Mbulu, ameingia kazini, mmemlipa kweli shilingi bilioni tatu pale, ameanza kazi, leo kasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni Daktari wa Uchumi, sasa ukimwacha yule mtu akakaa pale bila kulipa madeni haya ya wakandarasi, maana yake ni kwamba anaongeza *profit* ambapo kiuchumi ilitakiwa ufanye nini? Nimesoma kozi ya uchumi ndogo, na kiuchumi ulitakiwa umkate akichelewesha mradi *liquidated damage,* lakini hakuna. Leo anakukata wewe kitu kinaitwa *profit*, maana yake tunakwenda kulipa madeni. Tungeweza kulipa na mipango ikapangika na hela zikapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Mipango tunayopanga na tuone wapi fedha inapatikana na hii itatusaidia sana kuinua nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, ukiangalia maeneo mengi ni wasifu, kwa kweli ukiangalia kwenye kilimo, kimepanda nawapongeza sana; kuna maeneo mengine unaweza ukapiga kelele sana lakini hili la kilimo linagusa maeneo mengi sana. Mpango huu unaendelea kusaidia maeneo ya kilimo. Ukiangalia sasa hivi kilimo kwenye hotuba hapa imepanda kwa 3.7%, ni wazi tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia imewekwa vizuri sana kwenye eneo hili la umeme, yameongezwa kabisa maeneo mengi, hali hii itaenda kusaidia sana nchi yetu kukua. Pia kwa kweli napongeza eneo lingine la *SGR*. Tunampongeza Mheshimiwa Rais hapa, kwa kweli jambo hili siyo jambo dogo. Yapo mambo mengine, sisi tunaitwa Wabunge wa kupongeza. Hapana, lazima tuseme. Leo hii mtu anatoka hapa Dodoma anawahi Dar es Salaam, anatoka anarudi hapa, hili lilikuwa haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia bwawa linakwenda kumalizika. Hii ni miradi mikubwa, lakini hii miradi mikubwa usipoi-*connect* na barabara ndogo ndogo za kuingia kwenye hii *SGR* inakuwa hakuna maana yoyote. Mipango yetu hii iangaliwe. Hizi barabara ndogo Kibarashi, wapi unakata paingie kwenye *SGR?* Hii ya huku Haydom inakutana kule inaingia kwenye *SGR,* kwa hiyo, uchumi utakua, unazunguka tunapoelekea mbele. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba barabara tunazoenda kuzijenga na mipango hii ikikutana, barabara hizo tukaziweka hapa, huu uchumi ukawa unazunguka wenyewe, na kwenda mpaka nje ya nchi, tutakuwa tunatoa mazao kutoka mashambani tunapeleka viwandani; tukipeleka viwanda vyetu, tunapeleka pia nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta hii reli inapata kazi, lakini wakati huo barabara zetu kule zinapata kazi. Duniani kote angalia miundombinu ya barabara imekuwa ikiwekwa kwa umuhimu wa pekee, lakini hiyo miundombinu ikiwekwa umuhimu wa pekee ndiyo inayofanya uchumi wa nchi yoyote uendelee, hilo ni wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ukiangalia kwenye bajeti ambayo tunaiona, yapo mabwawa yamejengwa na ni makubwa, mabwawa yale pia lazima yapelekewe miundombinu ya barabara ili wanapotoa mazao kutoka maeneo yale yaweze kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ya madini, ukiangalia Liganga na Mchuchuma na maeneo haya ninayoyasema, ninamaanisha ni pamoja na haya tukiweza kupeleka kule lakini pia tukatafuta fedha; maana yake ninachojua kazi yetu kubwa hapa ni kweli kupanga bajeti, lakini tuweke nguvu kubwa pia katika kutafuta fedha. Eneo nililosema la kwanza ni hili linaloitwa hewa ya ukaa, ni fedha ya bure imekaa nje nje, misitu tunayo Mungu ametubariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kama ningekuwa ninapanga ningesema hapa ndiyo Edeni. Tanzania ni Edeni, ina misitu mingi. Kule kwetu imejaa, nimetoa mfano tu mwaka 2023 tumepata shilingi bilioni nne.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni nne sisi tunataka kwa mfano kule barabara, kile kitu kinachoitwa *advance payment* ni shilingi bilioni tatu, hebu wewe fikiria kama tungeweka ile misitu yote tukayapa yale mashirika

yanayovuna *carbon,* maana yake ni kwamba tungekuwa na fedha. Sasa nimewaambia kwa eneo hili moja tu, na muda ungekuwa unatosha ningesema maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunivumilia, nimesikia kengele. Ahsante sana, Mungu akubariki, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, ahsante sana. nilimtaja Mheshimiwa Iddi Kassim, Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa leo kuweza kuchangia mpango huu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nami leo kushiriki kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Mpango huu wa Maendeleo 2021/2024 na 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwenye Majimbo yetu, amefanya kazi kubwa sana. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili kwa maana ya Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango na Naibu wake Mheshimiwa Nyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imenipa taabu sana leo. Hapa nilipokuwa nimekaa nilikuwa naangalia anayefuata baada ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni nani? Nikaja kugundua ni Maalim Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niseme kwamba nafahamu ni kwa nini amevaa hivyo, ni kwa sababu anaamua leo kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Wakati tunajadili Mpango hapa kuna timu inaendelea huko kucheza, anaomba dua nyingi sana timu ile iweze kushinda, lakini nasema *In Shaa Allah* kwa sababu amekaa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba hapo, basi nafikiri hapo mambo yataenda vizuri. Namwombea sana timu iweze kushinda, lakini tujadili Mpango ambao ni mzuri sana ambao utatuletea maendeleo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunafahamu wote tulikuwa na changamoto kubwa sana ya suala zima la dola kwenye nchi yetu, lakini leo hii tunavyozungumza wananchi wanakupongeza sana, wanampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, dola zimeshuka kwa wingi, zipo mtaani na kwenye mabenki. Hapo mwanzo ulikuwa ukienda benki unapewa dola 500 tu kwa siku, lakini leo hii mpaka unaulizwa, vipi unataka ngapi tukupatie? Maana yake dola sasa ipo kwa wingi. Nakupongeza sana na endelea kushika hapo hapo uhakikishe ya kwamba dola inaendelea kushuka kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza sana kwa Mpango huu mzuri. Ukiangalia kwenye Majimbo yetu hasa kwenye Jimbo la Msalala, niseme tu kwamba Mpango huu wa Miaka Mitano 2021/2024 na 2025/2026, sambamba na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nafikiri Mpango huu umetekelezwa kwa 95% na hizi tano zimebaki ni kidogo tu, tunamalizia kwenda kwenye Uchaguzi wa 2024/2025. Ni matumaini yangu kabisa kwamba tutaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sijampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa. Katika Mpango wa Miundombinu; ujenzi wa miundombinu Mheshimiwa Bashungwa ametufanyia jambo kubwa sana kwenye Jimbo la Msalala. Kulikuwa kuna barabara moja kichefuchefu ilikuwa inasumbua mno, barabara inayotoka Kata ya Bulyanhulu kwenda pale Kahama. Kweli Mheshimiwa Waziri tulibanana sana lakini aliniambia tulia mjomba, mambo yanaenda vizuri. Amepambana mpaka kuhakikisha kwamba mkataba unasainiwa na kwa sasa barabara ile inashambuliwa, wale Wachina wanafanya kazi usiku na mchana mambo yanaenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika Mpango huu unaondelea, kuna barabara mbili. Barabara hizi tunaona limejengwa daraja, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza mradi huu wa ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi. Sasa baada ya kukamilika daraja hili na baada ya kukamilika barabara inayotoka Kahama - Bulyanhulu,

hapa katikati kuna kipande kidogo sana ambacho kinatoka kwenye Daraja la Busisi kuja mpaka Nyangw'ale linaunganisha mpaka Bulyanhulu kukamata lami ambayo inajengwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye Mpango huu ambao tunaendanao 2025/2026 tuone namna ya kuzingatia barabara hii ili kipande haki kidogo kilichobaki tuweze kukimalizia. Kumalizika kwa barabara hii ndogo hapa katikati itaenda kuinua uchumi mkubwa sana, wote mnafahamu. Leo hii baada ya kujengwa kipande hicho, itarahisisha sana hata mtu anayeenda Tabora, hata mtu anayeenda Dar es Salaam hawezi tena kupita Shinyanga ambayo ni njia ndefu sana, hii inakuwa ni njia ambayo ni *shortcut* kuja mpaka Kahama ambayo itanyanyua uchumi kwenye baadhi ya kata ambazo zinapitiwa na barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwenye Mpango huu ambao tunaendanao ni vyema tukazingatia barabara hii. Mmetuambia tayari fedha za upembuzi yakinifu zimetengwa, sasa tuone wakandarasi wanaenda *site* ili waweze kukamilisha kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na kwenye Mpango huu, basi tuingize fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Kuna barabara ambayo ipo ambayo imeahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, barabara inayotoka Misungwi inakuja mpaka Mango – Solwa - Maktolio inakuja Burige mpaka Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa Waziri wa Ujenzi alitupatia baadhi ya fedha kujenga baadhi ya kilomita. Kata ya Burige pale tumejenga kilomita moja imekamilika, tukaruka tukaenda pale Ngaya tumejenga kilomita moja, japo na yenyewe bado haijakamilika, naomba asukume sasa pale Ngaya na penyewe kwa sababu mkandarasi ameondoka kwa muda mrefu na mvua zinaenda kunyesha, aweze kurudi pale akamilishe barabara ile, lakini atimize ile ahadi yake kwa kazi nzuri anayoifanya katika kipande kutoka sasa Burige pale akaunganishe mpaka Ngaya ili tuweze ku-*connect* kutoka pale Burige mpaka Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile ni eneo ambalo lina uchumi mkubwa sana wa kilimo cha mpunga, na niseme tu kwamba mpunga wote mnaouona Kahama na mchele ambao unakuja kwa wingi Dodoma ni mchele unaotoka Jimbo la Msalala na Jimbo la Dada yangu Mheshimiwa Bahati Mbeya huko. Kwa hiyo, Msalala tunalima mpunga kwa wingi sana, hivyo tunahitaji barabara ili ziweze kusaidia, kwamba baada ya kukamilika *SGR* basi tunatumia fursa ile kusafirisha mazao yetu kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya afya, kazi kubwa sana imefanyika. Tumepatiwa vituo vitano vya afya, vimekamika, leo nimeona hapa ndugu yangu Mheshimiwa Festo ametuita kukagua kituo kingine cha afya, naamini kabisa kitaenda kujengwa kituo kile cha afya, lakini tuna chuo chetu tumeanzisha kama Halmashauri na tumekikabidhi kwenye Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa chuo hiki tumetumia kwa mapato ya ndani na *CSR* ya mgodi kiasi cha shilingi milioni 600 na chuo hiki kimekamilika. Kwa sasa tunapozungumzia habari ya upungufu wa watumishi, sisi tuliona fursa hiyo kwamba tuwekeze na tuishawishi sasa Wizara ije tuikabidhi chuo kile ili kiweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye Mpango huu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tupatiwe sasa watumishi ili chuo hiki kiweze kufunguliwa na tuweze kupata watumishi wengi ili kuwasambaza kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga zahanati zaidi ya 34 kwa mpigo, zimekamika, Mama Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amezikamilisha, tunavyo vituo vya afya 10 vimekamilika, tunayo hospitali ya Wilaya ya kisasa imekamika lakini changamoto sasa tunahitaji zahanati hizi ziweze kutoa huduma iliyokuwa bora ili tupeleke watumishi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mama Samia hajaishia hapo, kuna suala zima la ajira, na hili ndugu yangu

Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo naomba nilizungumzie. Kwa sasa tuna changamoto sana, hasa mimi nimesimama hapa kama Mbunge kijana kutetea vijana wenzangu. Vijana tuna changamoto sana ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha zaidi ya shilingi bilioni mbili tumejenga Chuo cha *VETA*, na chuo hicho kwa sasa kiko kwenye hatua ya ukamilishwaji. Namshukuru sana Waziri wa Elimu na Naibu wake kwa kutupatia fedha kujenga chuo cha wilaya kwenye Jimbo la Msalala na sasa kinakwenda kwenye hatua nzuri. Maana yake, kukamilika kwa kile chuo itasaidia vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia habari ya diplomasia ya uchumi, tunaangalia tu kuweka mazingira bora ya kukaribisha wawekezaji kwenye nchi yetu. Nataka nitoe changamoto hii, na niombe sana Waziri wa Kazi, kaka yangu Mheshimiwa Ridhiwani, kwenye Mpango huu unaokuja tunataka tuone kuna mkakati gani wa kusaidia vijana kupata ajira kwenye nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tumeona imetolewa takwimu kwamba fedha ambazo zinarudishwa na *diaspora* kuja kuwekezwa nchini, ukilinganisha kwenye maeneo yetu unaona kabisa Tanzania bado tuko chini. Kenya wanaongoza, Uganda wanaongoza na maeneo mengine. Kwa nini? Ni kwa sababu kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba Wizara ya Kazi inatengeneza ajira nje ya nchi na kuchukua vijana wetu waende wafanye kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda nchi mbalimbali, kama Qatar na maeneo mengine unaona kabisa kwamba Wakenya na Waganda wanasafiri kwenda kwenye nchi hizo kuchukua ajira. Maana yake ni kwamba Serikali inawasaidia wao kupata *opportunities* kwenda kule, na wakishakwenda kule maana yake ni nini? Wanatengeneza fedha na baadaye zile fedha zinarudi huku nyumbani kuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka tuone kwenye Mpango huu sisi vijana mnatuweka kwenye kundi gani? Nashauri tuone kwenye huu Mpango mnazingatia habari ya kutengeneza soko la ajira la nje kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwezo, vyuo vipo, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan amejenga kuhakikisha kwamba tunapatiwa uwezo wa kutosha ili vijana wetu waende wakapate ajira kule. Tukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza sana tatizo la ajira kwa vijana wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye suala la madini. Nimeona, na nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Antony Mavunde, anafanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya madini. Leo hii nimeona sekta ya madini inachangia 9.0% kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba ni kazi nzuri sana anayoifanya, lakini naomba, kwa sababu amekuja na mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba anapima maeneo na anawagawia wachimbaji wadogo wadogo maeneo hayo, vivyo hivyo kwenye Mpango unaokuja nataka tuone kwamba fedha inatengwa kwa ajili ya kukiwezesha Kitengo cha *GST* kununua vifaa vya kisasa, inunuliwe *helicopter* kwa ajili ya kufanya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya hivyo, ni kwamba tutakuwa tumewasaidia wachimbaji kwa kiwango kikubwa sana, kwa sababu kwa leo, ni kwamba wachimbaji hawa wanaingia hasara kubwa sana. Sawa wanapatiwa leseni, lakini hawajui nini kipo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwendo ule ule wa *5G* wa Mheshimiwa Waziri Mavunde, nawaombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango tufikirie namna ya kumwezesha Mheshimiwa Mavunde kwenye Wizara ya *GST,* waweze kununuliwa vifaa vya kisasa ili waende wakafanye utafiti mzuri na wananchi hawa wachimbaji wadogo wadogo wanapopatiwa zile leseni ziende zikawaletee manufaa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba kwenye Mpango huu, kama ilivyo kwenye maeneo mengi 10% kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kwenye maeneo mengine, sasa kwenye hii Wizara ya Madini, Mheshimiwa Waziri Mavunde tuone kwenye mkakati na Mpango huu unaokuja huko, tuone ni namna gani tunaweza kuingia *partnership* na kampuni za nje au kampuni zozote kuwawezesha na kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo vifaa vya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii utaona wachimbaji wanatumia nguvu kubwa sana kwenye kufanya tafiti, wanafanya tafiti wao wenyewe na wanachimba wao wenyewe, lakini vifaa wanavyotumia kwenye kuchimba ni vifaa duni. Sasa kwa sayansi na teknolojia ya sasa ni muhimu tufikirie namna ya kutafuta kampuni ya kuingia *partnership* na Serikali au Wizara iwe ndiyo dhamana ya kumdhamini mchimbaji mdogo mdogo aweze kukopeshwa vifaa ili aweze kufanya kazi yake vizuri kwenye maeneo hayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mawazo yangu kwa siku ya leo. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kusimama hapa nami kutoa mawazo yangu juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha

kwamba tumeweza kufanikisha katika Mpango wa Maendeleo uliopita kuwezesha kufanikisha reli ya *SGR* kiwango cha kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hili alilolitenda. Huu mradi umekwenda kuvumbua Uchumi. Mradi huu umekwenda kutusaidia sana katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, watu wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma, kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam. Pale *station* kuna vijana wa Taxi, bajaji na bodaboda, ambapo wengi wamepata ajira pale ya kusafirisha wananchi wanaoshuka kwenye treni zile kuelekea maeneo mbalimbali. Hilo siyo dogo, ni fursa kubwa kwa mkoa wetu. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu amjalie Mheshimiwa Rais wetu na ampe afya njema ili aendelee kupambania nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango pamoja na Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hizi zote mbili kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutuandalia mipango hii ya maendeleo na mapendekezo haya ambayo yanakwenda kuiinua nchi yetu. Ni jambo kubwa wanalifanya na kazi kubwa wanayoifanya. Tunawaona ni jinsi gani wana-*struggle* kutafuta fedha kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Wanafanya kazi nzuri, waendelee hivyo, wapambanie nchi yetu na Mungu ataendelea kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wa 2024/2025 nitaangalia kwenye kifungu cha 12, 13 na 15. Nikianza kwenye kifungu cha 13 ambacho katika vipaumbele vyake vilihakikisha vinaimarika kwa shughuli za kiuchumi, namshukuru Mwenyezi Mungu na ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha shughuli za kiuchumi ni pamoja na kuandaa miundombinu katika nchi yetu. Miundombinu ndiyo ambayo inakwenda kufungua uchumi wa nchi yetu. Tumemshuhudia Mheshimiwa Waziri wa Fedha tukisaini mkataba wa ujenzi wa Daraja la Jangwani. Hilo siyo jambo dogo, ni jambo kubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dar es Salaam wakitoka kazini wakifika pale *Fire*, mafuriko makubwa yakitokea pale kunakuwa hakuna njia na mji unakuwa haupitiki na shughuli zote za kiuchumi katika Mkoa wa Dar es Salaam zinasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekwenda kusaini mkataba wa ujenzi wa daraja ambalo litakuwa la kipekee na litakuwa refu na ambalo sasa linakwenda kufungua uchumi wa Dar es Salaam. Dar es Salaam ndiyo uchumi, Dar es Salaam ndiyo kila kitu. Kodi zote za nchi tunazipata kwa wingi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekityi, kwa hiyo, kile kilichofanyika na Serikali kwenda kulishika daraja la Jangwani, pia kwenye Mradi wa *DMDP* umeingia katika maeneo mbalimbali, madaraja madogo madogo, na pia kwenye miradi ya barabara za mitaani. Naipongeza sana Serikali yetu, inafanya jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona kwenye mapendekezo yaliyopita walizingatia mabadiliko ya tabianchi, na mapendekezo haya ya Mpango huu wa 2025/2026 wameweka kipengele cha kupendekeza kuangalia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo huwa linatuvurugia bajeti yetu ni mabadiliko ya tabianchi. Pale mvua zisizotabirika zinaponyesha, nchi nzima barabara zote zinaharibika, mito yote inafurika, madaraja madogo madogo yanavunjika na hivyo tunakuwa hatuna jinsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali katika kuangalia mapendekezo haya, haya mabadiliko ya tabianchi yasikae kama andiko tu, hapana, itengewe bajeti ambayo itakuwa inatusaidia badala ya kufanya *reallocation,* itatusaidia katika kipindi kile ambacho kunatokea mafuriko na mambo mengine ambayo yataathiri nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni agenda ya kidunia, hivyo basi ni lazima niwapongeze kwa kuingiza kwenye bajeti yetu au katika mapendekezo ya bajeti yetu. Sasa pamoja na kuiweka huko, basi tuiweke ikiwa na bajeti

pia, kwamba inapotokea kuna tatizo lolote la mvua, mafuriko na vitu vingine tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Mpango uliopita tumeona jambo lingine kubwa lililofanyika la kuanza kwa uzalishaji wa umeme wa maji megawati 705 katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Hili ni jambo kubwa. Kwa kweli tulikuwa tunahangaika na umeme, kipindi kama hiki cha kiangazi kikali ambacho maji hayapo, umeme ilikuwa ni mtihani, lakini sasa hivi umeme unapatikana katika maeneo mengi, lakini bado ziko changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo, kwa mfano maeneo ya Kigamboni, baada ya jana kuuliza swali hapa nilipata *message* nyingi mpaka na mimi mwenyewe nikachanganyikiwa. Ninaambiwa wewe unasema tu kupika, Kigamboni hata *TV* tu haiwaki. Ukiwasha *TV,* saa 12 jioni haiwaki, inabaki cheche tu hivi kutokana na umeme kuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, pamoja na mambo yote, hizi Megawatts 705 za umeme zimekuja, lakini bado tuangalie changamoto za wananchi, kwamba ni tatizo gani kubwa liliko kule ambalo haliwezi kutatulika kwa haraka? Kigamboni imejengeka, Kigamboni ya jana siyo ya leo, wananchi wamekuwa wengi, majengo yamekuwa mengi, watu wanaishi na shughuli za kiuchumi zimepanuka, viwanda vingi vinajengwa maeneo ya *Kisarawe Two* Kigamboni. Kwa hiyo, umeme unagawanyika, ule mdogo hawa wakianza kufanya kazi, hawa hawawezi kupata umeme. Tatizo lile ni kubwa. Naomba sana Mpango huo unaokuja uangalie ni jinsi ya kulitatua kabisa tatizo la umeme katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uboreshaji wa huduma za afya, Mpango uliyopita uliangalia. Naipongeze Serikali yetu, imefanya mambo makubwa sana katika sekta ya afya, kwenye hospitali yetu ya Mloganzila, siku za nyuma watu walikuwa wanaogopa hata kufika, lakini leo hii Hospitali ya Mloganzila watu wanakwambia, wewe kama una shida ya moyo, nenda Mloganzila. Hii ni kutokana na kuboreka kwa huduma ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Hospitali ya Muhimbili imeboresha huduma, huduma zake ni nzuri sana. Vilevile hospitali zetu za Wilaya za Temeke, Mwanamyamala na Amana zote ni hospitali ambazo sasa hivi zinatoa huduma hadi ya kusafisha figo. Jambo hili siyo dogo. Huduma hizi zote ni juhudi za Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake na Chama chake cha Mapinduzi kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, kuna ujenzi wa vituo vya afya vimejengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na vimejengwa kweli kweli, vina huduma za *x-ray,* huduma za meno, ukiingia pale mpaka utashangaa, kwamba hii ni hospitali au kituo cha afya cha Serikali. Au zamani ndiyo tulikuwa tunajua ni cha *private?* Ukweli ni cha Serikali ya Tanzania. Kwa hiyo, wananchi wanapata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto iliyopo ni watumishi. Bado idadi ya watumishi katika vituo vya afya vingi vya Mkoa wa Dar es Salaam haijaridhisha. Baada ya dondoo hizo za mpango uliopita, kwenye mpango huu wa 2025/2026 mimi nitaangalia kwenye vipaumbele. Kwenye vipaumbele wamezungumzia kuhusu uendelezaji wa miundombinu. Miundombinu iendelezwe kwa sababu bado kuna changamoto ya miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ukienda Bunju nyakati za jioni hapapitiki. Maeneo ya Tegeta, Bunju unakwenda mpaka Kunduchi, unakwenda hadi Mwenge magari yanakuwa na msongamano sana. Kutokana na mabasi yanayotoka Moshi na Arusha pamoja na magari madogo madogo kunakuwa na msongamano mkubwa sana. Tunaomba Serikali wakaangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wilaya ya Kigamboni bado kuna shida ya miundombinu ya barabara. Ile Barabara ya Kibada – *Kisarawe Two* hadi Tumbi Songani mpaka sasa hivi inakwenda kwa kilomita moja moja, hatujui mpaka lini tutafika Tumbi Songani, hiyo ni shida, naiomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Barabara ya Mbagala utatoka ulikotoka na nguvu zako unataka kwenda Lindi sijui Mkoa

wa Pwani ukifika Mbagala Rangi Tatu unaambiwa *stop* hakuna kupita kwa sababu msongamano ni mkubwa mno, magari hayaendi. Utakuta unaenda msongamano mpaka Kokoto na wakati mwinginie mpaka Kongowe. Naomba Serikali, barabara hii ni ya muda mrefu, tangu mimi ninaingia Bungeni inaingia kwenye bajeti inatoka, inaingia inatolewa, hatuelewi. Sasa naiomba Serikali waiangalie hii barabara kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukitoka Dar es Salaam kwa barabara unakuja Dodoma au Morogoro unakwenda kuishia Kibaha. Pale Kibaha kuna shida gani? Serikali waangalie tunataka kuinua uchumi na kufungua nchi; wengine watakwenda kwa *SGR* wengine wanarudi na barabara, lakini unapofika pale Kibaha Mkoa wa Pwani ndiyo unaishia, unaomba Mungu leo hapa Kibaha nitatoka salama au nitalala? Kwa sababu kunakuwa na msongamano usioeleweka. Serikali iangalie mbinu katika mradi ujao ya kutatua ile kero ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye masuala ya maji, sisi wa Dar es Salaam tukiulizwa kipaumbele chenu cha kwanza katika mpango, miundombinu, cha pili afya, na cha tatu maji. Tunaomba Bwawa la Kidunda litengewe bajeti ya kutosha kwa sababu bwawa lile likishakamilika litatuletea maji Mkoa wa Dar es Salaam kwa saa zote na kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafika sehemu, Mto Ruvu unazidiwa, maji yanakauka na hivyo kunakuwa hakuna sehemu ya kupata maji, hapo lazima mgao unaingia. Pia, vile visima vya Mpera vipo na vinaendelea kutoa maji, lakini bado kuna changamoto hasa kwa watu wanaokaa maeneo ya Mto Ruvu, bado kunakuwa na changamoto ya maji. Bwawa lile likamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu sijaona maoteo. Kwenye huu Mpango tuweke kabisa kwamba Bwawa la Kidunda liende likakamilike. Bwawa lile litakwenda kusaidia kufungua shughuli za kiuchumi kwa Mkoa wa Morogoro na pia kwa Mkoa wa Dar es Salaam tutapata maji, maji yatatumika majumbani na viwandani. Siyo jambo kubwa tunaona mkoa wetu unaendelea kuwa mkoa wa viwanda na mkoa wa kiuchumi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaipongeza sana Serikali yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariamu Kisangi, nilimtaja Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba univumilie kidogo kwa sababu nimejenga tabia ya kununukuu maandiko ambayo wenzetu wameyaandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuishukuru Serikali, hasa kuwashukuru wale wataalam wetu wawili wakubwa kwa sababu wamefanya kazi kubwa na wameifanya nchi yetu inaendelea kuwa na heshima kubwa sana duniani na kuaminika kwa sababu ya mipango yake ya uchumi na usimamizi wa mapato ya Taifa. Naomba niwapongeze na niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia mambo kama manne hivi. Jambo la kwanza naomba ninukuu kwenye ukurasa wa tano ambapo yapo mambo nitayanukuu siyo kwa sababu hayaeleweki, lakini kuna mambo napenda tufahamiane vizuri, hasa kwenye ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiusoma ushauri wa Kamati unaweza ukaona kama ni ushauri wa kawaida hivi, lakini ni ushauri mkubwa na mzito ambao kwa kweli kama Serikali itafuata huu ushauri, basi kazi hii itakuwa ni nyepesi kwa Serikali, na italifanya Taifa hili likue kwa sababu kila kitu kimewekwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika ukurasa wa tano, pale kwenye yale matarajio ya ukuaji wa uchumi kuna ushauri umetolewa. Nitanukuu baadhi. Kwa mfano, namba mbili wanasema, "kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa bandari zetu ili kupunguza gharama zinazotokana na meli kukaa bandarini kwa

muda mrefu, jambo ambalo linasababisha kuongezeka kwa *demurrage charge*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limeandikwa kwa wepesi sana, lakini pamoja na kwamba jitihada zinaendelea, bado hatujafikia kiwango cha meli kuweza kuingia siku moja na siku ya pili ikatoka kama ambavyo tunaamini hivyo sivyo. Bado mizigo au meli zinachelewa na hivyo kusababisha mlaji kuendelea kupata gharama kubwa kwa sababu meli hizi ni lazima zilipe kila muda unapokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu sasa, pamoja na kwamba hili limewekwa namba mbili, lakini linatakiwa kuwa namba moja kwa sababu sisi bado tunategemea zaidi ku-*import* kuliko ku-*export*. Hili ni ombi langu sana, kwenye hili, tulizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wanasema, "Serikali iweke mkazo katika kuboresha makusanyo." Hoja siyo kukusanya, Serikali inajitahidi sana kukusanya mapato, sina hakika, sijawahi kuongea na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, lakini ninadhani huwa hana muda wa kupumzika. Kwa hiyo, *issue* siyo kukusanya, *issue* ni uwezo wetu wa mifumo isomane na kusimamia matumizi mabaya. Kwa mfano, juzi tumesema hapa kwamba Serikali inatoa maelekezo lakini watendaji wetu bado wanaona kama yale maelekezo ni makaratasi. Kwa hiyo, naona hapa kwamba *issue* siyo kuongeza ufanisi kwenye kukusanya, hapana, bali tuongeze ufanisi kwenye usimamizi wa matumizi ya fedha zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema huko nyuma kwamba, tunaweza kufanya makosa kwenye kukusanya, lakini hatuwezi kufanya makosa kwenye matumizi kwa sababu taratibu ziko wazi. Inakuwaje leo tunatumia au tunapoteza zaidi ya shilingi bilioni 600, *simply* kwa sababu hatufuati kanuni za matumizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *issue* siyo kukusanya, *issue* ni tabia zetu na watendaji wetu kutokuheshimu sheria za mambo ya fedha, na bahati mbaya kwa sababu wanajua *loopholes* wanakimbia nazo na wanafanya wanachokitaka. Kwa hiyo, hilo naomba niliwekee mkazo. Kamati imeandika vizuri, lakini

nataka Serikali waliangalie vizuri kwa sababu *issue* siyo kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia mitaji. Watu wengi mpaka sasa wanapenda na wangependa kuja kuwekeza. Hata hivyo, pamoja na kujitahidi bado inaonekana uko ukiritimba wa hali ya juu kwa wawekezaji wanapotaka kuja kuwekeza. Wizara zimekuwa nyingi na idara zimekuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nawapa ushauri wangu ambao ni huu, kwamba, tutengeneze *single window system* ambayo mwekezaji akija hapo hakuna haja ya kwenda *TRA*, nenda Uhamiaji, nenda Polisi au *TIC*, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu pale China, ukienda ndani ya saa 12, umemaliza hizi biashara. Dawati limeanza kule mpaka huku. Sisi inakuwaje mpaka mwekezaji anapoteza matumaini? Kwa hiyo, hili naomba sana, naamini kwa weledi wa Mheshimiwa Waziri anaweza kuandaa mazingira ili wataalamu wetu wakajipanga. Haina haja mwekezaji azunguke nchi nzima eti anataka kuwekeza. Sisi ndio wahitaji wa ule uwekezaji, sio wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo naomba niende kwenye ukurasa wa 12 kwenye hiki Kishikwambi. Ukurasa huu wa 12 unazungumza kwenye ukuaji wa uchumi Afrika Mashariki. Sasa kuna nukuu moja tu hapa ningetaka niitumie. Anasema kwenye suala la kukuza huu Uchumi, naomba ninukuu: "Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ukuaji huo, Kamati inashauri yafuatayo: kwanza, takwimu zinaonesha kwamba Sekta ya Huduma imekua kwa kasi ukilinganisha na Sekta ya Uzalishaji."

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo lazima yaende *hand in hand*. Kama unataka kufanikiwa kwenye biashara, ni lazima kwenye kuzalisha na huduma tuoane au uzioanishe. Haiwezekani unataka kutoa huduma nzuri lakini hauna ulichokizalisha, au unazalisha na huna huduma nzuri. Kwa hiyo, pamoja na huduma zetu nzuri, mambo haya Serikali iwekee nguvu ili kuhakikisha kwenye huduma na uzalishaji zinakwenda

pamoja. Kwa hiyo, Kamati imelizungumza vizuri, naomba sana tulifanyie kazi kwa sababu litatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna haja ya kuhakikisha kwamba, bajeti ya Sekta ya Kilimo inatolewa kwa wakati na miradi inakamilika kwa wakati, kwa sababu Sekta ya Kilimo huchangia 26.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeongeza bajeti kwa zaidi ya 100% kwenye hoja ya Kilimo. Hata hivyo, bado inaonekana hatujafikia viwango ambavyo vikatufanya tuweze kuzalisha vizuri. Sisi tutumie vizuri, lakini pia tuweze kufanya mauzo nje ya nchi. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, Serikali ijitahidi; moja, ya mambo ya kuhakikisha kwamba tunazingatia matumizi yetu vizuri, ni kuiwezesha Wizara hii ili iweze kuongeza asilimia ya mchango wake kwenye pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye *page number 14 (ii)* inasema: "kuweka mazingira wezeshi kwenye Sekta ya Madini." Nina mashaka na takwimu za mchango wa madini kwenye Taifa letu. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye tena *homework* yake vizuri na aje atuambie huu ndiyo mchango halisi wa Sekta ya Madini? Ni kweli hiki ndicho tunachozalisha? Au kipo kingine ambacho tunazalisha na hatukioni humu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aifanyie kazi hii na aje atuambie kwamba, hapa kuna upungufu, ama tumepungua, ama tumeongeza. Kwa sababu nina mashaka na hili kwa sababu wenzetu huko nje takwimu zao za madini ni kubwa. Madini yale wanayatoa wapi? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili alifanyie kazi na aje atuambie kwamba, kweli hii ndiyo hesabu ya madini na ndiyo mchango wa madini kwa Taifa letu kwa sababu bado nina mashaka makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye mchango mmoja wa mwisho kwenye suala la madeni ya Serikali. Naomba ninukuu tena kidogo sana ili ikae kwenye kichwa changu. Anasema, "Deni la Serikali hadi Juni, 2024 lilikuwa ni shilingi trilioni 96.88 ikilinganishwa na trilioni 81.98 kwa mwaka

2023." Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, deni letu sasa ni shilingi trilioni 96.88.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu liko hivi, uko ushauri mwingi umetolewa hapa, kwa mfano, kuongeza wigo wa ukusanyaji. Nimesema *issue* siyo kukusanya, *issue* ni matumizi. Pia, mikopo inayopatikana ni vema Serikali ikaielekeza kwenye miradi, lakini vilevile, kutoa kipaumbele kwenye mikopo ya masharti nafuu na kuvuta vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* siyo kukopa, *issue* tunafanya nini kwenye mikopo yetu? Hata hivyo, *all in all* kukopa siyo fahari. Hata nyumbani kwako unapodaiwa unakuwa dhalili. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunapambana ili kukuza uchumi wa Taifa letu, bado iko nafasi kwa wataalamu wetu wakatafakari wanatutoaje hapa? Kwa sababu inaonekana tunasikia fahari kukopa. Kukopa siyo fahari. Tujibane, tujilazimishe ili tuondoke hapa. Tujiwekee mipango kwamba, ndani ya miaka 10 ijayo Tanzania kama Tanzania tuwe hatukopi tena kwa sababu kukopa siyo fahari na kukopa siyo kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumebanwa, lakini hatuna pa kutoka. Ila naamini kwa sababu wale wataalamu wetu ni wazuri, wanaweza wakatusaidia tukajiwekea mipango yetu kwamba, ndani ya kipindi cha miaka 10 Taifa hili liwe halikopi tena, kwa sababu tokea tumepata uhuru, tunakopa, tunaongeza na tunalipa. Maana yake sisi tumejiweka kwenye makucha ya watu, kazi yetu ni kuwafanyia kazi tukawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halipendezzi na halioneshi uwezo wetu wa elimu kwamba tumeelimika na tuna uwezo wa kujitoa mahali tulipo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor. Nilimtaja Mheshimiwa Soud Jumah, na Mheshimiwa Japhet Hasunga, ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2025/2026. Pia

nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa uwasilishaji mzuri, lakini pia na timu zao ambazo zimetayarisha haya maandiko na wao kuweza kuyawasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Nitagusia sekta tatu, nitaanza na Sekta ya Mazingira. Kama tunavyojua kwamba nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la janga la uharibifu wa misitu, halikadhalika na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua kwamba, Tanzania tunapoteza hekta 400,000 za misitu kwa mwaka kutokana na utumiaji mbaya wa misitu, ukataji, kilimo kisicho endelevu na kadhalika, vilevile, kwa Zanzibar tunapoteza karibu hekta 1,000 kwa mwaka. Ukiangalia kama *trend* itaendelea kama hivi, basi kuna hatari kubwa kwamba Tanzania itapata shida kubwa ya kimazingira huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini tufanye? Juzi katika mchango wake Mheshimiwa Abdallah Mwinyi, aligusia hapa kwamba pamoja na Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia ni kinara wa nishati safi na salama ya kupikia, pia tumepiga hatua nzuri kwa kiasi fulani, pamoja na *promotion* ambazo zinafanywa za majiko ya *LPG (Liquefied Petroleum Gas)*. Vilevile, kwa sababu chanzo kikubwa cha uharibifu wa misitu ni ukataji wa misitu kwa nishati ya kupika ikiwemo mkaa na kuni, sasa kama tunataka suluhisho la kudumu ni lazima twende kwenye *LNG (Liquified Natural Gas)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaweza kutoka hapa, tukakwamuka kwenye Mradi wa *LNG* ambao kwanza utakwenda kuchochea uchumi wetu, na pia utatusaidia kutuondoa kwenye mkwamo wa uharibifu wa mazingira. Kwa sababu *LNG* tutazalisha hapa kwetu, itakuwa rahisi *(affordable)* kwa sababu hii nishati ya *LPG* ni safi ila siyo *affordable* (siyo rahisi). Sasa *LNG* itakuwa ni safi na salama, lakini pia itakuwa ni rahisi, yaani *affordability* yake itawezekana kwa kila mmoja wetu. Kwa hiyo, naomba hili kwenye Mpango wetu huu Mheshimiwa Waziri akazingatie sana mradi huu wa *LNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kwenye suala la mazingira. Kama tunavyojua ni kwamba, tumekwama kwenye sera ya mazingira. Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ingekuja hapa kabla ya kumaliza Bunge hili, lakini Bunge hili linaendelea ila naona bado Sheria ya Mazingira haijaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira kwenye Mpango huu ni muhimu tuizingatie kwa sababu itakuja na mfuko wa fedha kwa ajili ya matatizo ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mpaka sasa hivi tuna tatizo kubwa la *climate financing*. Sisi tunakwenda kwenye midahalo ya Kimataifa, tunazungumzia kuhusu masuala ya wenzetu huko Wazungu na wenzao waingize fedha kwenye mifuko kama vile mifuko ya *Loss and damage* na kadhalika, lakini hapa nyumbani hatujafanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tunashinikiza wenzetu huko watunishe mifuko ya mazingira, akina *GCF, Adaptation Fund*, lakini na hapa ni lazima tufanye vya kutosha ili kuhakikisha tunakuwa na Mfuko wa Mazingira. Siyo kuwa na Mfuko wa Mazingira tu, lakini twende tukau-*operationalize* ufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili naomba sana lishughulikiwe, kwa sababu pamoja na kwamba Mfuko wa Mazingira utakuwa na Sheria mpya, lakini pia tutakwenda kuwa na Mamlaka ya Hewa Ukaa. Hapa tunazungumzia hewa ukaa na faida zake, lakini mpaka sasa hivi hakuna chombo cha kusimamia hewa ukaa. Tukiwa na Sheria mpya, itakwenda kuja na Mamlaka ya Hewa Ukaa. Halikadhalika, *NEMC* kuwa mamlaka bado ni changamoto nyingine kwa sababu *NEMC* bado haina meno ya kutosha. Hata hivyo, tutakapokuwa na Sheria mpya, vilevile imezingatia *NEMC* kupandishwa hadhi kuwa mamlaka. Kwa hiyo, ningeomba Mpango huu uzingatie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niende kwenye suala zima la maji. Kama tunavyojua maji ni uhai, maji ndiyo rasilimali pekee ambayo binadamu akiikosa, basi ni changamoto kubwa kwake. Sasa, *Alhamdulillah* lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Awesu, amejitahidi sana na timu yake. Wamefanya kazi nzuri kwenye maji, na ile 95% kwa mijini na 85%

kwa vijijini inakwenda kufikiwa kwa haraka, kwa sababu tunaona azma na nia yao njema na utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa sasa, ili tuweze kufika katika Ilani inavyotuelekeza, kuna miradi 247 ambayo Wizara ya Maji wanaitekeleza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tuhakikishe miradi hii inazingatiwa kwenye Mpango na inakwenda kuzingatiwa kwenye bajeti na inapelekewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tutakuwa tunaimba nyimbo hapa za maji, maji, maji, lakini bila ya kuwa na fedha za kutosha, hii miradi ambayo iko kwenye *pipeline* inaendelea kutekelezwa, kama haikupatiwa fedha itakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, naomba sana twende tukaushughulikie Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Maji umekuwa ukiyumbayumba. Mara fedha zinapokusanywa zimekuwa zikipelekwa kidogo, mara kuna pungufu na nini. Naomba ule Mfuko kwa utaratibu wa mara hii, uende ukapatiwe fedha kwa uhakika na fedha za kutosheleza ili ukasaidie utekelezaji wa mambo mengine pamoja na hii miradi 247.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika suala zima la vyanzo vingine vya mapato, kwa sababu mfuko umekuwa sasa hivi ukitegemea tu *TRA,* wakusanye fedha na wawaingizie, hakuna vyanzo vingine mbadala. Pia, naomba Mpango uzingatie kuweza kusaidia kuja na vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitakwenda kuingizwa katika Mfuko wa Maji ili kuutunisha Mfuko wa Maji na kuweza kushughulikia masuala mbalimbali ya huduma za maji ikiwa ni pamoja na visima hivi ambavyo sasa hivi vinachimbwa kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge hapa isipokuwa sisi Zanzibar, anapatiwa visima vitano, nafikiri na sisi tutafikiriwa. Sasa yote haya itategemea Mfuko wa Maji utakavyokuwa na fedha za kutosha. Kwa hiyo, twende tukaangalie vyanzo vipya vya mapato ili kutunisha mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kuna suala zima la uvunaji wa maji. Nchi yetu Mwenyezi Mungu ameijalia kubarikiwa

maji mengi na mvua nyingi. Hata hivyo, shida tuliyonayo haya maji hatuyavuni vya kutosha. Matokeo yake baada ya kuwa neema inakuwa nakama, yaani inakwenda kusababisha majanga katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwa sababu *potentiality* ya uvunaji wa maji wataalamu wanatuambia ni karibu lita bilioni 146, lakini mpaka sasa hivi tunavuna lita bilioni 40 tu, kwa hiyo, bado tuna safari ndefu ya kwenda mpaka tufikie hatua nzuri ya uvunaji wa maji. Kwa hiyo, Mpango huu naomba sana uende kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie kuhusu ushirikiano wa Zanzibar na Serikali ya Muungano. Najua kwamba Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi amefanya kazi nzuri sana katika miundombinu hasa ya barabara Zanzibar. Hivi sasa kuna *flyover* zinajengwa, na pia kuna barabara mpya zinajengwa na zile za zamani zinatengenezwa. Kwa hiyo, kwa kweli anafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tusiondoe shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Khalid ambaye ni Waziri wa Miundombinu. Kwa kweli anaifanyia haki nafasi aliyopewa kwa kufanya kazi nzuri za kutengeneza miundombinu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini nazungumza hivi? Siyo kusifia tu, lengo langu hapa ni kwamba, sekta hizi zinategemea sana fedha kutoka vyanzo mbalimbali zikiwemo Benki na taasisi nyingine za kifedha. Kwa hiyo, naomba katika Mpango huu tukakae na Mawaziri wa Zanzibar akiwemo Waziri wa Uvuvi. Kule kuna meli kupitia *IFAD* kama tatu za uvuvi kwa Zanzibar zinatakiwa zinunuliwe, tukaziweke kwenye Mpango. Pia, hii miundombinu ya barabara inahitaji fedha kutoka kwenye benki, mikopo na misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukakae na Mawaziri wa Zanzibar pamoja na Watendaji wao, tuweke utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha ili hii miradi ambayo Mheshimiwa Dkt. Mwinyi anafanya kazi kubwa, basi isiende kukwama. Tuhakikishe kwamba, mwaka mmoja uliobakia wa Mheshimiwa Dkt. Mwinyi

na Mheshimiwa Mama Samia, basi unakwenda vizuri zaidi kwa kuhakikisha zile ahadi zote na miundombinu yote ambayo sasa hivi iko kwenye *pipeline,* inakwenda kukamilika. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Hasunga, na Mheshimiwa Yustina Rahhi ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na uzima ili nami niweze kushiriki katika kutoa mchango wangu kwa Wizara hizi mbili. Jambo la kwanza nampongeza sana Waziri wa Mipango na Uwekezaji kwa taarifa yake nzuri sana aliyoitoa, na *framework* ya Mipango ambayo ameitoa, kwa kweli inaonesha mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya na Mwongozo wa Bajeti ambao ameutoa, unaokwenda kuhitimisha katika Mpango huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo amezifanya. Kwanza, katika kuongeza uwekezaji katika sekta za uzalishaji, amewekeza fedha nyingi sana kwenye sekta za uzalishaji. Pia, amewekeza fedha nyingi sana katika sekta za huduma mbalimbali ambazo sasa hivi tunaziita *economic services*. Kwa hiyo, kwenye eneo hili amewekeza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwekeza kwenye huduma mbalimbali ambazo Serikali ya Awamu ya Sita imewekeza ikiwemo Sekta ya Elimu, Afya na Maji ambapo ndipo tunaandaa sasa maendeleo ya watu, wawe na ujuzi na afya nzuri ili waweze kushiriki katika uzalishaji, lakini tunaona kuna changamoto ambazo bado zipo. Pia hizi changamoto zimekuwepo toka tunapata uhuru na mpaka leo nyingine bado zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mbalimbali zimejitahidi sana kutatua hizi changamoto kuanzia ya Awamu ya Kwanza mpaka hii ya Awamu ya Sita, tumewekeza sana lakini bado tunaona changamoto zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ambayo naiona na Mpango huu ambao tunao leo, lazima utupeleke katika kuitafutia ufumbuzi, ni changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Hili tatizo la ajira ni lazima tulitafutie ufumbuzi. Sasa hivi kuna vijana wengi ambao wamesoma katika vyuo mbalimbali, vyuo vikuu, vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya elimu ya kati na wengine ambao wamesoma elimu ya kawaida, lakini wengi bado hawana ajira za kujiajiri na hawana ajira za kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali ya namna hii tunapotaka kujenga Taifa lililo imara kiuchumi linalohitaji watu wenye uwezo wa kufanya kazi na ujuzi, lazima tuhakikishe kwa kweli hili tunaliwekea mkakati wa namna ya kulitafutia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vijana wanavyotembea mitaani huko na vyeti, wanavyotembea na wamebadilika imekuwa sasa ni Taifa la ombaomba. Vijana wengi wameingia katika sehemu ya *betting* kwenye mitandano mle, ku-*bet* kwamba wanaweza kutoka kwa kufanya hivyo. Nafikiri tutajenga Taifa imara kwa kufanya vijana wote na watu wote waweze kujiajiri, wafanye kazi katika maeneo mbalimbali ya huduma na uzalishaji, ndiyo tutajenga Taifa ambalo litakuwa ni Taifa himilivu, Taifa lenye uchumi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ninayoiona ni umaskini mkubwa ambao watu wengi wanao. Sasa hivi kwa takwimu tulizonazo karibu robo ya Watanzania bado wanaishi katika umaskini mkubwa. Tumepambana na hilo tatizo miaka nenda rudi, lakini bado kuna changamoto hiyo 26% ya *population* bado wako kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango huu lazima utuonyeshe tunatokaje hapa? Tutapunguzaje huu umaskini

kutoka 26.4% na sasa tuirudishe chini angalau Mpango utupeleke labda tufike hadi 10% ya watu ambao hawajiwezi, tutakuwa tumepiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hivyo, na bila kuondokana na hili, maana yake tutashindwa kujenga uchumi mkubwa, uchumi himilivu, uchumi ambao tutaweza sasa kuwa ni himilivu katika masuala mbalimbali. Kwa hiyo, nami nashauri kwamba mipango hii itupeleke hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii ambayo tunaifanya ambayo ni ya awamu ya mwisho katika huu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, sasa utuonyeshe namna gani tunaenda kujenga uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda ni pamoja na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi viwanda ni kitu muhimu sana na ili viwanda viweze kujengwa, tunahitaji kuwekeza ipasavyo kwenye vile viwanda vya awali *(extractive industries)* ambazo zikitoa ile malighafi, tuongeze thamani ziende sasa kwenye kuongeza thamani, pale ndiyo tutakuwa na *manufacturing industries* ambazo tutazalisha bidhaa mbalimbali na ndiyo hapo sasa tutaweza kujenga Taifa lililo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya hayo, tukiongeza uzalishaji, tutumie fursa tuliyonayo kama Taifa ambalo Tanzania iko mahali pazuri pa kuweza kufanya biashara. Sisi tukizalisha vizuri kwenye viwanda, tukazalisha vizuri kwenye maeneo mengine, maana yake sasa tutakuwa na uwezo wa kufanya biashara, tutahudumia nchi mbalimbali za Kusini mwa Afrika, nchi za Afrika Mashariki na nchi nyingine za nje, tutakuwa na uwezo wa kuzihudumia siyo tu kwa kuwauzia malighafi, Hapana. Tuuze bidhaa ambazo zimeshakamilika ambazo ni *finished product* ndiyo zitatuwezesha Taifa kuwa na uchumi ulio mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hayo, kule Mkoa wa Songwe na Mikoa ya Nyanda za juu tunayo Barabara ya TANZAM. Barabara ile inatoka Dar es Salaam kwenda mpaka Zambia inaunganisha na nchi za *SADC,* ile barabara kutoka

Igawa mpaka Tunduma sasa hivi imeharibika kwa kiwango kikubwa na ni barabara muhimu sana kwa sababu inapitisha magari mengi na bidhaa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na mikataba tuliyosaini mwaka 2023 nafikiri mpaka leo hakuna ambacho kinaendelea kwa sababu ule mpango wa *EPC+F* inaonekana bado una changamoto. Sasa hebu tutafute namna ya kufanya ili ile barabara ikamilike tuweze kuendelea kutoa mchango wa kiuchumi katika eneo la kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ni muhimu sana katika ile mikoa ni uimarishaji wa reli ya *TAZARA*. Nampongeza Mheshimiwa Rais, tuliona alipoenda ziara nchini China wamezungumza na baadhi ya mikataba wamezungumza namna ya kuifumua na kuiimarisha *TAZARA* ili iweze kutoa mchango mkubwa. *TAZARA* ni kiungo kikubwa sana katika mikoa ya nyanda za juu kusini katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hapa katikati tunayo *SGR* na maeneo mengine na kule tukiwa sasa na *TAZARA,* reli ya *TAZARA* ikiimarishwa, ikakaa vizuri, ikawa kwenye *standard gauge* kama ilivyo *SGR,* maana yake uchumi wetu utakuwa umekaa vizuri sana, tutakuwa na uwezo sasa wa kusafirisha hata bidhaa kupeleka nchi za *SADC* na hivyo kazi tuliyoifanya ya kupigania uhuru katika nchi za Afrika ya Kusini itakuwa na manufaa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale Mpemba tunahitaji pawe na bandari kavu ili ile mizigo inayosafirishwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam inayokuja na treni iweze sasa kukaa pale na watu kutoka Kongo, Zambia, Malawi, Zimbabwe waje kuchukulia mizigo pale. Wakichukulia pale, ndipo uchumi wetu utakuwa umekua na utaweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo lazima nazo ziimarishwe ili ziweze kuunganishwa na reli, ziunganishwe na viwanja vya ndege kusudi mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona kule kwa sababu Mkoa wa Songwe ni mkoa wa kilimo, na sisi tunalima sana, tulijenga maghala ambayo yamekaa kwa muda mrefu mpaka leo yamekaa. Zile fedha zilikuwa ni za mkopo, sasa majengo yamekamilika kwa 70%, mpaka leo yamekaa hayawezi kutumika. Kwa hiyo, ina maana thamani ya fedha inakuwa haipo bila kuyakamilisha haya maghala. Kwa hiyo, vile vihenge vilivyojengwa pale tunaomba Serikali katika Mpango huu ione namna ya kuvikamilisha ili viweze kutoa mchango mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimepigiwa simu nyingi sana, wananchi wa Jimbo la Vwawa wameuza mahindi toka mwezi wa Tisa, wa Kumi mpaka sasa hawajalipwa na sasa wanaenda kwenye kilimo. Tunataka wakazalishe zaidi wakanunue pembejeo na Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mipango mizuri sana katika kuwasaidia pembejeo wakulima, ruzuku ipo, mbolea zipo, mbegu zipo sasa ili wakazalishe wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ihakikishe kwamba kwa kweli inawasaidia, inawalipa mara moja waweze kununua pembejeo hizo, waweze kwenda kuzalisha. Tunahitaji tuzalishe kahawa kwa wingi, tuzalishe mahindi kwa wingi, tuzalishe kila aina ya mazao ili tuweze kuya-*process* na kuyaongeza thamani na kuyauza nchi za nje yatuletee fedha za kigeni na tujenge uchumi mzuri na vijana wetu wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata, naomba niwatangaze wageni waliopo Bungeni jioni hii.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylivester Mabula, mtoto wake kutoka Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 24 wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Watumishi 125 wa Shirika la Kimataifa linalohusika na kutafsiri lugha mbalimbali duniani kwa lugha za asili *(Seal International)*, karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Askofu Gwajima, ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026. Kwa nafasi ya pekee ninampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mipango yote iliyopita amesimamia utekelezaji na hakuna kilicholala. Miradi mikubwa imetekelezwa; *SGR* tumeiona, Bwawa la Mwalimu Nyerere tumeliona, miradi ya kati na miradi midogo ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza kwa sababu bajeti ya kila mwaka imeendelea kupanda. Ukiangalia bajeti ya mwaka 2021/2022 tulianza na shilingi trilioni 36, bajeti imeendelea kuongezeka. Hii tunayoendelea kutekeleza imekuwa kwenye shilingi trilioni 49, lakini sasa tunaenda kutekeleza bajeti ya shilingi trilioni 55. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* hapo ni kwenda kutafuta makusanyo, ukizingatia bajeti yetu ni *cash budget,* tunachokipata ndiyo tunachopeleka kwenye matumizi. Kwa hiyo, tunachotakiwa kwanza, namba moja ni jinsi ya kwenda kukusanya haya mapato tunayoona hapa kwenye *figure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na Wizara, *concentration* kubwa kwenye Mpango wetu huu wa 2025/2026 ni namna gani tunaenda kupata vyanzo vipya vingi vya uhakika ambavyo tunaweza kupata mapato hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mapato sehemu kubwa tunachukua kodi kutoka kwa wananchi, kwa wafanyabiashara na viwandani. Mamlaka ya Mapato *(TRA)* inafanya vizuri sana, nami ninachukua nafasi hii kuwapongeza kwa sababu kila mara *TRA* imekuwa ikivuka lengo na kwa nafasi ya pekee nampongeza sana Meneja wangu wa Mbulu Bibi Noela, anafanya vizuri sana. Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi ya kum-*promote* yule dada kwa sababu anasikiliza sana wateja wake. Wafanyabiashara wakienda na changamoto zao, yule dada anawasikiliza vizuri, wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, pengine tuwe *rationale* kwa mfano, tunapoongeza kila mwaka kodi kwenye viwanda, hata nikitoa mfano labda kiwanda cha kutengeneza pombe, bia hizi tukasema pengine haina athari kwa sababu pombe pengine siyo bidhaa muhimu sana kwenye maisha ya binadamu, lakini athari ipo pale pale kwa sababu ukiongeza kodi, ile kodi inaenda kumwathiri yule *consumer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *consumer* pale lazima bei itapanda na kwa sababu hiyo anaweza aka-*shift to another utility,* akaenda pengine kwenye kutafuta labda kilevi kwenye pombe za kienyeji ambapo kule Serikali inashindwa kupata kodi. Vilevile ni mbaya kwa afya yake lakini huku pia *production* itakuwa imepungua na Serikali pengine inaweza isipate kiwango kile cha kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa huo mfano lakini niseme kwamba viwanda vyote vya ndani vikizalisha bidhaa, bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi yetu ni ghali kuliko bidhaa zinazotoka nje. Hii ni kwa sababu ya gharama kubwa ya uzalishaji na gharama kubwa mojawapo ni kodi. Tukiwa tunaongeza kodi sehemu moja kwa wafanyabiashara na viwandani athari yake ndiyo hiyo ukiingiza vitu kutoka nje iwe chakula, iwe nguo, iwe vyombo vya ujenzi, vya nyumbani gharama za vitu vinavyozalishwa nje ya nchi yetu siku zote ni ndogo kuliko tunavyozalisha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili viwanda vyetu viwe shindani na kukuza uchumi wetu, tuangalie vyanzo vingine

ambavyo tunaweza tukapata mapato na tuwe *rationale* kwenye kuongeza pengine kodi kutoka kwa wafanyabiashara ambao tunajua wako *stationary* utawakuta pale na viwanda viko *stationary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa mfano kuna vyanzo tumeviacha, watu wameongea sana kuhusu Liganga, kila mwaka tunaongea Liganga na Mchuchuma na mwekezaji huyu tumesogea naye zaidi ya miaka 20, kila mwaka imekuwa ni *discussion,* ni kwa nini sasa Serikali kwa kutaka kukuza uchumi wetu isiamue kwa vyanzo vyake yenyewe kwenda kutekeleza huu mradi kama ambavyo imeshatekeleza miradi mkubwa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere? Kwa sababu hivi ndiyo vyanzo vya uhakika baadaye vitakavyosaidia uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo, kwa mfano nishati, nishati ni chanzo cha uhakika kinachokuza uchumi wetu. Tumekuwa na vyanzo vya kuleta nishati kwa mfano maji. Umeme tunaufua kutoka kwenye *hydroelectric power,* lakini tuna *potential* kubwa sana ya kuongeza umeme. Umeme huu hautoshi hata kwa matumizi ya ndani, lakini tungekuwa na fursa ya kuuza umeme nje ya nchi yetu, kwa sababu nchi yetu imezungukwa na mabwawa na mito na maji ya kutosha, ni kwa nini basi hata kwenye kuzalisha kwenye *small scale,* kama siyo Serikali, iruhusu hata watu binafsi wazalishe umeme halafu waje wauzie *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukija kwenye Halmashauri ya Mbulu, mto mmoja unaitwa Mto Haino, una *very nice water falls* ambazo ungeweza ku-*generate hydro-electric*. Nami naomba Waziri wa Nishati kama yuko hapa atembelee chanzo kile, ingeweza kuzalisha umeme kwa ajili ya Mbulu pengine na Babati. Hii tugeweza kuzalisha umeme kwenye chanzo cha gesi, upepo, na hata joto la ardhi ambapo kule Busekelo wamesha-*test* lakini hatuoni ni kwa kiwango gani inaongezwa. Hiki kingekuwa ni chanzo kizuri sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo, pia nchi yetu *geographically* Mungu alivyotubariki ingekuwa ni lango la

biashara hata kwa nchi za jirani kwa maana kuwa na bandari na bandari kavu, lakini ukitembelea hizi bandari ukatembelea biashara mipakani, ukaenda Mtukura, Horohoro, Namanga na sehemu nyingine, ufanisi kwa upande wa Tanzania siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukienda Mtukula, ukivuka upande wa Uganda utaona kwa kiasi gani biashara ile inafanyika kwa ufanisi. Wenzetu wana *scanner.* Mizigo ikifika pale itapekuliwa kwa *scanner,* wako *very fast.* Ukija Tanzania huku vitu vinafanyika *manually,* mizigo ile itashushwa itapekuliwa mmoja baada ya nyingine kwa ajili hiyo kuweka msururu wa usafiri na kwa ajili ya wenzetu wa jirani ambao wangetumia mipaka yetu na bandari zetu wana kila sababu ya kutukwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda bandarini, kontena nzima imebeba labda friji, kwa kuhisi pengine ndani ya friji kuna kitu kimefichwa friji zote zinashushwa *manually* na kupekuliwa *manually* zije zirudishwe ndiyo maana kuna *waiting charges* nyingi sana. Kwa hiyo, ni kwa nini basi tusifanye shughuli hizi kiutalaamu zaidi ili angalau Tanzania hii yenye fursa kuwa namna hiyo tukaweza kuboresha uchumi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hapa, kukusanya mapato ni jambo lingine, wamesema wenzetu, ukusanyaji wa mapato tunakusanya kwa uchungu mkubwa sana. Ukienda kwenye halmashauri ndiyo utazielewa halmashauri, Wakurugenzi wamewekewa malengo. Mkurugenzi anaambiwa ukikusanya chini ya 80% wewe sio Mkurugenzi, ukifika siku nyingine Mkurugenzi na wataalamu wake wako kwenye mageti usiku wanatafuta hivi wafikie 80% wanakusanya vyanzo, lakini ikishakusanywa ni kiasi gani inaenda kwenye maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria tunavyoenda kutekeleza Mpango wa 2025/2026 kama ni sheria, au ni kanuni ziletwe tukubaliane kabisa kama angalau siyo 40%, tukubaliane lazima kiwango cha fedha kirudi kule kwenye *development projects* akitwaa fedha mfanyabishara apite kwenye barabara nzuri ikikusanywa ushuru kutoka halmashauri, watu wapate maji, na huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, asilimia fulani irudi, isitoshe tu kwamba hizi fedha ni za safari za watalaamu, pengine Serikali kununua magari kila wakati, tuone namna gani tunabana matumizi na hizi fedha zirudi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba chanzo cha uhakika baadaye ni kilimo, na sekta zote za kiuchumi. Nashauri Mpango wetu wa 2025/2026 uwekezaji uendelee kuwekwa kwenye sekta hizi za kiuchumi ikiwepo kilimo, mifugo na maliasili. Kuna changamoto kote, ukiangalia kwenye mnyororo wa thamani wa mazao hata ukifanya uzalishaji sana, bado masoko ni changamoto kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuanzia mwanzo tuone, kwanza tuna uzalishaji mdogo, kwa sababu bado kuna changamoto kwenye hatua ya kwanza ya mnyororo wa thamani. Kwanza changamoto kubwa ni pembejeo. Namshukuru, na ninampongeza Rais kwamba kipindi hiki kwenye pembejeo mbegu zimepata ruzuku, mbolea zinapata ruzuku kitu ambacho naona pengine haitakuwa *sustainable in future*. Kinachotakiwa hapa ni sisi kuweza kuzalisha mbegu za kutosha na bora ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza waliokuwa wanatuzalishia majirani zetu, kwao kuna ukame, ni fursa kwetu Watanzania kwa sababu tuna ardhi nzuri na mazingira mazuri, tuzalishe mbegu tuuze nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hili la mbolea, tuhakikishe kwamba viwanda vya mbolea viko huku ndani, tuzalishe mbolea zetu za kutosha na ikiwezekana tuzi-*export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine muhimu sana ni kuendelea kuwekeza kwenye umwagiliaji. Tunachohitaji kwenye umwagiliaji ni kwamba hatuna maji na kama hatuna maji, kinachotakiwa ni kuwekeza kwenye mabwawa ya umwagiliaji pamoja na miundombinu mingine. Tuna *potential* kubwa sana, tuna maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji, kwa hiyo, natamani kuona Mpango wetu wa 2025/2026 umetenga fedha za kutosha kwa ajili ya umwagiliaji pamoja na kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakuwa na uzalishaji mwingi, lazima tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye *Agro-processing industries.* Kwa hiyo, nategemea kwamba Mpango unaokuja, Serikali iwezeshe *SIDO, CAMARTEC, TERDO* pamoja na *KMTC,* iwape bajeti ya kutosha, iwezeshe hata katika makundi madogo madogo hata kama siyo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ina uwezo wa kufundisha vikundi vya akina mama na vijana kusindika na kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao yanayozalishwa humu ndani. Tukiongeza mnyororo wa thamani kwanza tunaongeza kipato, lakini tunapunguza *post-harvest process. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni muhimu sana kuliko tunavyouza mazao yetu *raw,* mengine yanaharibika hasa *perishable foods* kuwekeza katika *agro-processing industries* kwa sababu tutazalisha vya kutosha. Kwa hiyo, nawaomba tu kwamba hayo mashirika madogo yawezeshwe wapate pesa yawasaidie wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu masoko, Serikali iweke mazingira mazuri. Nafurahi kwamba tumesaini mikataba ya kuuza mazao yetu ya asili kwenye nchi za jirani baada ya kukubaliana na *phytosanitary* kwa sababu hiyo dozi tayari mazao yale ambayo yalikuwa hayauziki nje sasa yanauzwa na mikataba imeshasainiwa. Naomba wananchi wa maeneo hayo wakulima waelimishwe ili wazalishe kwenye ile *standard* ambayo tunaweza tukauza nje ya nchi mazao yale kama parachichi na pilipili na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya mifugo; tuna fursa kubwa sana, tuna mifugo mingi lakini bado hatujapata tija kubwa kutoka kwenye mifugo. Bajeti inayokuja nataka kuona kwamba tumewekeza vya kutosha kwenye mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifugo tuzuie magonjwa kwa maana kwamba tujengewe majosho ya kutosha, lakini kusambaza mbegu za malisho ili mifugo inayokufa wakati wa kiangazi kwa kukosa malisho na maji, tu-*solve* hivyo, lakini

ng'ombe wapate chanjo ili nchi yetu iaminike kuuza mifugo yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi nimemtaja Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii. Pia, namshukuru Mheshimiwa Rais ambaye tangu tulipoanza kuzungumza kwa habari ya kuanzisha Wizara maalumu inayohusika na Mipango na Uwekezaji, alianzishaa mara moja na imefikishwa mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu ni kupokea, kujadili na kushauri Mpango wa Taifa wa Mwaka Mmoja ambao *basically* ni 2025 na 2026. Kupanga ni kuchagua. Kutokupanga ni kuchagua kushindwa, na yeyote ambaye hana mpango, huyo amepanga kushindwa. Narudia tena, yeyote ambaye hana mpango, basi amepanga kushindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipanga kwa muda mrefu gharama za kutekeleza mradi wowote pale duniani zinakuwa chini, lakini mpango wowote wa dharura au unaopangwa kwa muda mfupi, utekelezaji wake huwa ni wa ghali sana. Mfano mzuri ukikata tiketi ya ndege ili usafiri kesho, tiketi hiyo ni ya ghali sana lakini ukikata tiketi usafiri miezi mitatu ijayo, tiketi hiyo inakuwa bei ya chini. Hiyo ndiyo inatuonesha kwamba ukipanga utekelezaji wa mradi au kazi yoyote inayotokana na mpango wa muda mrefu, gharama zake zinakuwa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba katika Bara letu la Afrika nchi tajiri kwa maana ya *natural resources,* nchi yetu ni mojawapo. Kwa *observation* zangu ukiitoa Congo na nchi nyingine kadha wa kadha, nchi yetu Tanzania ni nchi iliyojaliwa na Mwenyezi Mungu *natural resources* za kutosha kuipeleka inakotakiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua natakiwa nijadili Mpango wa Mwaka Mmoja, ninafahamu hivyo, lakini kwa sababu anayepokea Mpango wa Mwaka Mmoja ndiye huyo huyo anayepokea Mpango wa Miaka 25, kwa hiyo, *it does not make a difference* kwa sababu ninazungumza na mtu yule yule au na Serikali ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wote niliokaa katika Bunge hili, sekta sita zikifanyiwa kazi, nchi hii ni tajiri kuliko maelezo. Sekta ya kilimo inaajiri watu wote; inaajiri profesa na inaajiri mtu asiyesoma wala kuandika. Sekta ya uvuvi inaajiri watu wote; inaajiri profesa na inaajiri mtu aliyesoma darasa la kwanza. Sekta ya ufugaji inaajiri watu wote; inaajiri mchungaji, inaajiri profesa na inaajiri mtu asiyejua kusoma na kuandika. Pia, gesi asilia inaajiri watu wote, madini yanaajiri watu wote na utalii unaajiri watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sekta sita zikipangiwa mpango wa muda mrefu zinaweza kuibadili nchi kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Anayebisha anabisha kwa sababu yake binafsi, na hana maslahi ya kutetea nchi yake. Nataka kutoa mfano mzuri kwenye gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia tuliyonayo katika nchi yetu kwa utafiti uliofanyika, tuna vitalu zaidi ya 11 vya gesi asilia na katika vitalu hivyo tuna jumla ya futi za ujazo trilioni 57.54. Ninarudia tena, tuna *cubic feet* trilioni 57.54 za gesi asilia, lakini kwa sasa tunazalisha gesi kwenye vitalu viwili pekee kwa maana ya *Mnazi Bay* iliyoko Mkoani Mtwara pamoja na Songosongo iliyoko Mkoani Lindi. Kwa hiyo basi, tuna futi za ujazo trilioni 47.13 ambazo hazijaguswa kabisa. Ninarudia tena, tuna futi za ujazo trilioni 47.13 ambazo hazijaguswa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize, hii maana yake nini? Ukizunguka kwenye masoko, utaona mitungi ya gesi *Mihan, Oryx*, Puma, *Taifa Gas* na *Oil com.* Mitungi hii yote hakuna hata mtungi mmoja unaozalishwa Tanzania. Mitungi hii yote inatoka Iran, Misri, China na nchi za kigeni na sisi tunayo gesi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tuna *cubic feet* trilioni hizo. Tanzania yetu hii ina mikoa 31, ina wilaya 139, ina halmashauri 184, tarafa zaidi ya 600, Kata zaidi ya 3,655, vijiji zaidi 17,772, vitongoji zaidi 63,000, ina mabalozi kama 1,000,000 na kaya kama 10,000,000. Kwa mujibu wa tathmini ya Wizara yetu, kama tukiamua kuitumia hii gesi yetu, yaani kila nyumba ya mtu ikawekewa gesi, tutatumia gesi kwa muda wa miaka 100. Hii ni *data* ya Serikali, siyo *data* zangu. *It is not my own generated data,* ni *data* za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tukiamua kila nyumba ya Mtanzania tutengeneze bomba la gesi kama ilivyo Ulaya kama lilivyo bomba la maji linalotoa maji ndani ya nyumba ya mtu tuingize bomba la gesi kwenye kila nyumba ya Mtanzania, Tanzania yote tutatumia hii gesi kwa muda wa miaka 100. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake ndiyo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba hatutakata miti. Kwa hiyo, *deforestation* itaondoka. Matokeo mengine mvua itaongezeka kwa sababu hujakata miti na kina mama hawatatumia kuni, mkaa na kinyesi cha ng'ombe kupikia na kuharibu afya zao. Pia, mapato ya Serikali yataongezeka na kukata miti kutapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hatujayaangalia hayo? Ni kwa sababu ya kukosa Mpango wa muda mrefu. Najua kuna gharama za kutimiza miradi kama hii kwa sababu ni miradi mikubwa, lakini mradi unaoufanya ili ukusababishe kupata fedha ndiyo mradi unaoupa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, yule ng'ombe anayekupa maziwa, unampa majani zaidi ili akupe maziwa mengi zaidi, lakini *we cannot do that* mpaka tupange Mpango wa muda mrefu. Hii ndiyo sababu tunayo mitungi yote inatoka nje. Mtungi wowote wa gesi unaouona, hakuna mtungi hata mmoja wa Tanzania. Hii inatisha, inahuzunisha na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi hili ni tatizo la mtu yeyote na ndiyo maana namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kwamba kwa sasa tuanze na Wizara

maalumu inayokuwa na mipango na uwekezaji na bahati nzuri ameiweka chini ya *University,* Ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo awatendee Watanzania kwa namna ambavyo *when you are eighty years old* hutajuta kwamba ulipewa Wizara hii kwa sababu inakuhitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja. Kule kwenye Jimbo la Kawe tumefanya hiyo *study.* Tumeamua kuingiza *gas* kwenye nyumba 480. Wamewekewa gesi, wana mita. Mwenge wa Uhuru ulipita pale, kwenye kila nyumba Kata ya Mikocheni, nyumba 4,000 na kitu yule mtu aliyekuwa anatumia umeme wa shilingi 50,000, sasa hivi analipa shilingi 5,000 mpaka 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana gani? Ina maana kama tuna Mpango wa muda mrefu tukaweka *cable* za gesi kwenye kila nyumba ya kila Mtanzania, gharama za maisha kwa wananchi zitapungua. Itawawia rahisi wananchi ku-*run* maisha yao na Serikali inapata maokoto ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana gani? Ina maana kwamba kila mwananchi wa Tanzania akianza kupika maokoto yanaanza kuingia Serikalini. Narudia tena, hii ina maana kwamba kila jioni Watanzania wote kila mtu atakayepika pesa inaingia Serikalini. Hii inaweza kuibadili nchi yetu kwa namna kubwa mno, lakini ni mradi ambao hauwezi kutekelezwa kwenye awamu moja au awamu mbili, bali ni mradi unaoweza kutekelezwa kwenye awamu nyingi. Kwa hiyo, lazima kuwa na maono ya muda mrefu ili kuwe na *continuation* ya kila awamu mahali inapoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Mawaziri tutawaua bure kwa kufikiri kwamba *they are incompetent in their jobs.* Nikupe mfano, Waziri wa Maji, hakuna mahali na hakuna wakati kwenye Serikali zilizopita Serikali imeweka pesa nyingi kwenye Wizara ya Maji kuliko Mama Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka fedha nyingi kwenye Wizara ya Maji kuliko Rais yeyote aliyewahi kutokea. Hiyo

ni *fact; is a naked truth. You cry, you refuse,* lakini hiyo ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tatizo la maji lipo. Mimi ni Mbunge wa Kawe, Dar es Salaam nimetembea shina kwa shina zaidi ya mashina 1,000, kuna baadhi ya kata Dar es Salaam zinapata maji mara mbili kwa wiki. Pamoja na *investment* hiyo, Kata ya Mbezi Juu, Kata ya Makongo na Kata ya Wazo ni mara mbili kwa wiki. Kwa nini? Ni kwa sababu wakati mnawekeza kwenye haya mabomba ya maji, mnakuwa mmefanya *calculation* ya kaya 1,000 kabla mradi haujaongezeka kuna watu wengine wamejenga tena, tayari kuna nyumba 20,000 na kuna viwanda 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *infrastructure* mliyoitengeneza inashindwa kufua dafu. Matokeo yake wana-*pump* maji mabomba yanapasuka ovyo na maji yanazagaa mitaani, ni kwa sababu ya kukosa Mpango. Tungekuwa na Mpango kabla ya kupeleka maji, hesabu ingefanywa ya uhitaji wa maji kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, *infrastructure* zingefanywa sawasawa na Mpango wa Taifa tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo tunaweza kushindwa kuyasema kwa kuogopa, lakini kupanga ni kuchagua na kutokupanga ni kuchagua kushindwa. Nikupe mfano, nini *solution* ya maji? Ni kutengeneza gridi ya Taifa ya Maji. Narudia tena, *solution* ya maji ni kutengeneza gridi ya Taifa ya Maji, kwa sababu sisi Tanzania hatuna tatizo na vyanzo vya maji. *We have no problem with water sources.* Mara, Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Songwe na Njombe kote kuna maji. *So, we do not have a problem with water sources.* Tuna tatizo na namna ya kuyatawanya haya maji ili yawe na mfumo wa kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wowote wa kutengeneza Gridi ya Taifa ya Maji unagharimu fedha na haugharimu *regime* moja, unagharimu mwendelezo wa *regime* mbalimbali ili kila mahali anapoishia mtu aendeleze mtu mwingine. Ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso amefanya kazi kubwa kuliko kawaida kwenye mambo ya

maji, lakini kama hakuna maono ya muda mrefu, mdogo wangu mtampasua kifua bure. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wana nafasi ya kufanya *summary* baadaye, *relax*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah aendelee!

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mwishoni mtazungumza, *relax, give my time*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gwajima subiri dakika moja.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ni sehemu za Kanuni za Bunge, asiwe na wasiwasi. Anachangia vizuri sana, nataka tu kumpa Taarifa kwamba, tayari Serikali ilishaanzisha *National Water Grid* na ndiyo maana tunatekeleza mradi wa maji kutoka *Lake Victoria* mpaka Dodoma na ndani yake siyo tu maji safi, pia kuna kilimo cha umwagiliaji katika mikoa yote inayopita. Kwa hiyo, mchango wake ni mzuri lakini apokee hiyo Taarifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Askofu unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu sana Profesa. Naomba niendelee. Kwa hiyo, kukiwa na Mpango wa muda mrefu kuna baadhi ya mambo tuta-*solve*, kwa mfano, tuna *Project* ya Liganga na Mchuchuma ambapo maana yake tuna mlima wa chuma na pembeni yake kuna mlima wa makaa ya mawe. Nirudie tena,

kuna mlima umejaa chuma na pembeni yake kuna mlima umejaa makaa ya mawe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Mungu alivyo wa ajabu kwa Tanzania hii, anawapa chuma na anawapa moto wa kuyeyusha hayo makaa ya mawe. Hayo makaa ya mawe yamekuwepo tangu Karne ya 18, hatujafanikiwa kuyeyusha. Siyo kwa sababu ya kosa la Serikali, Hapana. Mimi ni sehemu ya Bunge hili, ni kwa sababu hatuna Mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuonyeshe kwamba hatuna Mpango wa muda mrefu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia hiyo sentensi, kengele imelia muda mrefu.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tumetengeneza reli lakini *component* kubwa ya reli ni chuma. Kwa hiyo, tungeanza kwanza kutengeneza chuma ili kusudi kile chuma tukitumie kutengeneza reli, lakini leo chuma tunaagiza Misri na India kwa sababu ya kukosa Mipango. Tunaanza kujenga reli kwanza, tunaagiza chuma wakati tungeanza kuzalisha chuma halafu ndiyo tukaanza kutengeneza reli ingekuwa nafuu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nitaijadili hii hoja siku nyingine. Mungu awe pamoja na ninyi lakini kukosa maarifa na maono kunaangamiza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, unaweza kupeleka maelezo mengine kwa maandishi, Waheshimiwa Mawaziri watayapokea. Ninaendelea na Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nashukuru kupata hii nafasi ya kuchangia huu Mpango wa Taifa wa mwaka mmoja pamoja na Mwongozo wa

Utengenezaji wa Bajeti. Mheshimiwa Gwajima ameondoka na msemo wake mmoja mzuri nami nina msemo kama ule, “Usipoamua mwenyewe kupanga, basi jua utapangiwa.” Sisi hapa tumeamua wenyewe kupanga, kwa hiyo, hatutapangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ambayo nataka kuchangia ni katika sehemu ambayo inahusiana na rasilimali watu na ninazungumzia eneo la kukuza au kuendeleza ujuzi ambapo niko katika sekta hiyo, nafikiri kwa mwaka wa pili huu na hili neno tunalizungumza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema, ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mimi ninazungumzia watu. Tafsiri ya watu hapa inajulikana kwamba ni watu wenye ujuzi katika maeneo ambayo tunayo katika sekta tofauti tofauti ili tuendelee katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimevaa nguo nyeupe makusudi kwa sababu leo nimejiita *doctor.* Ninataka kuonesha u-*doctor* wangu. Nimevaa nguo nyeupe kusudi. Sasa naanza na *diagnosis* ya hii sehemu niliyoisema ya kukujuza ujuzi. Tanzania tulitakiwa katika watu, watu wenye *low skills* wawe 54% kutokana na uchumi wetu na hali yetu tulivyo lakini tuna hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye *low skills* sasa hivi ni 80%, wenye ujuzi wa kati *(semi-skilled)* wawe *at least* 34 % lakini hadi sasa hivi hawa watu wenye *semi skills* wako 16.6%. Wenye *skill* ya juu *(high skilled labour)* wawe na 12% lakini kwa bahati sasa hivi wako 3.6% ina maana kwamba tuko nje au kama ni mgonjwa, basi ni wagonjwa sana katika eneo hili la ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumeanzishwa utaratibu wa programu hii ya kukuza ujuzi ambapo programu hii iliwekwa ili tuweze kui-*fund* na tuweze kupata watu wenye ujuzi. Programu hii tumeiweka tukasema tutakusanya *Skills Development Levy* ili tuweze kukuza ujuzi na tungeweza kupata katika kipindi cha miaka mitano watu 681,000 ambapo kwa kila mwaka tungeweza kupata watu laki 136,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye takwimu za Serikali unakuta mwanzo tulianza kutoa watu 42,000 tukashuka na tukashusha fedha tukapata watu 12,000. Sasa hivi tunapata watu 10,000. Sisemi labda watu wa vyuo vikuu na sisemi na watu wanaopewa mikopo, wale hawaendi kusoma *skills*. Wale watakapomaliza ndiyo watakwenda kupata *skills*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo ndipo tunapotofautiana. Fedha zile zilikuwa ni makubaliano baina ya Serikali pamoja na sekta binafsi. Hizo fedha zikitoka, ujuzi hapo ukue, kwa maana hiyo katika Mpango ambao tunaujadili hapa bado tunaenda kufeli. Nimeona katika vipaumbele vimeangaliwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri tutakapoandika Mpango sasa, basi hebu hili tujaribu kulitazama vizuri, kwa sababu kama tusipolitazama vizuri litakuja kutu-*cost*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa ninatazama *postmortem*. *Postmortem* hii imefanywa na Kamati ya Bajeti, wanasema bidhaa hazina ubora na ushindani wa kimataifa, kwa sababu gani? Hatukuwa na *skills* na bidhaa zetu sasa zimekosa ushindani na hazina ubora, lakini katika *postmortem* hiyo wamesema matumizi ya teknolojia ya sasa yapo chini bado tunatumia teknolojia ya zamani wakati tuna fedha za kuweza kuwafundisha watu wakapata teknolojia mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *postmortem* nyingine ambayo hatujaifikia ni kwa mujibu wa ilani, ilikuwa tuzalishe ajira 8,000,000. Kwa mujibu wa ripoti ya Waziri wa Mipango kwa sasa hivi tumezalisha ajira 3,221,000. Ina maana moja kwa moja tunafeli katika suala hili. Mheshimiwa Waziri, nakuomba, hizi sekta zote tutasema uchumi umekua na kila sekta tutasema imekua, lakini katika kila *percentage* ya sekta tumeajiri watu wengine wa nje na tumeacha vijana wetu wa ndani kwa sababu, hawana ujuzi na ule ujuzi ni jambo la kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeamua kuchagua kuwapa vijana wetu kukuza ujuzi, basi tukuze ujuzi ili mwakani tuvuke. Sasa Mheshimiwa utakapokuja katika mwezi huo utakaofuata *at least* utupe mambo ambayo ujuzi utaonekana kwamba, umekua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda katika sekta nyingine ya ustawi wa jamii. Kwenye Sekta ya Ustawi wa Jamii, kwenye jedwali, hapa Mheshimiwa ameeleza viashiria ambavyo amevitaja, lakini mimi sitovitaja viashiria vile. Moja kwa moja natoa ushauri, utakapokuja na Mpango huu uje ututajie viashiria. Kule vimetajwa viashiria vitatu na kimoja ni kadi ya Taifa. Sasa, *at least* tunapendekeza tujue idadi ya wazee wanaoishi katika nyumba wanaolelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wazee wanaishi katika nyumba wanazoishi watu wenye ugonjwa wa ukoma ndiko wanakoishi wazee wetu. Serikali ije na Mpango, ije itueleze kwamba, hawa wazee watawafanyia nini? Katika nchi hii kuna nyumba moja tu, Misungwi, ambayo ndiyo imejengwa kisasa, lakini wote wale wapo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, kuna kitu kingine katika masuala haya ya makundi maalum ambayo yapo katika maendeleo ya jamii. Kwenye makundi maalum tumeanzisha programu ya kuwapa Wamachinga vitambulisho, vitambulisho vina tabu kidogo. Hapa tumetaja Vitambulisho vya Taifa, lakini tuangalie na vitambulisho vya Wamachinga. Kama ukija Mpango, uje utueleze utafanya nini katika kundi hili na tunajua kwamba, ni kundi kubwa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ambalo ninalipendekeza kwa Serikali yangu ambayo ninaikubali na ninaiamini na ninajua Mawaziri wana uwezo huo. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, umetoa mwongozo juu ya utengenezaji wa bajeti, katika mwongozo uliotoa utakapokuja na mwongozo mwezi Machi, basi *at least* ugusie mwongozo kwa mujibu wa sheria ambayo tumeipitisha hapa ya kumkinga mtoto. Kule tumetaja mabaraza na haya mabaraza ni mapya, yatakuwa yako katika halmashauri na yatafika mpaka Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa endapo haya mabaraza hayataingizwa katika mwongozo kwamba yapatiwe fedha, ina maana kwamba, sheria tuliyoipitisha juzi aliyoisaini Mheshimiwa Rais haitaweza kuja kwa sababu, inawezekana tukapanga kwa mazoea. Hili jambo halikuwepo mwanzo, tumelileta kwa mujibu

wa sheria na limetungiwa sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa tunaomba utoe mwongozo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tumetaja nafasi nyingi sana katika sheria ile juu ya kupatikana Maafisa wa Maendeleo na Maafisa wa Ustawi wa Jamii. Hii sekta mwanzo ilikuwa haina kipaumbele, kwa hiyo, hebu tujaribu kuangalia Vyuo vya Maendeleo na Ustawi wa Jamii viwepo vya kutosha, ili hizi sheria na mipango mingine tunayopanga iwe inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifika wakati wa kuchangia bajeti hapa, ikifika Siku ya Ustawi wa Jamii, kila mmoja analalamika mparaganyiko wa maadili. Kila mmoja anazungumza mpaka anataka kulia hapa, lakini leo kwenye Mpango hatuzungumzii au hatuwezi kusema kwamba, hicho kitu kifanywe vipi? Tunasubiri kwenye bajeti. Ukija pale kwenye bajeti, ukisema umeshachelewa, unakumbuka mtoto wakati mchuzi umekwisha. Sasa, tunalisema hili mapema kwamba Serikali ije iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalizungumza ingawa ni jambo la miaka mingi kama alivyozungumza Askofu Gwajima. Hili ni Bunge, tuna dira na mipango, lakini je, tuna *vision* gani kuhusu Bunge hili? Maana hili Bunge ndiyo linaibeba Serikali, isije ikawa mikono ya mtoto mchanga inambeba mtu mzima wa miaka 100. Sasa ni lazima tujaribu kuwa na *vision* ya Bunge letu huko mbele litakuwa la aina gani au na pili, lifanye nini na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *research* zipo, zinaonyesha Mabunge ya wenzetu wanafanya nini, wanaenda na mambo gani ya kiutawala na Waheshimiwa Wabunge wanaishi vipi? Sasa na sisi ni lazima tuje na Bunge ambalo kutokana na *vision* hiyo tunayoenda kuizaa huko, basi *at least* liwe linakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda wako, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King. Nilimtaja Mheshimiwa Issa Mtemvu, halafu tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie hoja iliyopo Mezani kwetu iliyowasilishwa na Mawaziri wetu; Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, ambaye amewasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026 na pia Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, ambaye ametuwasilishia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi, aliyetujalia afya pamoja na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi yetu. Anapambana kutuletea maendeleo ya Tanzania ya leo na kesho. Binafsi nawapongeza sana Mawaziri wetu wote wawili, Naibu Mawaziri wawili wanaowasaidia, na wataalam wetu katika hizi Wizara zao mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo mawili tu ya kuchangia. Moja, nitachangia kwenye eneo la Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026 na pili ni katika eneo la Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeendelea kutekeleza sera, programu na miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu. Hili linaongozwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitazungumza juu ya hali ya umaskini na maendeleo ya watu. Kiujumla eneo hili linazungumzwa katika misingi ya kuangalia huduma za jamii zilivyopatikana. Mpango umeeleza vizuri na uzuri Mpango wetu ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, sasa hivi ndiyo tunatekeleza Mpango wa mwaka wa mwisho kwenye ule Mpango wa Miaka Mitano. Tumeanza mwaka 2021/2022 mpaka sasa hivi tunaelekea 2025/2026. Kwa hiyo, mambo siyo tofauti sana, lakini ni mambo yanaendelea kuwa na sura au *vision* ya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais, katika eneo hili kwa kweli amewatendea Watanzania yaliyo makubwa sana. Ni kweli, kwenye eneo la elimu Mheshimiwa Rais amefanya makubwa sana. Anatumia zaidi ya shilingi trilioni 6.17 kwenye bajeti zetu ambazo zimepangwa katika mwaka huu unaoisha, lakini pia, katika mwaka unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo katika maeneo ya afya kawekeza zaidi ya shilingi trilioni 2.5, utawala na deni la Serikali zaidi ya shilingi trilioni 13 na eneo la miundombinu zaidi ya shilingi trilioni 5.5. Hizi ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, unaweza ukaona sura yetu kama Taifa tunapanga na tunaendelea kutekeleza kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa hatua hii nzuri ambayo imeendelea kuifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili kuna maeneo kadhaa. Moja, ni eneo la maji, lingine litakuwa eneo la nishati na eneo la tatu litakuwa ni la ardhi. Hapa kidogo nina ushauri, kwenye eneo la maji, amezungumza Mheshimiwa Gwajima kuisemea sehemu ya Dar es Salaam anayoiongoza. Kwanza natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, kaka yangu Jumaa Aweso, Mbunge, kwa kazi nzuri anayoifanya. Anafanya kazi nzuri sana, Watanzania wanajua na mimi nimeendelea kusema na hata wataalam wake wanajitahidi, lakini bado kuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ambayo ipo, nafikiri ni mgawanyo wa hitaji la huduma ambayo anaisimamia kwenye nchi yetu kila sehemu. Maana, hata yeye ana Kiswahili chake ambacho anazungumza, kwamba "maji hayana subira, maji huwezi kuyaahidi kesho, kila mmoja anayataka leo." Kwa hiyo, kutokana na changamoto ya *resource*

ya fedha ambayo tunayo, ndiyo maana tunajikuta hatuwezi kutimiza kwa kila sehemu, lakini Mpango wetu ni lazima ukalazimishe tufike mwisho katika baadhi ya maeneo watu kuendelea kulia kuhusu huduma ya maji, sidhani kama ni sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kawekeza sana Dar es Salaam na nchi nzima kwa ujumla, lakini niiseme Dar es Salaam, na hasa kwenye Jimbo la Kibamba. Mheshimiwa Rais kaingiza fedha nyingi sana, zaidi ya shilingi bilioni 60 kujenga mradi wa Changanyikeni – Bagamoyo matenki zaidi ya matatu. Tenki moja la zaidi ya shilingi bilioni sita la ujazo wa lita 6,000,000 limejengwa pale Tegeta A na limekamilika. Tenki lingine la Mshikamano nililiomba hapa na Mheshimiwa Rais akawekeza fedha za Uviko, mnakumbuka ndugu zangu, zaidi ya shilingi bilioni 4.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kupitia fedha za Mfuko wa Dunia, anatumia zaidi ya shilingi bilioni 42 kujenga tenki kubwa la ujazo wa lita 9,000,000 kule Bangulo – Ilala. Hii ni fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, unaweza ukatumia fedha zote hizi, lakini bado wananchi katika viunga mbalimbali wakaendelea kulia hawana huduma ya maji. Kwa hiyo, unaweza ukakosa mantiki sasa ya kutumia fedha zaidi ya shilingi bilioni 100 halafu wananchi wasiyaone maji. Kwa hiyo, ninaomba sana Mpango huu ufikishe hii miradi ya kimkakati, *flagship project* zifike mwisho ili matokeo yake yaonekane mapema. Kama tutakuwa tunaanzisha miradi haifiki mwisho, hifadhi ya maji ni jambo moja, lakini usambazaji wa maji ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna maeneo tenki lipo kabisa hapo hapo na hapa chini ni mita 20 tu, hawana maji na ni kilio kikubwa. Achana na maji kukauka Ruvu, hiyo ni ajenda nyingine, yaani usambazaji, tunalia zaidi ya miaka miwili, mitatu, pamoja na kuwa fedha nyingi zimekwenda. Kwa hiyo, naomba sana Mpango wetu ujielekeze kwenye kumaliza miradi ya kimkakati ili

matokeo yake yakitokea ndiyo tunasema hapa tuna tija juu ya mradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la nishati ya umeme. Tuko Dar es Salaam, nilikuwa najaribu kusikiliza sana Mpango utatuambia nini juu ya kukamilisha miradi ya umeme inayoendelea? Inaizungumza sana miradi ya vijijini kupitia *REA* tunaendelea vizuri sana, lakini leo tayari tunaanza kumtafuta maskini wa vijijini, tunagombea hapa aunganishwe kwa shilingi 300,000 au kwa shilingi 27,000. Nikarudi mjini, mjini hatuna maskini? Wapo, lakini tunawatambua wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatambua kwenye programu za Serikali, mojawapo ni *TASAF*. *TASAF* inatambua maskini ambao hawana uwezo ndani ya miji na mimi ninao wengi sana. Wanatumia zaidi ya shilingi bilioni kadhaa za fedha za Serikali, lakini inavyokuja kwenye kuwaunganishia umeme, sasa mnasema wakalipe shilingi 320,000. Huku tumewatambua kama maskini, lakini tukirudi *the other way round* tunawatambua kama matajiri, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mpango ujielekeze kwenye kukamilisha huduma ya nishati ya umeme mijini na hasa kuwafuata maskini wa mijini ili sasa wote pamoja tuweze kwenda kupambana kwenye uchumi huu ambao tunaenda kuupigania kama Taifa. Nafikiri nitakuwa nimeeleweka katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la ardhi kwenye huduma hizi ambazo Mpango huu ni mwaka wa nne sasa nauzungumza, Dar es Salaam au mijini tuna nyumba kongwe, nimekuwa nikisema hapa na nimewahi kutoa mfano. Nikiwa Diwani wa Kinondoni, pale tumewahi kufanya mambo ya msingi, ndiyo maana leo tunaona nyumba kongwe, na Magomeni, zimekuwa maghorofa makubwa. Bado tunayo Tandale, kwetu kule kwa Waluguru wengi, tuna Manzese, Magomeni nyingine hii, kote kuna nyumba kongwe kabisa zimekaa pale. Watu wanasubiri wafanyiane mambo ya ovyo wafe, abaki mmoja, apige mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiende kama Taifa, tukashawishi wananchi wale waone upo uchumi wa juu? Nyumba zao zile ndogo za udongo ziko nyuma ya maduka makubwa, waweze kuingia katika makubaliano mwaachie chini na *floor* ya kwanza, kuanzia *floor* ya tatu hadi ya 10 tupeleke wananchi wengine maskini. Kesho watatusaidia kuongeza mapato kupitia kodi ya ardhi na kodi nyingine ambazo zinatokana na kuishi maisha bora na pia, kuwasaidia kutoka kwenye nyumba zile za udongo ambazo ziko nyuma ya maghorofa. Ninyi hamjui, Kariakoo hadi leo kuna nyumba za udongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watahamia kwenye nyumba nzuri za ghorofa, kama wale wa Magomeni ambao wamehamia pazuri ambapo ndugu yangu, Mheshimwia Taletale, na yeye ni mkazi. Zamani alikuwa anakaa kwenye zile nyumba ndogo ndogo, kwa hiyo, sasa hivi Mbunge wangu huyu anakaa pazuri. Nafikiri hapo ninaweza kuwa nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la pili, nilisema nitazungumzia eneo la Mheshimwia Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mapendekezo ya Mpango na Bajeti. Eneo hili ninataka niseme kidogo tu, tuna changamoto. Bajeti yetu ya Serikali ambayo tunamalizanayo muda, ya shilingi bilioni 49.3, na tunayoitarajia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anasema ni *almost* shilingi bilioni 55.06, jambo jema. Hata hivyo, nimekuwa na mashaka sana, kwa nini taasisi zetu za Serikali haziingizwi kwenye Bajeti yetu Kuu ya Serikali, hawa ambao wapo chini ya *TR*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya kampuni 340 hatuzioni moja kwa moja, eneo lao la kibajeti tunaliona kwenye zile *subvention* au fedha ambazo Serikali Kuu ita-*support* kwenye zile taasisi, lakini makusanyo yao na mambo yao mengine wanapiga moja kwa moja *at source*. Hili ni jambo ambalo haliko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza ukaona upotevu mwingine wa fedha ni watu kujiamulia kutumia fedha ambazo hazijapitishwa na Bunge letu. Kwa hiyo, ni vizuri sana, na tunataka kuamini fedha yote inayotumika kwenye nchi yetu ni ile

ambayo ina kibali cha Bunge. Sasa, kama zipo fedha zinatumika nje, ndiyo mianya ya kupoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu walisema na kunukuu vitabu vya imani, nataka niwaambie, mapato tunayoyapata kama Taifa, tukitulianayo tukayasimamia kwenye matumizi, bado yanatosha. Tutahitaji nguvu ndogo sana ya kutafuta vyanzo vingine, lakini tunaendelea kutafuta vyanzo ilhali vyanzo tulivyonavyo na mapato yanayopatikana tumeyaachia kwenye matobo mengi na zinaendelea kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo nilisema sitasema sana, hayo yanatosha. Nakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu. Tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuongea juu ya hoja ambayo iko mbele yetu. Nawapongeza Mawaziri wote, lakini zaidi nampongeza Mheshimiwa Rais wetu na jemedari wetu mkuu kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika kujenga uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma Mpango ambao umewasilishwa na Mheshimiwa Waziri, Prof. Mkumbo. Nilisoma ukurasa wa 27 na ninaomba ninukuu. Ameandika kwamba, "Sensa ya 2022 imeonesha idadi ya watu inakua kutoka milioni 44, Sensa ya 2012 na sasa imekwenda watu milioni 61 kwa Sensa ya 2022." Hata hivyo, kukua kwa watu kunaongezeka kwa 3.2%, lakini uchumi wetu unakua kwa asilimia tano kwa mwaka. Profesa amekiri kwamba, ili kuhimili ongezeko la watu, uchumi wetu inabidi ukue kuanzia asilimia nane mpaka 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, andiko lake limeendelea kudadavua kwamba, ifikapo mwaka 2035 Tanzania itakuwa na watu zaidi ya milioni 85. Ongezeko hili la watu tusipoamua kupanga leo, mbele ya safari tunakwenda kupoteana. Mchungaji Baba Askofu wakati anachangia hapa, ameongelea masuala ya

kupanga. Pia Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hoja hii wameongelea faida ya kupanga na hasara za kutokupanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuziba pengo hili la ongezeko la watu na kukua kwa uchumi tunahitaji kujizatiti leo, tusisubiri kesho. Baba Askofu ni rafiki yangu, wakati anachangia ameongelea kwamba tunaagiza nje vitu vingi na tuna ugonjwa huo kama Taifa. Tuna ugonjwa wa kupenda kuagiza hata vitu ambavyo tungeweza kuvizalisha hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma kwenye taarifa moja, mwaka 2023 Tanzania pamoja na kujaliwa maziwa mengi, kila kona ya Taifa hili tuna maziwa, mabwawa, Ziwa Tanganyika lipo, Ziwa Victoria ninapotoka lipo, Nyasa lipo, Nyumba ya Mungu, maziwa na mabwawa ni mengi sana, lakini cha ajabu mwaka 2023 Serikali imeagiza samaki kutoka nje ya nchi wenye thamani ya dola 330,000 kutoka China na wapi huko nje ya nchi wakati tuna maziwa, yamejaa samaki na kila mazao ya samaki. Ni aibu. *(Makofi)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumjulisha mwongeaji, Daktari Msomi kwamba, hapo bandarini sasa hivi kuna samaki ambao wanatoka Indonesia tumewaagiza waje wauzwe hapa kwetu Dar es Salaam. Sasa, hii hali dalili yake ni mbaya sana. Ninamjulisha mwongeaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ni Taarifa, naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo kama tukipanga ipasavyo sekta ya uvuvi…

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia na kutoa Taarifa. Hoja aliyoichangia Dkt. Kikoyo ni nzuri na baadaye ikapata Taarifa kutoka kwa Askofu Gwajima. Ukweli ni kwamba, hiki alichokisema Askofu Gwajima ni kweli, Bandari ya Dar es Salaam utakuta *containers* za samaki, lakini hizo *containers* siyo *for local consumption* ya hapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.* Hizo ni *transit. I tell you* ni *transit,* kwa sababu gani? Mpaka sasa hivi sisi kilo moja ya samaki *imported* Tanzania ni dola 2.5. Sasa ibadilishe dola 2.5 iweke katika *Tanzanian Shillings,* ili upate kilo moja ya hao samaki watakuwa ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hailipi kwa sababu, sasa hivi sato anayetoka Mwanza anapofika Dar es Salaam au hapa Dodoma atauzwa shilingi 10,000 au shilingi 8,000 au shilingi 9,000, akizidi sana ni shilingi 12,000. Sasa chukua 2.5 tunayoitaka sisi Serikali, zidisha mara fedha ya Kitanzania, halafu jumlisha na gharama nyingine utaona kwamba, hiyo ni biashara isiyolipa. Mtu anayeleta samaki Tanzania leo, maana yake ameji-*risk* kuweza kulipa fedha nyingi sana katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho kwa kuwa, nitapata nafasi ya kuchangia, nitawaeleza Waheshimiwa vizuri, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo na Mheshimiwa Askofu Gwajima ili wapate *numbers* vizuri na kwa ufasaha zaidi, ili kesho na kesho kutwa watakapokuwa wanachangia wachangie kwa uhakika na kwa manufaa mapana sana ya Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba uniongezee muda niweze kumalizia mchango wangu. Ninachotaka kusema ni kwa nia njema kwamba, hizi sekta za kiuchumi ambazo ni uchumi jumuishi, kama uvuvi na kilimo, katika Mpango wa muda mfupi ni sehemu ambazo naomba na kuishauri Serikali ikaelekeze fedha huko, ili vijana wengi ambao wanakimbizana mitaani kutafuta ajira, tukawekeze kule, waweze kuchangia pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kusema kweli imetutoa matongotongo machoni. Mradi wa *SGR* ambao sasa tunasafiri kwa haraka kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, tulizoea kutumia saa nane mpaka tisa kwa magari yetu, wengine wataamua watapanda ndege saa moja, lakini kwa kukamilisha huu mradi tumejenga historia ambayo haitafutika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Uchukuzi sasa iharakishe mchakato wa kuhamisha mzigo kutoka barabara inayotoka Bandari yetu ya Dar es Salaam angalau tuanze kui-*clear* hapa Dodoma kupunguza *congestion* kwenye barabara yetu ya Morogoro – Dodoma, ili iweze kupumua. Pia, tupunguze hata matumizi ya mafuta na dizeli ambayo tunayaagiza kwa bei kubwa kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sekta ya uvuvi. Leo nilikuwa naongea na wavuvi wetu huko Kagera na sisi pato letu kubwa linatokana na Ziwa Victoria, wananchi wanalalamika kwamba, sasa hivi samaki hawapatikani, ni kazi kubwa kupata dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru mjomba, Mheshimiwa Waziri Ulega, alipokuwa Muleba aliagiza nyavu na vifaa vyote vinavyotumika kuvua ambavyo vilikuwa vinaitwa haramu visiteketezwe bali wakamatwe na waelekezwe jinsi ya kupata nyavu nzuri na zinapatikana wapi? Namshukuru Mheshimiwa

Waziri na kazi hiyo inaendelea na wananchi wetu wa Muleba wanakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo tulilonalo ni kwamba, wanapolalamika na wenyewe wana majibu wanasema, samaki hawapatikani kwa sababu kuna mwanga mkubwa sana unaotokana na uvuvi wa dagaa. Kweli ukipita, mimi ambaye ninapita pale usiku, ukiangalia ziwani utadhani ni mji sijui wa wapi, labda Chicago huko, taa ambazo zipo ziwani ni nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua, tunaomba utusaidie kwa sababu, ziwa letu sisi ndiyo machimbo yetu. Kagera hatuna dhahabu na almasi. Almasi na dhahabu yetu ni Ziwa letu Victoria. Tunaomba mtusaidie, ili vijana wetu waendelee kutengeneza fedha, kutafuta uchumi na kuchangia pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo. Waheshimiwa tumemaliza wachangiaji wa leo.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile hatuna matangazo ya aina yoyote kwa sasa hivi na kazi zetu zimeisha, basi nawatakia jioni njema na ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.06 Usiku, Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 7 Novemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*